

**MTINDO KATIKA WATU WA *GEHENNA***

Na

**Janepher Barasa Murumba**

**C50/69101/2011**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO KIKUU  
CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA 2013**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote.

**Jina :** **Janepher Barasa Murumba**

Sahihi: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Jina :** **Dkt. Amiri Swaleh**

Sahihi: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

**Jina :** **Dkt. Mwangangi wa Musyoka**

Sahihi: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

## **TABARUKU**

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu: Raymond Barasa Makhanu na Florah Gweyani Barasa kwa juhudi zao za kunilea, kunielimisha, kunifunza haja ya uvumilivu na kujitolea maishani. Waliniunga mkono na kunishauri kwa lolote nililoazimu kulifanya. Wamekuwa kielelezo bora na kunifunza umuhimu wa elimu maishani.

## SHUKRANI

Ninakiri kwamba kazi hii haingeweza kukamilika bila ya usaidizi, uongozi na mchango wa watu wengi. Ni vigumu kuwataja wote; hata hivyo, nitawataja wachache. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia hekima, afya na uwezo wa kuifanya kazi hii.

Pili, ninatoa shukrani maalum kwa wasimamizi wangu Dkt. Amiri Swaleh na Dkt. Mwangangi wa Musyoka kwa kunisimamia bila ya kuchoka muda wote nilipokuwa nikifanya kazi hii. Walinipa moyo katika kila hatua za kazi hii na kupitia kila sehemu kwa haraka na kwa makini ili kuniwezesha kukamilisha utafiti wangu kwa wakati. Mawaidha yao mema na ya kitaalamu yalinitia ari na mshawasha wa kuwaza zaidi katika kuboresha kazi hii. Uongozi wao wa busara, masahihisho na ushauri wa dhati umenisaidia kukamilisha kazi hii. Mungu awabariki nyote.

Shukrani zangu pia nazitoa kwa wahadhiri walionifunza katika Idara ya Isimu na Lugha ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Walinisaidia, wakaniongoza na kunielekeza katika safari hii ya usomi ambayo haikuwa rahisi. Hawa ni: Prof. John Habwe, Prof. K.W. Wamitila, Prof. Mohamed Abdulaziz, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Omboga Zaja, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Alfred Buregeya, Bw. Basilio Mungania, Dkt. Tom Olali na Dkt. Ayub Mukhwana.

Shukrani zangu pia ziwaendee wenzangu ambao tuliabiri jahazi moja la kutafuta shahada ya uzamili na kuhakikisha tumefika mwisho wa safari hii pamoja. Tulihimizana na kusaidiana kwa kila hali ili kuhakikisha kuwa hakuna mmoja wetu angelemewa na safari hii. Tuliokuwa nao ni pamoja na: Elizabeth Yego, Jedidah Mwangi, Alice Ochichi na Aziza Omara. Nawaombea dua njema katika kila mlitendalo.

Sitamsahau mume wangu, John na watoto wangu Stephen, Philip na John Paul pamoja na Nancy Barasa ambao walinifaa pakubwa kwa kunipa moyo na kuipiga chapa kazi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mungu awabariki.

Hatimaye ninatoa shukrani zangu kwa marafiki zangu hususan Everlyne Were ambao walinifaa kwa mijadala na vitabu katika ufanisi wa mradi huu. Hawa wote niliowataja na wengine ambao sikuwataja nawashukuru kwa kunifaa katika kufanikisha kazi hii. Mungu awabariki nyote.

## YALIYOMO

Mada -----	i
Ungamo -----	ii
Tabaruku -----	iii
Shukrani -----	iv
Yaliyomo -----	v
Orodha ya vifupisho -----	ix

### **SURA YA KWANZA: PENDEKEZO LA UTAFITI**

1.0 Utangulizi -----	1
1.1 Tatizo la utafiti -----	1
1.2 Madhumuni ya utafiti -----	2
1.3 Maswali ya utafiti -----	2
1.4 Sababu za kuchagua mada -----	2
1.5 Upeo na mipaka ya utafiti -----	3
1.6 Misingi ya Nadharia -----	4
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada -----	26
1.8 Njia za utafiti -----	28
1.9 Hitimisho -----	29

**SURA YA PILI: UHUSIKA NA WAHUSIKA KATIKA WATU WA  
*GEHENNA***

2.0	Utangulizi -----	30
2.1	Uhusika na wahusika -----	30
2.2	Usawiri wa wahusika -----	32
2.3	Mbinu za kuwasawiri wahusika -----	33
2.4	Makundi ya wahusika katika <i>Watu wa Gehenna</i> -----	37
	2.4.1 Wahusika wakuu -----	38
	2.4.2 Wahusika wadogo/ wasaidizi -----	49
2.5	Hitimisho -----	68

**SURA YA TATU: UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA WATU WA *GEHENNA***

3.0	Utangulizi -----	70
3.1	Tamathali za usemi -----	70
	3.1.1 Sitiari -----	72
	3.1.2 Jazanda -----	75
	3.1.3 Tashbihi -----	79
	3.1.4 Kinaya/kejeli -----	82

3.1.5	Taswira -----	86
3.1.6	Tashihisi -----	89
3.1.7	Maswali ya balagha -----	90
3.1.8	Takriri -----	92
3.2	Hitimisho -----	95

## **SURA YA NNE: MANDHARI NA USIMULIZI**

4.0	Utangulizi -----	96
4.1	Dhana ya mandhari -----	96
4.2	Aina za mandhari katika <i>Watu wa Gehenna</i> -----	98
4.2.1	Mandhari ya kijiografia/ halisi-----	98
4.2.2	Mandhari ya kinjozi -----	100
4.3	Muundo wa masimulizi -----	106
4.3.1	Utangulizi -----	106
4.3.2	Usimulizi ngazi -----	107
4.3.3	Usimulizi wa nafsi ya tatu -----	108
4.4	Hitimisho -----	112

## **SURA YA TANO: HITIMISHO**

5.0	Utangulizi -----	114
5.1	Muhtasari wa matokeo ya utafiti -----	114
5.2	Ufaafu wa Nadharia -----	117
5.3	Mapendekezo -----	118
	MAREJELEO -----	120

## **ORODHA YA VIFUPISHO**

Dkt.	-	Daktari
k.m.	-	kwa mfano
k.v.	-	kama vile
n.k.	-	na kadhalika
Prof.	-	Profesa
TUKI	-	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TY.	-	Tafsiri yangu
u.k.	-	ukurasa

## **SURA YA KWANZA: PENDEKEZO LA UTAFITI**

### **1.0 UTANGULIZI**

Katika sura hii, tumeshughulikia pendekezo la utafiti wetu. Kwanza, tulieleza tatizo la utafiti wetu pamoja na kutoa madhumuni ya utafiti huu ili kubainisha malengo yetu. Tumeshughulikia maswali ya utafiti wetu ambayo ndiyo mihimili ya utafiti huu. Vilevile, tumefafanua sababu za kuchagua mada hii pamoja na kueleza upeo na mipaka ya utafiti wetu. Kufuatia, tumebainisha misingi ya nadharia tulizozitumia na yale yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Tumehitimisha faslu hii kwa kueleza njia tulizotumia katika utafiti wetu.

### **1.1 TATIZO LA UTAFITI**

*Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) ina mtindo unaojibainisha kwa matumizi ya vipengele mbalimbali vya fani kama usimulizi, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha na ploti changamano.

Tatizo la utafiti huu lilikuwa kuchambua vipengele mahsusi vya kimtindo vinavyodhihirika katika riwaya hii na kutoa maelezo ya jinsi vinavyoathiri muundo wake na vinavyochangia uwasilishaji wa ujumbe.

Tulichunguza jinsi wahusika walivyosawiriwa na kutumiwa kukuza ujumbe. Kwa ujumla, utafiti huu ulichunguza vipengele vya kimtindo kwa pamoja katika riwaya hii na jinsi vinavyochangia ukamilifu wake. Hatimaye, tulichunguza namna mwandishi anavyotumia mtindo katika kukuza na kuendeleza ujumbe wake.

## **1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI**

Yafuatayo ni malengo ya utafiti huu:

- i. Kubainisha jinsi vipengele vya mtindo vilivyotumiwa katika *Watu wa Gehenna* vinavyoathiri muundo wake.
- ii. Kuchunguza jinsi mtindo wa riwaya hii unavyoathiri uwasilishaji wa maudhui/ ujumbe.
- iii. Kuchanganua mtindo wa *Watu wa Gehenna* ili kuiainisha riwaya hii.

## **1.3 MASWALI YA UTAFITI**

- i. Vipengele mbalimbali vya mtindo vinavyojitokeza katika *Watu wa Gehenna* vinaathiri vipi muundo wake?
- ii. Mtindo wa riwaya hii unaathiri vipi uwasilishaji wa ujumbe?
- iii. Mtindo wa *Watu wa Gehenna* unachangia vipi motifu ya uhalisiajabu?

## **1.4 SABABU ZA KUTEUA MADA**

Tumechagua mada hii kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, katika usomaji wetu wa *Watu wa Gehenna*, tumegundua kwamba, kazi hii imekiuka baadhi ya kaida za uandishi zilizozoeleka katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili. Mifano ya ukiushi huu ni katika ngazi za wahusika, matumizi ya lugha, usimulizi, mandhari na msuko. Pia, riwaya nzima ina matukio ya kiajabuajabu na ya kifantasia/ kinjozi. Kutokana na ugunduzi huu, tulipata msukumo wa kuihakiki kimtindo tukiwa na malengo kuwa matokeo ya utafiti huu yatawezesha uelewekaji wa riwaya ya kiuhalisiajabu, na watafiti wengine wataweza kuihakiki katika vipengele tofauti.

Vilevile, matokeo haya yatawawezesha watafiti wa baadaye kuhakiki kazi nyingine zenye mwelekeo wa kiuhalisiajabu; iwe ni riwaya, tamthilia, hadithi fupi au ushairi.

Sababu nyingine ni kwamba, hii ni riwaya iliyochapishwa hivi karibuni na uhakiki wa vipengele tofauti vya mtindo haujafanywa. Hakuna tafiti tunazozijua ambazo zimefanywa kuhusu *Watu wa Gehenna*. Hili ni kutokana na usomaji wetu wa makala na tasnifu mbalimbali maktabani na kwenye tovuti. Kwa hivyo, utafiti wetu utawafaidi wasomaji na watafiti, na kuchangia pakubwa uhakiki wa riwaya na fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

Tatu, tulipata msukumo wa kuichagua mada hii kwa sababu kuna pengo la kiuhakiki ambalo tulidhamiria kuliziba hasa kutokana na mapendekezo ya tafiti za awali kuhusu riwaya za kimajaribio. Kutokana na utafiti wa Nyabunga (2005), “Uhakiki wa *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) za K.W. Wamitila”, aliyependekeza kuwa, watafiti wengine washughulikie kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili na kuzihakiki kwa kutumia Nadharia ya Uhalisiajabu. Kwamba, utafiti huo unaweza kulenga riwaya nyingine, hadithi fupi, mashairi au hata tamthilia za Kiswahili. Mapendekezo hayo ni kati ya mambo yaliyotupa msukumo wa kiuhakiki riwaya ya *Watu wa Gehenna* kimtindo. Kwa hivyo, utafiti wetu unadhamiria kukuza na kupanua uelewekaji wa riwaya na fasihi ya Kiswahili kwa jumla. Uhakiki wetu utakuwa changamoto kwa wahakiki na wasomi wa baadaye wa fasihi ya Kiswahili kuvihakiki vipengele vingine vya riwaya mpya.

## **1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI**

Utafiti huu umejikita katika riwaya moja ya Kiswahili ambayo ni *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Katika riwaya hii, tumechunguza kipengele cha fani hususan ngazi ya

wahusika, tamathali za usemi, usimulizi na mandhari. Tumechunguza sifa za kimtindo katika kiwango cha wahusika kwa kuthibitisha kuwa usawiri wao hauzingatii misingi ya jadi ya kuwasawiri kama binadamu halisi. Hali kadhalika, tumetathmini jinsi usimulizi na mandhari mbalimbali yanavyoendeleza ujumbe katika riwaya inayohusika. Pia, tumechunguza jinsi matumizi ya lugha katika riwaya hii yanavyokiuka kaida zilizozoeleka; na tamathali za usemi zilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe.

Utafiti wetu umeegemea pakubwa riwaya ya *Watu wa Gehenna* kwa sababu ina masuala ya kutosheleza malengo yetu. Hata hivyo, kuna riwaya nyingine, tamthilia, hadithi fupi au mashairi yanayoweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia za Umitindo na Uhalisiajabu. Tumezirejelea na kunukuu kazi hizo iwapo zinachangia katika ukuzaji na uendelezaji wa mada yetu.

## **1.6 MISINGI YA NADHARIA**

Nadharia ambazo tunaamini zimeafiki utafiti huu ni Nadharia ya Elimumitindo (Umitindo) na Nadharia ya Uhalisiajabu. Tumezitumia nadharia hizi mbili katika kuishughulikia mada yetu ili kuafikia malengo tuliyoyataja awali.

### **1.6.1 NADHARIA YA UMITINDO**

#### **1.6.1 Utangulizi**

Mjadala mkubwa umekuwepo kuhusu maana ya istilahi “mtindo”, ingawa istilahi hii imetumiwa sana katika uhakiki wa fasihi na hasa Elimumitindo. Huwa inatumiwa katika miktadha mipana. Katika ujumla wake, neno “mtindo” hutumiwa kurejelea “jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani, na mtu fulani na kwa lengo fulani” (Leech na Short 1981:10). Ili kufafanua dai hili, tutarejelea maelezo ya mwanaisimu wa Kiswisi

Ferdinand de Saussure<sup>1</sup> aliyetofautisha dhana za “langue” na “parole” kwa kurejelea lugha. Maneno haya hayana visawe katika Kiswahili.

Kwa mujibu wa de Saussure, “langue” ni utaratibu mzima wa kanuni za lugha zinazojulikana na wazungumzaji wa lugha husika, yaani, ni mfumo wa lugha ya jamii inayohusika. “Parole” ni matumizi ya utaratibu wa lugha ya mzungumzaji binafsi. Ni uteuzi wa kanuni ambazo msemaji huzitumia katika uandishi na uzungumzi wake. Kwa hivyo, mtindo ni kama “parole” kwa kuwa ni uteuzi kutoka katika utaratibu wa kanuni zilizoko za lugha. Kwa muhtasari, lugha inayojulikana na wazungumzaji (“langage”) inaundwa kutokana na kanuni za lugha “langue” pamoja na matumizi yake katika mazungumzo na maandishi ‘parole’. (Chapman 1973:9, Kitsao 1975:8-11, Leech na Short 1981:10-11 na Wales 1990:287).

Mtindo unaweza kuhusishwa na lugha iliyoandikwa, lugha ya kifasihi na isiyokuwa ya kifasihi ingawa kwa kawaida unahusishwa na matini za kifasihi zilizoandikwa. Katika uandishi wa fasihi, mtindo hutumiwa kwa maana nyingi: ni mazoea ya lugha kama wanavyosema wana-umitindo Crystal na Davy (1969:9-10). Huweza kuhusisha mazoea ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha. Hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza, wa kutoa hotuba hadharani, n.k. Mtindo ni upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Ni jinsi waandishi huandika na pia ni njia tofauti za watu wanavyozungumza au kuandika katika miktadha ya kawaida ya kila siku.

---

<sup>1</sup> Ferdinand de Saussure ndiye mwasisi wa Nadharia ya Umuundo, aliyebuni dhana za ‘langage’, ‘langue’ na ‘parole’. Dhana hizi hazina tafsiri katika Kiswahili.

Vilevile mtindo ni ukiushi katika matumizi ya lugha, iwe ni ya kifasihi au isiyo ya kifasihi. Huhusisha ukiushi kutoka kaida za lugha ambazo zimezoeleka au za kimapokeo. Ukiushi huu pia hujitokeza katika matumizi ya rejesta au sajili mbalimbali za lugha (McIntosh 1963:243; Kitsao 1975:17; Leech na Short 1981: 38-39 na Wales 1990:371-372).

### **1.6.1.1 Nadharia ya Umitindo**

Mwasisi wa Nadharia ya Umitindo ni Geoffrey Leech ambaye alipokuwa akiandika tasnifu yake ya uzamili, alipenda lugha ya Fasihi, ambayo kwayo aliandika makala mbili, mnamo mwaka 1965 na mwaka 1966. Kwa mara ya kwanza, kutokana na kazi hizi za Leech, isimu ya kisasa ilihusishwa na usomaji/ufundishaji wa lugha ya fasihi. Mtazamo huu ulizua kutokuelewana na hata ugomvi baina ya wasomi wa fasihi na wa isimu. Ni wakati huu ambapo Leech alionelea mwafaka upatikane baina ya mitazamo-husika miwili; wa kiisimu na ule wa kifasihi.

Kwa hivyo, kutokana na maoni ya wanaisimu na wahakiki walioshikilia kuwa taaluma hizi mbili; uhakiki wa kifasihi na kazi za kiisimu hutofautiana na kuwa hazina uhusiano wowote, Leech alipata motisha wa kuandika kitabu chake, *A Linguistic Guide to English Poetry* (1969) ambamo alishughulikia suala la mtindo katika kuchanganua matini za kifasihi. Leech alipata msukumo mkubwa pia kutoka kwa Nowotny (1962) na Quirk (1985)<sup>2</sup>.

---

<sup>2</sup> Quirk R. et al (1985). *A Comprehensive Grammar of the English Language*. London: Longman.

Leech (1969:2) anasema yafuatayo kuhusu umitindo:

Elimumitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu. Kama taaluma, inafungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinyume, kinaya/kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu, elimumitindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa.(TY)

Kulingana na Leech, malengo ya stadi za Elimumitindo ni fasihi pamoja na maumbo mengine ya matini zilizoandikwa katika nyanja za matangazo ya biashara, utamaduni, siasa au dini. Kwamba, umitindo pia hujaribu kubainisha kanuni za kuelezea uteuzi mahsusi unaofanywa na wahusika katika matumizi yao ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi.

Sifa nyingine za umitindo alizozitaja Leech ni pamoja na matumizi ya dayalojia au mazungumzo yanayohusisha lafudhi za kimaeneo na lahaja za wazungumzaji, lugha elezi na sarufi km. sauti, urefu wa sentensi na rejesta. 'Elimumitindo' ni istilahi inayoweza kutumiwa kubainisha uhusiano uliopo baina ya umbo na athari zake katika kiwango fulani cha lugha.

Akizungumzia lugha katika Fasihi, Leech anasema kuwa, athari ya matini yoyote ile huamuliwa kwa kiasi kikubwa na mtindo. Kwamba, mtindo ni njia na jinsi lugha inavyotumiwa, nao mtindo haujabanwa tu katika fasihi, ila ni sehemu ya usemi wowote ule kwa sababu katika kila muktadha, msemaji huchagua jinsi ya kuzungumza.

Kwa muhtasari, Umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi wa matini za kifasihi kwa kuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi - yenye nidhamu na taratibu za kitaaluma; na huweza kuelezwa kama nadharia iliyo katikati ya isimu na fasihi. Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa kinachosemwa (maudhui) na jinsi kinavyosemwa (fani). Nadharia ya Elimumitindo imepitia hatua kadha kufikia sasa.

Wamitila (2003:39) anasema:

Dhana hii hutumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa lugha na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Ni taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi au jinsi lugha inavyotumiwa katika matini au kazi za kifasihi. Elimumitindo huweza kuhusisha uchunguzi wa sifa za kimitindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Wamitila anaunga mkono madai ya Leech kwamba, Nadharia ya Umitindo ni mwafaka katika kuhakiki kazi za kiisimu pamoja na za kifasihi. Huwezesha kuchunguza jinsi

lugha ilivyotumiwa katika matini za kifasihi, na hivyo basi, kuwezesha uchanganuzi wa vipengele vya fani na maudhui.

Kwa kuchangia dhana ya Umitindo, Crystal na Davy (1969:10) wanasema hivi:

Lengo la Umitindo ni kuchanganua tabia za lugha kwa madhumuni ya kubainisha sifa mahsusi zinazobanwa katika miktadha maalum kutoka kwa sifa za kijumla za kiisimu ambazo hupatikana katika kila muktadha wa matumizi ya lugha<sup>3</sup>. (TY)

#### **1.6.1.2 Viwango katika uchanganuzi wa Nadharia ya Umitindo**

Nadharia ya Umitindo ina viwango ambavyo humwezesha mchanganuzi wa matini ya kifasihi kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. Leech (1969:42) anaorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambao hutokea katika mtindo wa kazi za kifasihi. Viwango vya ukiushi ni hivi vifuatavyo:

- (i) Ukiushi wa kimsamiati/kileksia
- (ii) Ukiushi wa kisarufi
- (iii) Ukiushi wa kilahaja
- (iv) Ukiushi wa sajili/rejesta
- (v) Ukiushi wa kifonolojia
- (vi) Ukiushi wa kimaandishi/kigrafolojia
- (vii) Ukiushi wa kimapisi/kihistoria
- (viii) Ukiushi wa kisemantiki

---

<sup>3</sup> Tasnifu ya uzamili ya Jay Kitsao (1975 uk. 19)

Simpson (2004) anaorodhesha na kufafanua vipengele vya kimsingi ambavyo vinafaa kuchunguzwa katika kazi za kifasihi na mhakiki ambaye anatumia mwelekeo wa kihakiki wa Mitindo. Vipengele hivyo vya Simpson vinafafanuliwa na Wamitila (2008) ambaye pia anachangia pakubwa nadharia hii ya Umitindo. Mambo haya ni lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo; muwala, mshikamano na mtindo; na mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

Yafuatayo ni mambo muhimu yanayopaswa kuchunguzwa katika matini kwa kutegemea Nadharia ya Umitindo kama wanavyoeleza Leech (1969), Simpson (2004) na Wamitila (2008).

### **1.6.1.3 Kiwango cha Maandishi au Grafolojia**

Pia huitwa kiwango cha utendaji. Kiwango hiki kinahusisha vipengele vya kifonetiki, kifonolojia na kigrafolojia. Kinahusu jinsi lugha inavyotamkwa na kuandikwa.

Kwa kawaida, kila kazi ya fasihi huwa katika maandishi fulani na mahsus tena huwa katika abjadi zinazoeleweka na kuzoeleka na walengwa. Hata hivyo, matini za kifasihi huweza kuwa na sifa za kimaandishi ambazo zinachimuzwa na hivyo kutilia uzito kiwango hiki cha ukiushi.

Ukiushi huu unahusu mambo yafuatayo; kubadilisha matamshi ya maneno k.v miujiza liwe “miuza”; matumizi ya herufi kubwa kwa njia isiyo ya kawaida; kutumia herufi ndogo mahali pa herufi kubwa; matumizi ya herufi za mlazo/italiki; mpangilio wa aya (au ukosefu wake) na matumizi ya viwakifishi kama koma, alama ya hisi, koloni, na vistari (Leech 1969, Wamitila 2008:512).

#### **1.6.1.4 Kiwango cha Umbo**

Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati unaotumiwa. Kwa kuwa fasihi inatumia lugha kujieleza, vipengele ambavyo huhusishwa katika uteuzi huu ni vingi. Kuna kiwango cha kimsamiati (kileksia), matumizi ya lahaja, na kiwango cha rejesta/sajili (yaani, jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha maalum). Ukiushi wa kimsamiati unahusu yafuatayo: kubuni maneno mapya kwa kutumia minyambuliko isiyo ya kawaida na ubunaji huu hutokea kwa kutofuata kanuni za kisarufi km. maskini – ‘maskinisha’, dhambi – ‘ikanidhambi’. Pia kuna matumizi ya maneno ya kale/kizamani km. kutumia *munyu* (chumvi), *swi* (samaki) na *nyuni* (ndege); matumizi ya inkisari na mazida; kuchanganya ndimi/ kuhamisha ndimi na matumizi ya maneno ya kigeni kama ya Kiingereza au Kilatini.

Suala la uteuzi halihusishwi na maneno peke yake. Mwandishi pia anafanya uteuzi wa wahusika anaowatumia kwenye kazi yake; usimulizi anaoutumia na mtazamo wake; na mada anayoishughulikia. Kwa mfano, uteuzi wa mhusika anayepatikana katika mazingira au muktadha maalum unamaanisha kuwa lazima lugha yake iafikiane na mazingira hayo.

#### **1.6.1.5 Kiwango cha Kisarufi**

Kiwango hiki ni nguzo ya matamshi ya kiisimu na ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Huwa inajumlisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia. Hushughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kubainisha visehemu vyake ambavyo huwa na dhima maalumu. Ukiushi huu huhusisha masuala kama kubananga sarufi; matumizi ya anafora - neno moja kuanza kila mstari hasa katika nyimbo na mashairi na kurudiwarudiwa kwa sentensi au kifungu. Huwepo pia, ukiushi wa kilahaja

na matumizi ya rejesta/sajili. Kwa ujumla, huzingatia ukiushi katika muundo wa kawaida wa matumizi ya lugha, urefu wa sentensi (fupi au ndefu) na sentensi zenye dosari. (Leech 1969 na Wamitila 2008:512).

#### **1.6.1.6 Kiwango cha Kisemantiki**

Kiwango hiki kinahusu lugha ya kitamathali na miundo ya lugha ambayo ni sifa muhimu ya kuchunguza matini ya kifasihi tunapotumia nadharia ya Umitindo. Ni matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa aina hii unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi; mbinu ya kinaya/kejeli; mbinu ya kweli-kinzani (paradoksi); mbinu ya oksimora (tanakuzi) km. anwani *Kiza katika Nuru* ya S.A. Mohamed; na mbinu ya sitiari k.m ujana ni moshi. Pia, huhusisha matumizi ya jazanda, yaani lugha ya picha aidha za kimaelezo au za kiishara (ambazo si taswira au picha tu bali zina ujumbe wa ziada) (Wamitila 2008:518).

#### **1.6.1.7 Mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo**

Katika kiwango hiki, mhakiki wa kimitindo anafaa kuchunguza mazungumzo au usemezano baina ya wahusika na mbinu nyingine ambazo zinatumiwa katika mazungumzo hayo kwa lengo la kuwasilisha usemi na mawazo ya wahusika (Wamitila 2008:519).

Kwa mujibu wa Ngara (1982), wahusika wa riwaya wanawakilisha matumizi ya lugha ya kawaida katika jamii kama binadamu wa kawaida. Aghalabu, binadamu hutumia lugha kwa njia ambazo zinatofautiana katika viwango vya misamiati, miundo ya

sentensi, mkazo, n.k. Tofauti hizi za kimatumizi zinapaswa kuonekana katika tungo za kifasihi hususan riwaya.

Ni jukumu la mhakiki kuangazia tofauti zilizoko katika matumizi ya lugha miongoni wa wahusika. Ikiwa wahusika ni wasomi au walioelimika huenda wakaongea Kiswahili sanifu kutokana na athari za elimu waliyopata. Wenye elimu ndogo huenda wakaathiriwa na lugha ya kwanza, na watumie lafudhi. Huwepo matumizi ya lugha za kigeni kama Kiingereza na Kilatini. Kulingana na Ngara (1982), huku kutofautisha wahusika katika misingi ya matumizi ya lugha ni sifa nzuri ya uandishi; na matumizi yao yanaakisi matumizi ya lugha katika jamii.

#### **1.6.1.8 Usimulizi au Muundo wa Masimulizi**

Usimulizi hurejelea hali ya kuwepo hali au matukio katika hadithi yanayosimuliwa, na kuleta mabadiliko. Uchunguzi wa muundo wa usimulizi unahusika kimsingi na uchunguzi wa ploti au msuko wa kazi husika. Matukio na visa katika matini ya kazi ya kifasihi lazima yafuate ruwaza fulani. Msuko huweza kuwa wa moja kwa moja au changamano. Mpangilio wa matukio huendana na wakati toka mwanzo hadi mwisho; au huwepo mpangilio wa kwenda mbele na nyuma (mbinu rejeshi).

Vilevile kuna utoaji wa maelezo/masimulizi. Mara nyingi, huwepo sauti inayotoa masimulizi aidha ya mwandishi au ya mhusika mmojawapo. Masimulizi huweza kutolewa katika nafsi ya kwanza, au katika nafsi ya tatu ambapo mhakiki atabainisha sifa hizi za kimtindo na athari inayoleta kwa wanaosimuliwa. Mara nyingine nafsi zote mbili (ya kwanza na ya tatu) hutumiwa ili kuleta athari fulani, kwa mfano, *Nguvu ya Sala* ya K.W. Wamitila (1999).

Kimsingi, matini za kifasihi huwa na muundo wenye sehemu tatu: mwanzo ambao ndio unaoelekeza kwenye mfuatano wa kiwakati. Jukumu la mwanzo ni mfichuo wa mhusika au dhamira. Kwa kawaida, mfichuo huweza kuwa mwanzoni, wa hatua kwa hatua (unaotokeza kwenye sura tofauti tofauti), mfichuo uliokawizwa na mfichuo ulioahirishwa; kisha sehemu ya kati (kiini), na mwisho ambao una utatuzi wa tatizo kuu ambalo ndilo kiini cha mgogoro (Simpson 2004:18 na Wamitila 2008:515-516).

#### **1.6.1.9 Itikadi, mtazamo na mtindo**

Mwandishi huchukua mkabala fulani kuhusu anayoyazungumzia na mtazamo huu unaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye upokezi wa maneno anayoyasema au jinsi mlengwa anavyoyaelewa au kukipokea kisa kinachosimuliwa. Mtazamo ni dhana muhimu katika uchanganuzi wa mitindo ya matini. Vilevile, ni muhimu kuchanganua mwelekeo wa kimsimamo au kimawazo (yaani itikadi) unaochukuliwa na msimulizi wa kazi inayohusika. Lugha huwa ni nyenzo muhimu ya kubainisha au hata kuchimuza itikadi hiyo. Mchanganuzi wa kimitindo anastahili kuchunguza jinsi uteuzi wa maneno au uteuzi wa kiisimu unavyochangia katika kuiangazia itikadi hiyo (Wamitila 2008:519-520).

#### **1.6.1.10 Ufaafu wa Nadharia ya Umitindo**

Kama tulivyoona hapo juu, suala la mtindo katika fasihi ni pana na Nadharia ya Umitindo ina viwango vingi vya kuweza kuchanganulia matini za kifasihi. Hata hivyo, ili kushughulikia uhakiki wetu wa kifani katika *Watu wa Gehenna* vyema, hatukutumia

vigezo vyote ila tuliteua baadhi tu ya vipengele ambavyo vinafaa katika kushughulikia mada yetu na kuvichunguza kwa undani.

Kwa kuwa utafiti huu unahusu matini ya kifasihi, tunadhamiria kuchunguza vipengele vya tamathali za usemi na kileksia, mazungumzo (uhusika na wahusika) na usimulizi katika muktadha wa kimtindo. Vipengele hivi vina nafasi kubwa katika riwaya tunayoishughulikia.

### **1.6.2 NADHARIA YA UHALISIAJABU**

Kulingana na maelezo ya Zamora (1995), Nadharia ya Uhalisiajabu ilianza mwaka wa 1925. Matumizi ya istilahi “uhalisiajabu” inahusishwa na msanii wa Kijerumani, Franz Roh aliyeshi kati ya mwaka 1890 na 1965 nchini Ujerumani. Roh alisomea katika vyuo vikuu vya Leipzig, Berlin na Basel. Mnamo mwaka 1920, Roh alipata shahada yake ya uzamifu (PhD) huko Munich kutokana na kazi yake iliyohusu “Michoro ya Kidachi ya karne ya 17”.

Mnamo mwaka wa 1925, Franz Roh aliandika na kuchapisha makala kuhusu sanaa ya uchoraji aliyoyaita, “*Nach-expressionismus: magischer Realismus: Probleme der neuesten europaischen Malerei*”; kwa Kiingereza ikiwa, “*After-Expressionism: Magic Realism: Problems of the newest European Painting*”.<sup>4</sup> Baadaye Roh alichapisha makala yake. Makala hii ikitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili inaashiria hali ya uajabu au umazingaombwe unaoelezea miujiza iliyomo kwenye uyakinifu wa kila siku. Franz Roh

---

<sup>4</sup> Sorensen, Lee (ed.). *Dictionary of Art Historians*. Retrieved November 27, 2000.

alitumia istilahi “uhalisiajabu” katika muktadha wa sanaa kuelezea na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uajabu uliomo kwenye uhalisi uliozoeleka. (Wafula na Njogu 2007:113).

Msukumo wa Franz Roh katika kuibuni istilahi “uhalisiajabu” ulitokana na kazi za kisanii za wasanii wa Ulaya ambao, baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, walirudi katika mtindo mpya usiozoeleka wa uhalisia katika kazi zao. Baadhi yao ni wasanii wa Kimarekani Ivan Albright, Philip Howard Evergood, Paul Cadmus, Peter Blume na George Tooker; wasanii wa Kijerumani George Grosz, Christian Schad, Otto Dix, Alexander Kanoldt, Conrad Felixmuller, Georg Schrimpf, Carl Grossberg na Franz Radziwill; msanii wa Kitaliano, Giorgio de Chirico na msanii wa Kifaransa, Henri Rousseau miongoni mwa wengine. Kutokana na hali ya wasanii hawa kuzingatia uhalisia mpya katika kazi zao, Franz Roh aliuita mtindo huu mpya “Baada-ya-Kujieleza” na wala si “uhalisiajabu”. Kisha baadaye, Roh aligundua kwamba, istilahi yake haikuwa na uzito wa kimaana unaojisimamia, ila tu iliashiria uhusiano wa kiwakati na “kujieleza”. Kwa hivyo, Roh alibadilisha istilahi hiyo na kuiita “uhalisiajabu” na wala sio “uhalisia wa kimaafumbo”. Kwa njia hii, msanii Franz Roh akawa amebuni istilahi “uhalisiajabu”. Kwake, uajabu au umazingaombwe wa ulimwengu halisi hujitokeza kwetu kifantasia. Na hapo ndipo istilahi yake ikashika kasi.

Makala ya Franz Roh yalitafsiriwa kwa lugha ya Kihispania na Fernando Vela aliyekuwa mwanafunzi wa Jose Ortega Gasset. Mnamo mwaka 1927, makala haya ya Roh yalikuwa tayari yamechapishwa katika Juzuu la Kihispania lililoitwa *Revista Occidente*, nacho kitabu chake kikachapishwa nchini Uhispania na Marekani ya Kusini. Uchapishwaji wa makala ya Roh uliwapa waandishi wengi wa Uropa motisha kubwa.

Wanafalsafa wengi wakiwemo wasanii ambao mnamo mwaka wa 1930 walikuwa wamehama Ujerumani, Czechoslovakia na Austria sasa waliguria Marekani ya Kusini. Kufuatia kuwepo kwa tamaduni au imani nzito katika visasili miongoni mwa Wahindi wa Marekani Kusini, mazingira yalikuwa mwafaka kwa kuikubali dhana ya uhalisiajabu huko Marekani ya Kusini. Ni hapa ndipo istilahi “uhalisiajabu” ilianza kuhusishwa na kazi za kifasihi.<sup>5</sup>

Mtazamo kuwa mtindo wa uhalisiajabu una asili yake Marekani ya Kusini, umetiliwa nguvu na waandishi wengine wa umazingaombwe/ uajabu kama vile Jorge Luis Borges, Isabel Allende wa Chile, washindi wa Tuzo la Fasihi la “Nobel”: Miguel Angel Asturias wa Cuba/Guatemala na Gabriel Garcia Marquez wa Colombia. Wengine ni mwandishi wa Kiswisi, Hermann Hesse; Gunter Grass (wa Ujerumani), Toni Morrison (wa Marekani) na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wote wanachukuliwa kama wana-uhalisiajabu.

Kwa muhtasari, Franz Roh anasema:

Uhalisiajabu ni uwasilishi wa ujumbe na hufichua hali ya kiroho na umazingaombwe katika chombo kwa kubainisha kudhihirika kwake na kukifanya zaidi ya kuwa halisi. Katika hali hii, uhalisiajabu hutuingiza katika ulimwengu wa kinjozi kwa kuwasilishwa kama “uhalisi”.<sup>6</sup>(TY)

---

<sup>5</sup> Guenter, I.(1995) “*Magic Realism in the Weimar Republic*” in Zamora, P.L. and Faris W.B. *Magic Realism: Theory, History, Community*. London: Duke University Press.

<sup>6</sup> Kama nambari 4 hapo juu.

Mbali na mwanzilishi wa nadharia hii, Franz Roh, kuna wataalamu wengine na wana-nadharia ambao wametafiti kuhusu nadharia hii ya uhalisiajabu. Baadhi yao ni kama wafuatao pamoja na mchango wao.

Gabriel Garcia Marquez ni mwandishi wa Colombia ambaye anahusishwa pakubwa na mtindo wa uandishi wa “kiuhalisiajabu”. Marquez alifungamanisha uhalisia na fantasia pamoja na njozi, visasili na ngano. Ingawa Marquez anafikiriwa na wasomaji wengi wa kimagharibi kuwa mwandishi wa kifantasia, yeye mwenyewe anapinga madai hayo na kusema kuwa ni mhalisia ambaye anajaribu kuelezea jinsi hali ilivyokuwa nchini mwake Colombia kwa njia ya kweli iwezekanavyo. Katika riwaya yake, *One Hundred Years of Solitude*, Marquez (1980) anaelezea kuhusu wafanyakazi wa Macondo ambao wanaandaa mgomo na baadaye uvumi unaenezwa kuwa serikali imewaua mamia ya wafanyakazi. Kisa hiki kimetajwa kama cha kifantasia kuliko vingine kwa sababu tukio la kihistoria linapuuzwa na kuwasilishwa kama uvumi tu. Kwa ujumla, Marquez ameandika matukio yasiyokuwa uhalisia wa moja kwa moja kama vile: mvua ya maua kunyesha na pia kuhusu wazee wenye mbawa.<sup>7</sup>

Salman Rushdie ni mwandishi wa uhalisiajabu pia. Alizaliwa mwaka wa 1947 nchini India na ni mwandishi wa riwaya za Kiingereza. Rushdie katika riwaya yake ya pili, *Midnight's Children* (1981), ambayo ilishinda tuzo la *Booker* mnamo mwaka 1981, anatumia mtindo wa uhalisiajabu. Riwaya hii inahusu maendeleo ya kisiasa nchini mwake, India, katika miongo iliyofuata kupatikana uhuru wa nchi hiyo kutoka kwa Uingereza. Vilevile, Rushdie ameandika *The Satanic Verses* (1988) ambayo ni riwaya yake ya nne inayoonyesha ameathiriwa kwa kiasi na maisha ya Mtume Muhammad.

---

<sup>7</sup> Marquez, G.G. (1998). *One Hundred Years of Solitude*. London: Everyman's Library.

Katika riwaya hii, Rushdie anatumia uhalisiajabu, matukio ya kawaida na watu katika kuwabuni wahusika wake. Riwayani, mmesheheni usimulizi wa kimvunjiko na visa vya uhalisiajabu vinavyosimuliwa kama njozi zinazompitia mhusika mmoja. Mifano ni wahusika Gibreel Farishta na Saladin Chamcha ambao mwanzoni, wanakwama katika ndege iliyotekwa nyara ikielekea Uingereza kutoka India na kulipukia angani lakini wote wananusurika kiajabuajabu. Kisha, katika hali ya kimiujiza, Farishta anabadilika kihusika na kuwa malaika Jibrili, naye Chamcha anakuwa ibilisi. Matukio ya uhalisiajabu yanaendelezwa katika riwaya nzima.<sup>8</sup>

Nchini Cuba, kuna mwandishi Alejo Carpentier ambaye pia amechangia pakubwa uandishi wa kiuhalisiajabu. Carpentier aliishi kati ya mwaka 1904 na 1980. Alisomea Chuo Kikuu cha Havana na aliwahi kupata tuzo za *Miguel de Cervantes, Prix, Medicis etranger*. Kama mwandishi, Carpentier ameathiri sana fasihi ya Marekani Kusini katika kilele chake kimaandishi. Mojawapo ya vitabu alivyoviandika kwa mtindo wa uhalisiajabu ni *The Kingdom of this World* (1949) ambacho kinahusu mapinduzi katika nchi ya Haiti mwishoni mwa karne ya 18. Carpentier anaegemea vipengele vya historia na jiografia ya Marekani ya Kusini na anaonyesha kuwa mpaka baina ya uajabu na uhalisi ni mwembamba mno. Vilevile, Carpentier ameandika *The Lost Steps* (1979) akitumia mtindo wa uhalisiajabu na kifantasia kuelezea historia na utamaduni wa Cuba kiubunifu.<sup>9</sup>

Cooper (1998) pia anachangia dhana ya uhalisiajabu. Katika kitabu chake, anawarejelea waandishi watatu wa kiuhalisiajabu wa Afrika Magharibi. Hawa ni Syl Cheney-Coker

---

<sup>8</sup> Rushdie, S. (1988). *The Satanic Verses*. United Kingdom: Viking Press.

<sup>9</sup> Carpentier, A (1979). *The Lost Steps*. Harmondsworth: Penguin Books.

wa Sierra Leone, Ben Okri wa Nigeria na Kojo Laing wa Ghana. Cooper anasema kwamba uandishi wao umeathiriwa na sababu za kiuchumi, kijamii (hasa imani katika visasili kupitia kwa mazingaombwe) na kisiasa.

Kwa mfano, Cooper (1998:1) akimnukuu Okri (1991) anasema:

Mara kwa ghafla, katika utovu wa kichwa changu,  
jicho lilifunguka; na nikaona mwangaza uliokuwa  
angavu zaidi, unaovutia ulimwengu.<sup>10</sup> (TY)

Kulingana na Cooper (1998:15), uhalisiajabu hunawiri kwa msingi wa mabadiliko ya kiuchumi/ kibepari, kijamii na hata kitamaduni, ambayo ndiyo huwachochea waandishi.

Katika nchi ya Peru, mwandishi Mario Vargas Llosa naye ametumia mtindo wa uhalisiajabu katika kazi zake. Llosa alizaliwa nchini Peru mnamo mwaka 1936 na alishinda Tuzo ya Fasihi ya Nobel ya mwaka 2010. Katika kitabu chake, *The Politics of Magical Realism*, Mario Llosa anasema kuwa uhalisiajabu aghalabu huenziwa na waandishi wengi wa Marekani ya Kusini, ambao wameshinda tuzo ya Nobel kwa ajili ya kazi zao.

Zamora na Faris (1995:4-5) wanasema:

Uhalisiajabu ni mtindo wa kuandika na kuvuka  
mipaka, iwe ya kilugha, kisiasa, kijiografia au  
kibayolojia. Uhalisiajabu huwezesha kuingiliana na  
kuwepo kwa mandhari tofauti na hali kinzani ambazo

---

<sup>10</sup> Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Fiction: Seeing with a Third Eye*. London: Routledge.

kwa kawaida haziwezekani katika mitindo mingine ya uandishi. (TY)

Llosa anaongeza kuwa, waandishi wa kiuhalisiajabu hukita hadithi zao katika ajenda za kisiasa na kijamii huku zikiathiri maoni ya kisiasa ya mataifa na viongozi wao.

Mario Llosa pia ameandika riwaya ya *The Green House* (1966) ambamo anazingatia uhalisiajabu kwa kutumia visasili vya kitaifa. Katika riwaya hii, Llosa analinganisha jinsi maisha ya watu yalivyokuwa nchini Peru, kwa mfano kuteswa na kunyimwa haki ya kuunda chama cha ushirika miongoni mwa wenyeji ili wapate bei nzuri kwa ngozi zao. Kwa hivyo, anayoyaeleza katika riwaya yake kwa njia ya kiuajabu ni ukweli wa matukio halisi ya nchini mwake.<sup>11</sup>

Mbatiah (2002:60) anasema:

Istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Uhalisia wa kimaajabu huhusishwa zaidi na nchi

---

<sup>11</sup> Llosa, M. V. (1966). *The Green House*. New York: Harper and Row.

zinazoendelea kutoka bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia.

Wamitila (2003:274) katika kutoa mchango wake kuhusu uhalisiajabu, anakubaliana na maelezo ya Mbatiah. Anasema:

Dhana hii huhusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu. Sifa yake kuu ni kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane kama ya kawaida tu. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika.

Kutokana na mawazo ya Mbatiah (2002) na Wamitila (2003), tunapata kuona kuwa, uhalisiajabu ni namna fulani ya kueleza uhalisi unaotuzunguka kwa njia mpya.

Mbali na wataalamu hawa, kuna waandishi na wananadharia wengine ambao wametafiti kuhusu nadharia hii ya uhalisiajabu. Baadhi yao ni Morrison, Juan Rulfo, Alexander (1990), Okri (1991), Drought (1993), Williams (1995), Danow (1995), Allende (1995), Rios (1999) na Ousbv (2002).

Pia, kuna baadhi ya waandishi wa fasihi ya Kiswahili wanaoweza kuwekwa katika kundi hili. Hawa ni E. Kezilahabi – mwandishi wa *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991); W.E. Mkufya – *Ziraili na Zirani* (1999); S.A.Mohamed – *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006); K.W. Wamitila – *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004).

#### **1.6.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu**

- i. Kueleza matukio ya kiajabu au ya kifantasia au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kuyafanya yaonekane ya kawaida. Huwepo hali ya kushangaza, kuduwaza na kuogofya.
- ii. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Huwa hakuna mipaka ya uhalisi na utohalisi katika uhalisiajabu. Pengine wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.
- iii. Mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa. Yaani, wana-uhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila ya kujiweka katika mazingira finyu kama vile ya jamii, nchi au bara fulani.
- iv. Wakati na mwanda (mahali/mandhari) hupanuliwa na kuwa na uhusiano mkubwa. Mpaka wa jadi baina ya nyakati huvunjwa kiasi kwamba matukio hayafuati kanuni ya uhalisi wa kiwakati. Mara nyingi mtazamo huu wa wakati unafungamana na suala la ndoto. Katika hali hii, mtunzi huweza kueleza kile kinachomkumba binadamu kabla ya kuzaliwa na baada ya kifo.  
Mwanda wa kisimulizi pia hupanuliwa. Huweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu wa kidhanifu au ulimwengu wa kinjozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti huvunjwa. Hali hii humwezesha msimulizi au mhusika kujitosa kwenye tathmini ya kisaikolojia.

- v. Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Huwepo mvunjiko katika usimulizi. Wasanii huweza kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili.
- vi. Mazingira huwa ni sehemu muhimu katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu/ mazimwi na misitu mikubwa yenye giza totoro hurejelewa. Pia, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu.
- vii. Uhalisiajabu unahusisha kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu. Hali mbalimbali kama uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na wenyeji/utamaduni huonekana zikiingiliana.

Tukiichunguza mihimili hii muhimu ya nadharia ya uhalisiajabu, tunapata kwamba inatosheleza uhakiki wa kazi yetu. Kwa kuizingatia, tumeweza kuielewa riwaya tunayoishughulikia ya *Watu wa Gehenna* na hatimaye kufanikisha malengo yetu. Ni muhimu pia kutaja kwamba, katika utafiti wetu, si mihimili yote iliyotumiwa. Tuliitumia ile iliyofaa zaidi kufafanua riwaya tunayoichunguza.

#### **1.6.2.2 Ufaafu wa Nadharia ya Uhalisiajabu**

Tunapoisoma riwaya ya *Watu wa Gehenna* kwa undani, pamoja na kuichunguza mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu, tunahisi kuwa, nadharia hii inafaa katika kuchunguza mada yetu ya utafiti. Teneti nyingi za nadharia hii zinafungamana na vipengele vingi katika riwaya tunayoishughulikia.

Kwanza, kuna matukio ya kiajabu na ya kifantasia ambayo ni mojawapo ya sifa za uhalisiajabu. Matukio haya yanajitokeza kupitia kwa wahusika na kuzua hali ya

kuogofya, kuduwaza na kushangaza. Pili, uhalisi na ndoto vimechanganyika, nayo hii ni sifa muhimu sana katika uandishi wa kiuhalisiajabu. Mandhari ya aina hii yameonyesha sifa ya utokaji kwenye ulimwengu halisi na kuingia kwenye ulimwengu wa kimawazo, kisha labda kurudi kwenye ulimwengu halisi. Riwayani, mhusika anapatwa na aina ya lepe na akiwa katika hali hii, anaweza kusafiri kutoka hali moja hadi nyingine. Hata wahusika wameweza kuishi maisha ya baadaye au kurudi nyuma kwenye maisha yao ya awali.

Tatu, kuna uduara wa wakati; ambapo mpaka wa jadi wa kueleza na kuonyesha nyakati umevunjwa. Matukio mengi katika *Watu wa Gehenna* hayajafuata kanuni ya uhalisi wa kiwakati na hali hii inafungamana na suala la ndoto. Wakati uliotumiwa ni wa kiduara na wala si wa kimstari. Tumegundua kwamba, wahusika wanafanya matendo yao kwa kipindi kirefu sana na hata wanabakia katika hali hizo.

Nne, mwanda umepanuliwa katika riwaya hii kwa kuwa matukio hayajajikita katika muktadha finyu wa jamii, nchi au bara moja, tofauti na ilivyo katika mitindo iliyozoeleka ya uandishi. Hali hii imewezeshwa kupitia kwa jinsi ambavyo wahusika wa kiuhalisiajabu walivyoubwa na mtunzi.

Tano, kuna matukio mengi yasiyofuatana kimantiki jinsi ilivyozoeleka kwa sababu ya mvunjiko katika usimulizi. Hadithi ya *Watu wa Gehenna* ina visa vingi ambavyo vinatokea katika kisa kikuu. Mtunzi amefanya hivi kupitia mbinu ya urejeshi, kumbukizi na pia kujenga wahusika wenye nafsi mbili.

Kwa ufupi, hii ni mifano tu ya mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu na hali halisi ya riwaya teule, jambo linalotufanya tuamini nadharia hii ni mwafaka kwa mada ya utafiti wetu.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Katika fasihi ya Kiswahili, kuna waandishi/ watafiti watangulizi katika uwanja huu wa uchanganuzi wa kimtindo. Ufuatao ni muhtasari wa mada mbalimbali kuhusu tafiti za kimtindo na uhakiki wa kazi za kiuhalisiajabu.

Kitsao (1975), amehakiki mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili akitumia nadharia ya Crystal na Davy (1969) iliyohusu Kiingereza kinachozungumzwa. Kitsao amefafanua kwa undani dhana ya mtindo na elimimitindo huku akionyesha namna mtindo unavyojitokeza katika kazi za kifasihi. Kisha, akachunguza jinsi mtindo unavyojitokeza katika kazi teule alizozishughulikia: mashairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. Utafiti wetu unahusu uchanganuzi wa vipengele vya mtindo katika riwaya moja tu. Kwa hivyo, matokeo ya utafiti wa Kitsao ni muhimu kwa utafiti wa mada yetu kwa kuwa yanatupatia mwelekeo wa kuvihakiki vipengele vya mtindo katika riwaya tunayoishughulikia.

Nyabunga (2005) ametafiti kuhusu “Uhakiki wa *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) za K.W. Wamitila” katika misingi ya Nadharia ya Uhalisiajabu. Katika utafiti wake, Nyabunga anachunguza kwa undani suala la uhalisiajabu katika riwaya hizi kwa kuangazia mihimili kadhaa ya nadharia ya uhalisiajabu. Nyabunga ameshughulikia riwaya mbili za kimajaribio na sisi, utafiti wetu unaangazia riwaya moja tu. Utafiti wetu umejiegemeza katika vipengele vinne vya mtindo hususan wahusika, tamathali za usemi, usimulizi na mandhari na tumevishughulikia kwa undani katika misingi ya Nadharia za

Umitindo na Uhalisiajabu. Matokeo ya utafiti wa Nyabunga yanatufaa sana hasa katika kuirejelea mihimili inayohusika kwa kuzingatia uhusika usiozoeleka pamoja na mandhari ya kiginingi au kisihiri katika kusawiri kazi ya kinathari.

Mtafiti Olali (2010) amehakiki riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) kwa anwani “Muundo (“Structure”) na Dhidi-Muundo (“Anti-Structure”) katika riwaya mpya ya *Babu Alipofufuka*” katika *The Nairobi Journal of Literature* (Na. 6, 2010). Katika utafiti huu, Olali anabainisha udhidi-muundo katika matumizi ya mbinu za uhalisiajabu kwa mfano jinsi unavyodhihirika nyumbani mwa K, katika Limonsin na anapokuwa Neo-Casino. Anadhihirisha kuwa, muundo na mtindo katika riwaya za kimajaribio hutofautiana kwa kiwango kikubwa na kazi za kiuhalisia. Utafiti wetu unalenga kuchanganua vipengele mahususi vya mtindo: wahusika, tamathali za usemi, usimulizi na mandhari katika riwaya mpya. Hivyo basi matokeo ya utafiti wa Olali kuhusu uchanganuzi wa tamathali za usemi na mbinu za lugha yametufaa sana katika uchanganuzi wa kipengele cha mtindo katika riwaya tunayoishughulikia.

Bakari (2011) anatafiti dhana ya “Usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu!* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda* (2002)”. Katika utafiti huu anabainisha vipengele mbalimbali vya kiuhalisiajabu; na kuonyesha jinsi watunzi wa riwaya hizi wanavyotumia mtindo wa uhalisiajabu ili kueleza matatizo yanayoibuka katika ulimwengu wa sasa. Mtafiti huyu anaangazia maudhui katika riwaya mbili na hadithi fupi lakini utafiti wetu unaangazia vipengele vya mtindo katika riwaya moja tu na kuonyesha ukamilifu wake unavyobainika. Matokeo ya utafiti wa Bakari yametufaa sana hasa katika kuainisha vipengele vya kimtindo na kiuhalisiajabu.

Lugwiri (2011), ni mtafiti ambaye anashughulikia “Sitiari, Taashira na Tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka: uhakiki wa kimtindo*”. Katika utafiti huu, Lugwiri anatumia Nadharia ya Umitindo na anabainisha wazi jinsi vipengele vya tamathali za usemi vinavyobainika katika utenzi-husika. Anaonyesha kuwa tamathali za usemi ni mihimili mikuu ya maudhui na dhamira. Kwa kuwa utafiti wetu unahusu mtindo katika riwaya, matokeo ya utafiti wa Lugwiri yametufaa pakubwa katika kuchanganua vipengele vya kimtindo tulivyovishughulikia.

Mtafiti mwingine wa kazi za kimajaribio na kiuhalisiajabu ni Mugwika (2012) ambaye anatafiti “Dhana ya Uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba*”. Mugwika anachunguza uchimuzi katika kiwango cha wahusika na cha matumizi ya lugha kwa mtazamo wa nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Kwa kuwa riwaya ya *Mafamba* ina mshabaha na *Watu wa Gehenna* hasa kwa kukiuka kaida za uandishi zilizozoeleka, matokeo ya utafiti wake yametufaa sana katika kuchanganua fani katika riwaya yetu teule. Tofauti tu ni kwamba tumetumia Nadharia za Umitindo na Uhalisiajabu katika utafiti wetu.

## **1.8 NJIA ZA UTAFITI**

Utafiti wetu utakuwa wa maktabani.

Tumeisoma riwaya ya *Watu wa Gehenna* kwa undani na kuchanganua vipengele vya fani tulivyovitaja awali na pia riwaya nyingine za kimajaribio zilizoandikwa na waandishi mbalimbali ili kutathmini sifa za kifani. Vilevile, tumerejelea vitabu, makala na maandishi yanayohusu Nadharia ya Umitindo na Nadharia ya Uhalisiajabu tulizozitumia katika utafiti wetu.

Tumerejelea makala na tasnifu mbalimbali zilizoandikwa kuhusu umitindo katika kazi za kifasihi na pia tukakita utafiti wetu katika tovuti kwenye mitandao tofauti ili kupata yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Umitindo na ya Uhalisiajabu. Tumeshirikisha pia maoni ya wataalamu katika taaluma hii kuhusiana na mada na nadharia za utafiti wetu, pamoja na kuufumbata ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu, wahadhiri mbalimbali wakiwemo wanafasihi na wanaisimu.

## **1.9 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumeorodhesha na kueleza somo la utafiti wetu ambalo ni ‘Mtindo katika *Watu wa Gehenna*’. Tumbainisha tatizo la utafiti wetu, madhumuni pamoja na maswali ya utafiti ambayo yanatuongoza katika kutafiti mada yetu. Vilevile, tumeeleza sababu za kuchagua mada tunayoishughulikia ambazo hasa ni za kiakademia/ kiusomi na tukabainisha upeo na mipaka ya utafiti wetu. Mbali na hayo, tumetaja misingi ya nadharia ambazo tumetumia katika kuishughulikia mada yetu. Tumezifafanua nadharia mbili ambazo tumetumia, nazo ni nadharia ya Umitindo na nadharia ya Uhalisiajabu. Tumezichanganua nadharia hizi kwa undani kwa kueleza mwasisi wa kila mojawapo, mihimili yake pamoja na ufaafu kwa kuitafiti mada yetu.

Hatimaye, tumeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada inayohusika na kueleza umuhimu wake kwa somo ambalo tunalishughulikia. Tumekamilisha sura hii kwa kubainisha mbinu ambazo tumezitumia katika utafiti wa mada yetu.

## **SURA YA PILI: UHUSIKA NA WAHUSIKA KATIKA WATU WA GEHENNA**

### **2.0 UTANGULIZI**

Katika sura hii, tumeshughulikia kipengele cha uhusika na wahusika. Kwanza, tumechunguza mbinu zinazotumiwa na watunzi katika kuwasawiri wahusika katika kazi za kifasihi kwa jumla na baadaye, tukachanganua makundi ya wahusika wanaopatikana katika *Watu wa Gehenna*.

### **2.1 Uhusika na wahusika**

Uhusika ni dhana au istilahi ambayo hutumiwa kuelezea mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Baadhi ya waandishi ambao hutilia mkazo suala la uhusika huwa wanaamini kuwa kilicho na uzito na maana katika fasihi ni jinsi matukio yanayopatikana katika kazi yanavyowaathiri wahusika. Athari hiyo huwa na matokeo mengi kuhusu mikabala yao sambamba na matukio yaliyotokea (Wamitila 2003:278).

Njogu na Chimerah (1999:250) katika kuchangia dhana ya uhusika wanasema:

Uhusika ni umithilishaji wa vitendo vya viumbe wa hadithini na vile vya viumbe katika ulimwengu razini. Vitendo vya viumbe hao husababishwa na kuingiliana kwao na mazingira ya ubunifu, kama ambavyo vitendo vya viumbe razini huwa vimesababishwa na

maingiliano baina yao wao wenyewe na mazingira  
yao, ambayo ni razini.

Uhusika wa jadi umejengwa kwenye usawirishaji wa wahusika kwa msingi wa uhalisi wa kijamii. Wahusika wa jadi au wa kimapokeo wanakaribiana na binadamu wanaopatikana katika ulimwengu halisi.

Wamitila (2003:123) anafafanua dhana ya wahusika kama ifuatavyo:

Mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida.

Kulingana na Wamitila (2008:369), wahusika ni nyenzo kuu ya fasihi kwa sababu wao ndio jira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika.

Mtazamo wa dhana ya wahusika hutofautiana kutegemea mkabala anaouchukua mhakiki na nadharia ya fasihi inayohusika. Kwa hivyo, "Mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu."

Huwepo mhusika wa kihalisia ambaye msingi mkuu wa kumsawiri ni kanuni ya maisha halisi; yaani hutegemea kanuni ya ushabihikweli. Tunapowaeleza wahusika kama 'binadamu wa hadithini' huwa tunaegemea kanuni hii. Mhusika wa kihalisia ana sifa nyingi zinazohusishwa na binadamu katika maisha ya kila siku.

Kisha tuna mhusika wa kinjozi ambaye anahusishwa kwa kiasi na njozi au fantasia. Mhusika wa aina hii hupatikana katika ulimwengu wa ajabu au wenye sifa za ulimbwende anapoingiliana na viumbe wasiokuwa wa kawaida. Sifa anazopewa mhusika huyu, ziwe nzuri au mbaya hukuzwa kuliko kawaida. Njozi hutumiwa kueleza fasihi ambayo huonyesha uwazaji wa kiwango cha juu cha matukio yasiyokuwa ya kawaida. Dhana ya njozi ni pana mno na huweza kujumlisha bunilizi za kisayansi na kazi za kihalisiajabu (ambazo zinahusishwa na matukio yasiyokuwa ya kawaida na bila kutoa sababu za kutokea kwake).

## **2.2 Usawiri wa Wahusika**

Wamitila (2003:312) anasema yafuatayo kuhusu dhana ya kusawiri wahusika:

Hii ni dhana inayotumiwa kuelezea jinsi wahusika wa kifasihi walivyochorwa au kuwasilishwa na msanii au mtunzi wa kazi fulani. Usawiri wa wahusika huhusisha majina yao, lugha wanazopewa na matumizi yao ya kifasihi.

Usawiri wa wahusika wa kifasihi unaweza kufungamanishwa kwa kiasi kikubwa na wakati ambao unaweza kuangaliwa kwa namna tofauti. Wale wahusika wanaopatikana

katika kazi za mwanzoni wanafungamana na wahusika wanaopatikana katika fasihi simulizi, na wanaonyesha jinsi wakati unavyoweza kuathiri mtazamo wa wahusika wa fasihi (Wamitila 2008:162). Riwaya za kisasa zinatangua baadhi ya misingi ya usawiri, nyingine hata kubadilisha dhana nzima ya mhusika. K.m majina hudenguliwa tukapata wahusika kama K katika *Babu Alipofufuka*; Eks katika *Watu wa Gehenna*; Ndi na Bi. M katika *Dunia Yao* (2006).

Katika msingi huu, tumechunguza uhusika ulivyotumika kukuza fani katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Ujumbe na mtindo hudhihirika katika lugha waitumiayo wahusika, dhima na majukumu wanayopewa pamoja na muundo wake.

### **2.3 MBINU ZA KUWASAWIRI WAHUSIKA**

Kuna mbinu kadha ambazo watunzi huweza kutumia katika kuwasawiri wahusika. Wahusika huweza kuwasilishwa kwa njia dhahiri au isiyokuwa dhahiri, kudhihirishwa na kuendelezwa kwa njia tofauti, kuanzia za kijuujuu hadi za undani au za kina hadi kwa undani wa kisaikolojia. Zifuatazo ni baadhi ya mbinu ambazo hutumiwa kuwasawiri wahusika katika kazi za kiriwaya.

#### **2.3.1 Maelezo ya msimulizi au mwandishi.**

Katika mbinu hii, msimulizi anaweza kueleza wasifu wa mhusika, msukumo wa matendo yake, mazingira yake na amali zake ili msomaji auone mtazamo huo na labda hata akubaliane naye. Njia hii hujulikana kama 'uhusika wa kimuhtasari' kutokana na ile hali kuwa mwandishi anatoa muhtasari wa mhusika fulani kwa maneno au sentensi kadha (Hawthorn 2001:93-94 na Wamitila 2008:171, 376). Ingawa mtindo huu hutumiwa na

watunzi wengi wa kazi za kifasihi (kwa kuwa humrahisishia msomaji kazi), una udhaifu wa kuchimuza mkabala wa mhusika au hata mtazamo alionao mtunzi anayehusika.

Katika *Watu wa Gehenna*, kuna wahusika wengi ambao wamesawiriwa kupitia kwa maelezo ya msimulizi. Hawa ni Eks Ngwenyama na mkewe, Takosani binti Abdalla; Takosani binti Inatesh, Akilimali van Krockoff, Baadayadhiki, Bi. Saeeda Khan, Mishi binti Bwan Rehema na wengineo.

### **2.3.2 Maelezo au maneno ya wahusika wengine.**

Njia hii huhusu maelezo ambayo yanatolewa na mhusika mmoja kumhusu mhusika mwingine au wengine. Mara nyingi, mtindo huu hutuelekeza kimsingi kwenye mkabala wa mhusika anayehusika. Hata hivyo, maelezo ya mhusika mmoja kumhusu mwingine huenda yasitegemewe hasa kutokana na uwezekano wa maelezo hayo kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo wa mhusika binafsi. (Wamitila 2008: 172). Mfano katika riwaya tunayoishughulikia ni Takosani binti Inatesh ambaye anatambuliwa na Sikujua kama 'jini' kutokana na kauli yake ya kutaka kumpa utajiri (Olali 2012:48-49).

### **2.3.3 Mbinu ya matendo au matumizi ya mazungumzo.**

Pia huitwa 'mbinu ya kidrama'. Katika mbinu hii, maneno yanayosemwa na wahusika baina yao huwa ni msingi mkubwa wa kuwakuza na kuwaendeleza hao hao wahusika. Mtunzi huwakuza kwa kuwaonyesha wahusika wakitenda matendo na kuzungumza huku akiwaacha wasomaji wawaone na kuzichanganua tabia zao kutokana na matendo au mazungumzo yao. Mazungumzo huchukuliwa kama njia ya kuendeleza mgogoro (tendo) lililoko katika kazi ya kifasihi au dhamira au maudhui. Hutekeleza kazi ya

kumsawiri mhusika. Matendo ya wahusika yanaweza kutuelekeza katika kuelewa tabia, imani, mategemeo au matumaini, hisia zao, kero zao, ndoto zao au hata udhaifu wao. (Njogu na Chimerah (1999:46); Hawthorn (2001:95) na Wamitila (2008:376).

Katika *Watu wa Gehenna*, mbinu hii imetumiwa sana katika kuwasawiri wahusika hasa kwa kuwa hadithi nzima imejikita katika mazungumzo ya kidrama au dayalojia. Mifano ni Eks, MKUU, Mzee Afisul, Takosani binti Inatesh, Mishi binti Bwan Rehema, Baadayadhiki, Faki Nahodha, Hikmat na wengineo.

#### **2.3.4 Mbinu ya majazi au matumizi ya majina**

Katika riwaya ya Kiswahili, majina huwa ni msingi muhimu wa uhusika. Katika mbinu hii, mtunzi hutumia majina ambayo yanafumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Kwa njia hii, msomaji huweza kuifahamu tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi zaidi. Vilevile, mtunzi huweza kuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahusu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima. Hata hivyo, kuna udhaifu kwa kuwa msomaji hashirikishwi katika uamuzi wa wasifu wa mhusika; hulazimika tu kuridhika na maoni ya mwandishi. Mara nyingi, njia hii ya kuwasawiri wahusika huhusisha matumizi ya kinaya au kejeli, na mihusianisho na ishara. Kwa mfano, Rais Kapera katika tamthilia ya *Kaptula la Marx* ya E. Kezilahabi (2010). Jina kapera laweza kuchukuliwa kama ishara ya kutokuwa na matunda yoyote kwa siasa na falsafa ya kiongozi huyu (Wamitila 2008:170, 378).

Mifano ya wahusika waliopewa majina ya majazi ni wengi katika *Watu wa Gehenna*. Kuna Daktari na wanafunzi wa utabibu, Mzee Afisul, Takosani binti Inatesh, MKUU,

Siyawezi, Baadayadhiki, Faki Nahodha, Inspekta Maliyamungu, Munkariatakuua Leo, Kinaya, Pasua, Ujana, Yunasi, na Kasisi Taabu.

### **2.3.5 Mbinu ya ulinganuzi na mgotanisho**

Hii ni mbinu ambayo mwandishi anaweza kuitumia katika kuwakuza na kuwaendeleza wahusika kwa kuwalinganua au kuwaweka sambamba, yaani katika muktadha sawa. Mtunzi hufanya hivyo ili kuonyesha tofauti kati ya wahusika wawili kwa uwazi zaidi. Kwa kawaida, wahusika wanaolinganuliwa hueleweka zaidi kuliko wale wasio katika mazingira hayo.

Mifano katika *Watu wa Gehenna* ni Siyawezi akilinganuliwa na wanafunzi wenzake wa Chuo Kikuu cha Kuhisika ambao ni Saida, Kinaya, Pasua na Ujana. Siyawezi ni mwadilifu na mtiifu lakini wenzake ni watovu wa maadili.

### **2.3.6 Mbinu ya mwingilianomatini**

Matini za kifasihi huhusiana na kuingiliana kwa njia tofauti. Kuingiliana huko kunaweza kutokeza katika viwango tofauti vikiwemo kiwango cha hadithi inayohusika, dhamira, ishara au sitiari; na katika kiwango cha usawiri na uendelezaji wa wahusika. Kazi za kifasihi ambazo zimekitwa katika matumizi ya simulizi-kuu za jamii fulani au za utamaduni wa kimagharibi (kwa mfano Ukristo), zinaonyesha waziwazi sifa hii katika usawiri wa wahusika (Wamitila 2008:380-381, 389-390). Mifano ya wahusika katika *Watu wa Gehenna*, wanaosawiriwa kwa njia hii ni MKUU, Mzee Afisul na Munkari. Hawa ni wahusika wa kimwingilianomatini kwa kuwa tathmini yetu kuwahusu inaathiriwa na simulizi zao katika Biblia Takatifu au Korani.

## 2.4 MAKUNDI YA WAHUSIKA KATIKA *WATU WA GEHENNA*

Katika riwaya tunayoishughulikia, kuna makundi mawili makuu ya wahusika: wahusika halisi na wahusika wa kimazingaombwe. Wahusika ambao wamesawiriwa kama wa kiuhalisia ni Eks Ngwenyama na Takosani binti Abdalla ambao ni mume na mke; Sikujua na Mwalimu Baya, makasisi Yunasi na Taabu, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kuhisika: Hikmat, Kinaya, Pasua na Saida; Bi. Saeeda Khan, Faki Nahodha na Vuai Nahodha; Lakeisha, Baingana na Siyawezi; na Inspekta Maliyamungu na Krockoff van Akilimali.

Kundi la wahusika wa kimazingaombwe ndilo linalotawala riwaya nzima kwa sababu hata wahusika wa kihalisia tuliowataja wanasawiriwa katika mandhari ya kinjozi na mwandishi. Kuna wahusika majini kama Mishi binti Bwan Rehema, Takosani binti Inatesh, Shamsa (Baadayadhiki), Daktari wa Majini Tisa na mtoto Saida. Kuna wahusika wa kiungu ambao ni MKUU, Munkari, Mzee Afisul, *Shemhamforash* na Nyamaume. Kuna wahusika nafsi kama nafsi ya Eks (ikizungumza na Eks), nafsi ya Baingana (ikiwa ndani ya nafsi ya Hikmat na kuhojiana naye); na nafsi ya Hikmat.

Tofauti kubwa kati ya wahusika wa kimapokeo (jadi) na wahusika katika *Watu wa Gehenna* inatokana na jinsi mtunzi Olali anavyosawiri wahusika katika kazi yake. Olali anatumia mbinu ya mhusika jumui ambaye anajumlisha wahusika wengi katika mhusika mmoja (Wamitila 2008:388-389). Katika riwaya hii, kuna wahusika wawili tu, Eks na Takosani binti Abdalla. Hawa ndio wahusika pekee katika riwaya nzima lakini wamepewa nafasi za wahusika wengine katika hadithi. Wamesawiriwa kwa njia ya kupewa sifa zinazowakilisha wahusika wengine tofauti.

Mbali na haya makundi mawili, wahusika katika *Watu wa Gehenna* wanaweza kugawanywa katika matapo mengine kiuamilifu. Makundi haya ni: wahusika wakuu, wasaidizi/wadogo, wajenzi na jumui. Katika kufafanua makundi haya, tumefafanua pia aina mbalimbali za wahusika zikiwemo duara/mviringo, bapa, shinda, wahusika wa kinjozi, wa kimwingilianomatini na wa kimapinduzi.

#### **2.4.1 Wahusika wakuu.**

Hawa ni wahusika ambao hutawala kazi ya kifasihi, wanahusika katika utendaji wa matukio muhimu na wanawakilisha dhamira na maudhui ya kazi husika. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999:41), wahusika hawa huwa na dhima ya kuisukuma riwaya mbele kwa sababu migogoro na matendo yote muhimu yanawahusu. Dhamira kuu ya mwandishi hujitokeza kupitia wao, na msimamo wa mwandishi kuhusu dhamira, matukio ya vitushi vya hadithi hujibainisha kupitia kwa matendo na maneno yao. Mwingiliano wao na wahusika wengine ndiyo mbinu ya kufafanua dhamira kuu. Mhusika mkuu anaweza kuwa mtu binafsi, anayejidhihirisha moja kwa moja, au kitengo cha jamii (Njogu na Chimerah (1999:41) na Hawthorn (2001:90).

Wamitila (2003:125) anasema:

Mhusika mkuu ni mhusika ambaye anaitawala kazi ya kifasihi tangu mwanzo hadi mwisho. Mhusika huyu anaweza kutokeza mara kwa mara katika kazi hiyo au asijitokeze. Wahusika wakuu hubeba kiini cha dhamira

na maudhui ya kazi inayohusika pamoja na maana ya hadithi hiyo.

Kutokana na mawazo haya, mhusika mkuu ameumbwa makusudi kutekeleza majukumu fulani anayodhamiria mwandishi. Matendo yake, furaha yake, machukizo yake na kuwepo kwake kunadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya mwandishi.

Katika kundi hili kuna wahusika wafuatao katika *Watu wa Gehenna*: Eks Ngwenyama, Hikmat na Bi. Saeeda Khan.

**(a) Eks Ngwenyama.**

Huyu ndiye mhusika mkuu katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*.

Mtunzi anamsawiri mhusika huyu kwa mtindo changamano na kwa ubunifu mkubwa; kinyume na ilivyozeleza katika uhusika wa jadi. Eks ni mhusika jumui, kwa maana ya kuwa, anajumlisha wahusika wengi (katika mhusika huyo huyo mmoja). Katika hadithi nzima, Eks anapewa sifa zinazomfanya awakilishe wahusika tofauti kwa wakati mmoja; na anatumiwa kuonyesha fujo za maisha. Katika mandhari ya kinjozi, anawakilishwa na wahusika Sikujua, Mwalimu Baya, Hikmat, mchungaji Yunasi, Faki Nahodha, Krockoff na wengine. Mtunzi anamsawiri kwa njia ambayo kwayo anawakilisha wahusika tofauti; na pia, ni aina ya sitiari ya dhana nzima ya maisha katika ulimwengu wa sasa (Wamitila 2008:389).

Eks anasawiriwa kupitia maelezo ya msimulizi. Alimwoa Takosani binti Abdallah na hawakubarikiwa mtoto; sababu ikiwa ni ya kiafya. Eks alikuwa na kasoro katika shahawa

zake; hakuwa na shahawa za kutosha na pia kasi ya shahawa hizo ilikuwa ya kulaza damu (uk. 18). Hatimaye mkewe anaaga dunia. Baada ya kifo cha mkewe, Eks anabaki pweke jambo linalomfanya amuo Lakeisha ili aishi naye na apate usaidizi. Tayari Lakeisha alikuwa na watoto wawili, Baingana na Siyawezi.

Eks ni mtu mwenye mapenzi kwa kuwa anawapenda watoto wake wa kambo pamoja na mama yao, na wanaishi kwa furaha kubwa katika ndoa kwa miaka kumi na mitatu. Eks anawakidhia mahitaji yote yakiwemo kumnunulia mkewe tarakilishi anapomwomba (uk. 190-191). Lakini, Lakeisha anapapia 'maendeleo' ya kitarakilishi na kumpata mume tajiri katika mtandao wa *facebook* na kuomba talaka kwa Eks. Eks anampa talaka na wanaachana huku Eks akibaki na watoto wa Lakeisha. Miezi sita baada ya Lakeisha kuondoka, Eks anamwoa mke mwingine ambaye anakataa kuishi na watoto wake (Baingana na Siyawezi). Eks anahama akawa anawatembelea mwanzoni lakini mwishowe anakata mguu (uk. 193). Kutokana na maelezo haya, Eks ni mhusika duara. Anabadilika kitabia kutokana na wakati na mazingira yake. Kwa mfano, mkewe alipoaga, aliathirika pakubwa na baadaye akaoa mke mwingine. Kule kuondokewa na mke wa pili pia kunambadilisha tena akaoa mara nyingine tena. Hali hii ya kubadilika inaendelea hadi mwisho.

Kupitia maelezo ya msimulizi, Eks aliwahi kufanya kazi katika kampuni moja ya kutengeneza saruji iliyoitwa *The World Cementers Inc.* kwa miaka arobaini. Kutokana na mazingira ya kikazi, Eks anaathirika kiafya akawa anasahausahau mambo kama matukio na tarehe maalumu haraka, akaugua ugonjwa wa mapafu, wa moyo na kuwa na

matatizo ya figo. Eks anakuwa na maumivu mengi akawa hatembezi vizuri kwa miguu yake. Kwa upande mwingine, malipo ya uzeeni anayopewa yanamezwa na gharama za juu za matibabu (uk. 14-15). Ujumbe unaoendelezwa hapa ni jinsi waajiri wengi huwatumia wafanyikazi kwa lengo la kupata faida kubwa bila ya kujali maslahi ya wafanyakazi hao ki-ujira na kiafya.

Mtunzi vilevile anamsawiri Eks kupitia mbinu ya mazungumzo na nafsi yake na Mzee Afisul. Katika mandhari ya kinjozi, Eks anasikia sauti ya Mzee Afisul ambaye anamhoji kuhusu 'Binadamu ni nani?' na suala la 'superior intelligence' na anatumia kielelezo cha sataranji kumfafanulia (uk. 22-23). Katika mahojiano haya, Eks anasawiriwa kama mhusika asiyejifahamu; hajui binadamu ni nani, na ikiwa ana akili aila ama hana. Kwake, binadamu ni familia ya *Hominidae* na wa spishi ya *Homo Sapiens* (uk. 10-12).

Katika mandhari ya kinjozi, tunampata Eks akiwa mhusika mtiifu. Nafsi yake inamwamuru afe na kweli anakufa na kisha anafufuka baada ya miaka saba (uk. 30). Tunaambiwa katika miaka hiyo saba, Eks anafanya mahojiano na MKUU ambaye anamwonya dhidi ya kupotoshwa na Mzee Afisul kuhusu binadamu ni nani. MKUU anampa mawaidha kuhusu umuhimu wa mboga na matunda kwa mwili wa binadamu.

Hatimaye Eks anapokea amri saba za MKUU. Anaambiwa abadilishe jina lake la Eks, umri wake upunguzwe kutoka miaka 70 hadi 23, atafute mchumba mwingine aoe baada ya kifo cha Takosani na afunge safari, aondoke Mvita hadi Al Jazeera Al Khadra kutafuta mchumba huyo. Pia, akiwa huko Al Jazeera, achangie mradi mmoja wa kuhifadhi maji; asirudi tena Mvita na mwisho, asiwahi kuukaribia mlango wa Gehenna (uk. 36).

Eks ni mhusika ambaye hadithi nzima ya *Watu wa Gehenna* inafanyika katika mawazo yake. Baada ya matukio yote njozini mwake, mkewe, Takosani binti Abdalla anamwamsha mumewe, akiwa amelowa jasho. Tunaambiwa hivi:

Alikuwa amelowa jasho na kuonekana kama alikuwa kwenye jinamizi. Hakujua alikuwa amelala kwa muda gani. Alipoyafumbua macho yake yaliyokuwa mekundu kama damu kutokana na usingizi ule mrefu, Eks kwa mara nyingine alijiona na kuiona dunia halisi.  
(uk. 267)

Ili kuthibitisha kuwa Eks alikuwa mhusika jumui, msimulizi anasema haya kumhusu:

Alikumbuka jinsi alivyobadili na kuchukua maumbile ya wahusika wengi tofauti tofauti. Alikumbuka vema kuwa huko, alikuwa mara anazinduka, mara analala, mara anaamka, mara anafufuka, mara yumo Gehenna, mara anateketea, mara yu baharini. (uk. 267)

**(b) Bi. Saeeda Khan**

Ni Mpakistani ambaye anamiliki hospitali ya KK Khan jijini Nairobi. Alihamia Uingereza baada ya kuhama Nairobi. Mhusika huyu anasawiriwa kupitia maelezo ya msimulizi. Aliwahi kufanyiwa upasuaji wa sikio lake la kulia pale Bayswater alipokuwa na tezi moja iliyokuwa ndani kabisa na ilistahili kung'olewa. Wakati huu Saeeda anatumiwa na

Daktari kuwafundisha wanafunzi wa utabibu. Mbele yake, daktari anawaeleza wanafunzi kuhusu tatizo la mgonjwa, operesheni itakayofanywa, muda itakaochukua pamoja na hatari zilizopo katika upasuaji huo.

Kupitia maelezo katika barua ambayo Munkariatakuua Leo anamwandikia Inspekta Maliyamungu, Bi. Saeeda Khan alishiriki katika biashara ya kuwasafirisha watu hadi Uingereza kwa minajili ya kuwapunja. Kwa mfano, anampeleka Bi. Mwanahamisi Mruke Uingereza amfanyie kazi na anamwahidi malipo ya shilingi laki moja za Kenya na pauni kumi za Uingereza kila mwezi. Hata hivyo, Bi. Mruke anapofika huko, Bi. Saeeda anaanza kumdhulumu. Kwanza, anatawaa pasipoti yake na visa akaziweka ili Bi. Mruke asitoroke. Pili, Bi. Mruke anafanya kazi zote za nyumba siku saba kwa juma, na kuwahudumia watoto walemavu wa Bi. Saeeda. Bi. Mruke anabaguliwa upande wa chakula na aghalabu hakupewa chakula. Pia, hakupewa chumba chake binafsi na badala yake anapewa kigodoro chembamba na shuka alale jikoni sakafuni. Baada ya mateso haya yote, Bi. Saeeda hamlipi mshahara aliomwahidi na mtoto wake aliyebaki Kenya anakosa karo ya shule. Dhuluma zaidi ni kuwa, wazazi wa Bi. Mruke wanapougua na hatimaye wanakufa, Bi. Mruke hapewi ruhusa kuhudhuria mazishi yao (uk. 86-87). Mhusika Bi. Saeeda anatumia kuendeleza ujumbe wa dhuluma kwa wafanyikazi wa nyumbani, huku waajiri matajiri kama yeye wakijidai wanawasaidia.

Bi. Saeeda Khan pia anashiriki biashara ya kuwaua wagonjwa wakiwemo maalbino na kuuza sehemu zao za mwili na nyeti kwa gharama ya juu. Mfano mzuri ni kisa cha Baingana na Lakeisha. Lakeisha alikuwa rafiki na jirani ya Bi. Saeeda anapokuwa Kenya.

Wakati Lakeisha anajifungua mtoto zeruzeru (Baingana), Bi. Saeeda anampenda kinafiki; anamletea peremende akijua atafaidika kutokana na mwili wake wa ki-albino (uk. 182). Katika mandhari ya kinjozi, Bi. Saeeda Khan na wanaume watatu wanamwua kwa parange mtoto Baingana na kukata sehemu zake za mwili. Mahakama ya Gehenna inampata na hatia ya kumuua Baingana na kuuza sehemu za mwili wake kwa wapiga ramli na kumhukumu kifo. Katika kujitetea, Bi. Saeeda ‘anakiri’ kosa hili bila kujua.

Anauliza jaji:

Je, hawa ni binadamu? ..... Mbona si kweli kwani tulipata baraka kutokana na viwiliwili vya zeruzeru na hata hospitali yangu iltokana na viwiliwili vya zeruzeru? (uk. 187)

Bi. Saeeda ni mnafiki. Anapohukumiwa na jaji, anasema kuwa yeye ni mtu mwema.

Msimulizi anatumia haya:

Bi. Saeeda Khan aliuliza ni kosa gani alilolifanya kuingia Gehenna kwani alijitahidi kuwa raia mwema – mwanamke mwema na tena mwanafamilia mzuri na mchapakazi. Alisema jinsi alivyojitahidi kufanya yote sawa na mapenzi ya Mungu (uk. 187).

Anapoulizwa sababu ya kutaka kumuua Baingana kwa parange anasema:

Nilimpenda Baingana na kumthamini. (uk. 187)

Vilevile, kupitia maelezo ya msimulizi, Bi. Saeeda anashirikiana na Kasisi Taabu katika biashara za nyeti za maalbino. Hata katika gazeti kuna habari kwa kichwa, *Body part thieves hit mortuary* na washukiwa katika sakata hiyo ni Bi. Saeeda Khan na Taabu. Waliuza sehemu za mwili na nyeti za binadamu hasa za mazeruzeru (uk. 198-200).

Maudhui yanayoendelezwa ni kuwa, Bi. Saeeda anashiriki biashara haramu ya nyeti za binadamu. Anapewa adhabu ya kutumbukizwa katika rusu ya tatu ya *chhaldabius* katika moto mkali Gehenna. Pia, ni bayana kwamba biashara ya nyeti za binadamu inaendelezwa na watu mbalimbali wakiwemo madaktari, wahudumu wa mochari, makasisi kama Taabu na matajiri kama Bi. Saeeda Khan. Hata hivyo, adhabu ilikuwa inawasubiri Gehenna.

Bi. Saeeda Khan anaadhibiwa kwa kutupwa Gehenna. Anajaribu kutoroka kwa sababu ya uchungu na maumivu na analia hata machozi ya damu, lakini wapi. Moto mkubwa unamwakia na kumchoma na wenzake. Ndiye aliyekuwa kiongozi wa watu wa Gehenna kwa sababu alikuwa ametenda dhambi nyingi alipokuwa duniani (uk. 222).

Kwa ujumla, Bi. Saeeda Khan ni mhusika bapa-sugu. Anashiriki uovu wa biashara haramu ya nyeti za zeruzeru kuanzia mwanzo hadi mwisho. Pia, anawadhulumu wafanyakazi wa nyumbani. Hakubadilika hadi anaadhibiwa Gehenna kwenye moto mkali.

### **(c) Hikmat**

Mwanzoni, Hikmat anasawiriwa kama mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kuhisika. Kupitia maelezo ya msimulizi, Hikmat alikuwa kiongozi wa wanafunzi chuoni. Anawaongoza

wenzake katika mapambano makali na polisi na ndiye anayebeba bango la *The Corrupt Politician's Creed*. Polisi wanamfyatulia risasi ila haikumpata kwa sababu anafyatuka haraka. Maandamano yanapoendelea, polisi wanamjeruhi vibaya Hikmat na anapelekwa hospitalini (uk. 121-123). Kutokana na dhima hii, Hikmat anasawiriwa kama mwana-mapinduzi. Anapigania haki za wanafunzi chuoni na kupinga uongozi mbaya wa chuo kikuu.

Miaka ishirini baada ya kumaliza masomo ya chuo kikuu, tunakutana na Hikmat akiwa mwanasiasa ambaye sasa anapigania kiti cha ubunge kupitia Chama cha Mwananchi ili aweze kuwakomboa wananchi dhidi ya umaskini na mateso mengi.

Msimulizi anatusimulia hivi:

Halaiki kubwa ilikusanyika kumwombea dua Hikmat wakati wa kuzindua rasmi kampeni za ubunge kwa Chama cha Mwananchi pale Ndotoni. Walimwombea ili awe na ujasiri katika kuwakomboa wananchi kutokana na umaskini na madhila mengine – kama alivyokuwa anafanya akiwa Chuo Kikuu cha Kuhisika.

(uk. 155)

Hikmat bado ni mwanaharakati. Kupitia hotuba yake kwa wananchi wa Ndotoni (akiwa fikrani), halaiki kubwa inakusanyika kumsikiliza, kumhimiza na kumwombea dua chini ya uongozi wa mhusika mzee. Ingawa chama chake hakina hela, Hikmat anawaomba wananchi wajitolee mhanga na kutegemea msaada wa Mwenyezi Mungu kama silaha

yao. Hikmat anawazindua wananchi kwa kuwaeleza jinsi wanavyokandamizwa na kudhulumwa na viongozi ambao hawaelewi matatizo yao. Anasema ufiisadi umekithiri Ndotoni ambapo kila mtu sharti atoe hongo (chirimiri) ndiposa asaidiwe katika sekta yoyote ya nchi. Anasema hivi:

Chirimiri sio tu ni adui wa haki bali pia ni kikwazo cha maendeleo. Chirimiri imeziathiri sekta zote za nchi yetu kiasi kuwa ili mtu apate haki yake hana budi kujipapasa. Kipimo kizuri cha mizizi ya chirimiri nchini ni kura za maoni za chama tawala zilizomalizika hivi karibuni. Chama tawala kimejijengea utawala wa vitisho na matumizi ya nguvu za hela. (uk. 156)

Hatimaye, Hikmat anaufafanulia umati manifesto ya Chama cha Mwananchi. Baadhi ya sera zake ni kujenga viwanda ili kutoa ajira kwa vijana, kuboresha sekta ya kilimo, kuunda serikali ndogo ya wizara kumi na tatu, kuboresha elimu hasa ya lazima na bure, kuimarisha afya ya wananchi, kuboresha usafiri, kufutilia mbali kodi na mwisho kuipanga upya sera ya kigeni (uk. 157-160). Kupitia kwa mhusika huyu, mtunzi anatumia wazi jinsi viongozi wa vyama hutoa ahadi kwa umma, na wanapopigiwa kura, hawazitimizi ahadi hizo na badala yake wanawanyanya waliowapa mamlaka. Anatumia uozo wa viongozi wa nchi yake.

Hikmat ni mhusika jumui. Anapotazama runinga, kuna kipindi cha *The Night of the Living Dead* ambacho kinaigizwa akilini mwake. Kuna mjadala unaohusu mataifa ya

Kiafra juu ya utekelezaji wa maazimio ya *Mirage* 0000. Wanajopo ni Ikmat, Kmat na Mat ambao ni nafsi nakili za Hikmat. Wanajadiliana kuhusu upujufu wa maadili; na jinsi viongozi hawawaonyeshi wananchi njia, badala yake wanatumikiwa tu na kusujudiwa. Hata wakulima hawawezeshwi kuzalisha chakula cha kutosha.

Mtunzi anamsawiri mhusika Hikmat kwa ubunifu mkubwa. Wanajopo Ikmat, Kmat na Mat wanaoendeleza mjadala ni nafsi za Hikmat.

Msimulizi anasema hivi:

Ingawa kulikuwa na wahusika wanne, hakika mhusika alikuwa ni mmoja – yeye. Ingawa kila mmoja alionyesha kutokuwa na upungufu wa uchambuzi yakinifu wa mwingine, wote walikuwa wanasema mambo ambayo yana ukweli ndani yake. Alikuwa ni mmoja tu. Si watu wanne. (uk. 181)

Isitoshe, Hikmat ambaye ni mtazamaji anabadilisha nafasi na kuwa mtangazaji. Anachangia mjadala wa wanajopo wenzake; yeye anakuwa mwanajopo wa nne. Mtunzi amevunja kaida ya uhusika katika hali hii.

Mtunzi anamsawiri Hikmat kama mhusika wa kimapinduzi ili kubainisha ujumbe mzito-matatizo yanayoikumba Kiafra. Baadhi ya masuala haya ni kuwa, lugha ya *F.M. Stations* ni ya kuaibisha, nyumba za ibada ni za kibiashara, jando la Kiafra (shule, familia, maabadini, n.k) limedhalilishwa; rasilmali/urithi wa Kiafra umegeuka kuwa mali ya wageni, ufisadi umekithiri, hakuna usalama wa kiafya na elimu si bora. Anawazindua

wananchi kuacha kujihurumia na kuhuzunika, na badala yake wapiganie haki, uhuru na usawa katika jamii. Anawaonya wasirejeele katu maandiko katika kitabu cha Maombolezo (4:8-9) katika Biblia Takatifu (uk. 172).

#### **2.4.2 Wahusika wadogo/ wasaidizi**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:125), mhusika mdogo au msaidizi ni mhusika ambaye hachukui nafasi kubwa katika kazi ya fasihi bali hutumiwa kujenga au kukuza dhamira fulani maalumu au kuwasaidia wahusika wakuu. Inawezekana wahusika wa aina hii wakawa na mchango fulani kwenye dhamira kuu lakini nafasi yao inabaki kuwa ndogo. Wahusika wasaidizi hutumiwa kumsaidia msomaji amwelewe vyema mhusika mkuu. Kupitia maingiliano baina ya mhusika mkuu na mhusika msaidizi, tunapata mwanga zaidi kuhusu hulka na wasifu wa mhusika mkuu. Matapo haya mawili yanategemeana (Njogu na Chimerah 1999:41-42). Wafuatao ni mifano ya wahusika wasaidizi katika *Watu wa Gehenna*.

##### **(a) MKUU**

Huyu ni mhusika wa kimwingilianomatini. Mhusika huyu anabainika kupitia mazungumzo yake na Eks Ngwenyama. Yeye ni mkubwa, kwa maana ya kuwa, ana mamlaka na uwezo juu ya binadamu na viumbe wengine. Kama alivyo Mungu katika Biblia Takatifu ndivyo alivyo mhusika MKUU katika *Watu wa Gehenna*.

MKUU anasawiriwa katika mandhari ya kinjozi. Anahojiana na Eks kwa muda wa miaka saba Eks akiwa amekufa, kwa hivyo hayuko katika ulimwengu halisi.

Msimulizi anasema:

Baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kulichukua miaka saba. Katika miaka hiyo saba, MKUU na Eks walikuwa wanaulizana na kujibizana. MKUU akiuliza maswali naye Eks akimjibu (uk. 30).

Ili kudhihirisha uwezo wake, MKUU anaelewa mambo yote yaliyojiri baina ya Eks na Mzee Afisul katika mazungumzo yake yaliyohusu 'binadamu ni nani', na ikiwa ana akili razini. Kisha anamwonya dhidi ya kupotoshwa na Mzee Afisul kwa kupewa maelezo maovu kuhusu sataranji. Kutokana na uwezo wake, MKUU anamwuliza Eks aliyoyaona anapokuwa mfu; na Eks anapokosa kumtaja yote aliyoyaona, MKUU anamkumbusha. Hatimaye MKUU anamuelekeza na kumfafanulia Eks umuhimu wa matunda na mboga ambavyo Eks na mkewe waliona ni vyakula vya sungura (huku wakipendelea nyama). MKUU anamwambia kuwa laiti Takosani angekula vyakula hivi ambavyo vina manufaa kwa mwili wa binadamu, wanalimpata mtoto (uk. 30-35). Ni muhimu kubaini hapa kuwa mhusika MKUU amesawiriwa ili kuukosoa mtazamo uliopo kuwa mboga na matunda ni vyakula vya sungura. Mungu ameviumba kwa manufaa ya binadamu.

Katika mazungumzo zaidi, MKUU anampa Eks amri saba zitakazomfariji kutokana na huzuni na ukiwa wa kumpoteza mkewe Takosani na kumlaumu Mzee Afisul kwa kutojua kwake mwenyewe (uk. 20, 36). Amri hizi zinadhahirisha uwezo mkubwa wa MKUU. Anamliwaza na kumshauri ahame Mvita na kwenda kumtafuta mchumba Al Jazeera Al

Khadra. Isitoshe, anarudisha umri wake nyuma (kutoka miaka 70 hadi 23) ili aweze kuishi maisha mapya.

Hatimaye, MKUU anamtolea Eks hotuba kuhusu matatizo yanayowakumba watu duniani hasa Kiafra. Kutokana na ukuu wake (ule uwezo wake wa kiungu), anafahamu vyema kinachowasumbua watu ulimwenguni. Anasema wakiafra wana matatizo ya kiafya kutokana na kutotilia maanani dawa za asili huku wakizipapia dawa za nchi za magharibi, zenye gharama ya juu (uk. 36-37). Yafuatayo ni maneno ya MKUU kwa Eks:

Mungu alipomuumba mwanadamu alimwekea duniani kila aina ya miti kwa matumizi mbalimbali na moja ya matumizi hayo ilikuwa ni dawa. Kwa hivyo, duniani kuna dawa za kutibu kila ugonjwa pamoja na ugonjwa hatari wa dhambi. (uk. 37)

Kwamba, ulimwenguni kuna dawa za kutibu kila ugonjwa ukiwemo ukimwi. Hata anarejelea maandishi katika Biblia. Mkuu anamweleza Eks kuwa, adui mkubwa wa mwanadamu ni maendeleo (uk. 38). Kwamba, binadamu anatengeneza ndege bila kutengeneza mahali pa kuiegsha hewani. Pia, anatengeneza simu za mkono bila kujenga hospitali za kutibu saratani inayosababishwa na simu hizo za mkono. Anaunda magari na kuyaendesha akiwa mlevi; na kusababisha ajali halafu anamlaumu Mungu. Anatengeneza umeme, ukiwaunguza watu wanamlaumu Mungu. Kwa hivyo, binadamu mwenyewe anapaswa ajilaumu kwa matatizo yanayomkumba (uk. 37-38).

Katika usawiri wa mhusika huyu, MKUU anamshauri binadamu wamrudie Mungu na kumtegemea na atawaponya kwa utaalamu wake, kwa kuwa “vyote vilivyomo ndani yake ni mali ya Mungu. Utukufu ni wake milele na milele, amina” (uk. 39). Anawaonya watu dhidi ya kunyanyasa wengine. Ukuu wa MKUU unajitokeza zaidi kupitia matendo yake. Kwa mfano, baada ya kumpa Eks amri saba, anafyatuka na kufifia angani kisha anarudi kumtolea binadamu ushauri (uk. 36).

Katika mandhari mengine tofauti ya kinjozi, mhusika MKUU anamweleza Kasisi Yunasi mambo yatakayotokea baadaye kupitia kwa sauti anayoisikia Yunasi. Akimwandikia Kasisi Taabu barua pepe (uk. 146-147), Kasisi Yunasi anamweleza yote aliyoambiwa na sauti ya MKUU. Ujumbe unahusu mlipuko wa jengo kubwa la *Gehenna Systems Centre Inc.* kule New York ambamo Yunasi na Saida (mkewe) wanafanya kazi. Hakika, aliyosema MKUU yanafanyika na kukamilika (ingawa ni katika mandhari ya kinjozi). Hili ni dhihirisho kuwa mhusika MKUU kweli ni mkubwa na mwenye uwezo mkubwa wa kuona yaliyopita, yaliyopo na yajayo ulimwenguni. Ni mhusika anayesimamia haki na ukweli duniani. Anawatetea wanadamu na kuwaonya dhidi ya maelekezo maovu ya Mzee Afisul.

### **(b) Sikujua**

Huyu ni mhusika mdogo katika *Watu wa Gehenna*. Ni rafiki mkubwa wa Mwalimu Baya. Anasawiriwa kupitia maelezo ya msimulizi kuhusu wasifu na maisha yake. Sikujua hajawahi kuoza na anatafuta mwanamke wa maisha yake (uk. 41). Anapokuwa njiani kwenda kumtembelea rafikiye, Mwalimu Baya, anakutana na totooshoo maridadi na

analipenda kwa mara ya kwanza. Anaanza uhusiano nalo na anasahau kuwa alikuwa yuaenda kwa rafikiye, Baya.

Sikujua amepewa jina la kimajazi. Neno 'sikujua' lina maana ya kutokuwa na ufahamu wa jambo fulani (ujinga). Mhusika Sikujua anapokutana na Takosani binti Inatesh njiani, anashawishika haraka na urembo wake na anakatiza safari yake kwenda kwa Baya. Kile ambacho hajui ni kuwa mwanamke huyu ni 'jini' au ni binti ya shetani kama jina lake linavyoashiria, na wala si binadamu halisi.

Mhusika huyu anasawiriwa zaidi kupitia mazungumzo yake na Takosani binti Inatesh. Ni mhusika asiyekuwa mwangalifu na ana pupa. Mara tu baada ya kukutana na Takosani katika mtaa wa *Reficul Meadows* (uk. 44), anampenda na kupendekeza awe mke wake. Hata ingawa Takosani 'anamkatalia' mwanzoni, Sikujua anashikilia wazo la kutaka kumuoa na kwamba angekuwa mume bora. Anamwambia:

Takosani, wanaume wanatofautiana. Niamini naweza  
kuwa mume bora (uk. 41).

Katika mazungumzo yao, Takosani anagusia masuala mazito ambayo yangemtanabahisha Sikujua kumchunguza zaidi lakini wapi, anakuwa zumbukuku! Mfano ni pale anapomweleza masharti yake ya kuombea kaburi la mamake kila usiku; kuogelea baharini na kupenda kuona michezo mingi isiyo ya kawaida (uk. 42-43). Hata hivyo, Sikujua ni zumbukuku wa kutoweza kufahamu na kuyafumbua mafumbo hayo ya Takosani na anang'ang'ania kumpenda tu. Vilevile, hakuwa makini wa kutambua matendo ya kiajabu ya Takosani. Kwa mfano, Takosani anapoondoka kwake Sikujua

asubuhi moja, anaondoka kupitia ukutani (si mlangoni) na Sikujua hatambui jambo hilo. Hizi zote zilikuwa ishara za kudokeza uhusika wa Takosani binti Inatesh.

Sikujua ni mhusika anayeshawishika upesi hasa kwa kupofushwa na 'penzi' lake kwa Takosani binti Inatesh. Kwa mfano, anapomwambia Takosani anaongea kama 'jini' kwa kutaka kumpa utajiri, na pia, anapofumba macho na wanajikuta pangoni; Takosani anakataa na kusema yeye ni binadamu halisi na hajui mambo ya majini. Sikujua anakubali ushawishi wa Takosani (uk. 49). Ishara nyingine ambayo Sikujua anashindwa kubaini ni hali ya Takosani kutaka santuri ya 'Mwaka wa Shetani' na kumfafanulia kuwa maandishi yameandikwa kinyumenyume; ni *Inatesh aw akawm* (uk. 51-52). Yeye anausikiliza wimbo huo tu bila kudadisi zaidi.

Kupitia mbinu rejeshi, Sikujua ni mhusika ambaye aliwahi kuwa mbunge na anapokuwa mbunge, anashiriki maovu kadhaa yakiwemo vita vya kikabila, mauaji ya watu baada ya uchaguzi na kuwapotosha watu kwa kutumia nguvu za giza kupata cheo cha ubunge. Pia anakata maelfu ya miti na kunyakua ardhi; na aliwaua watu 666 na akapewa tuzo ya *Knight in the National Order of the Legion of Honour*. Vilevile aliwahi kutumia dawa ya kuongeza nguvu za kiume zinazotokana na uchawi na pia kumhimiza mwanamke fulani kutumia dawa iliyotoka kwa wachawi ili kutengeneza ubikira bandia (uk. 60-62). Sikujua alipenda kusoma *The Codex Gigas*<sup>12</sup> ambayo ni biblia ya shetani. Kwa sababu ya makosa haya, Sikujua anaadhibiwa vikali kwa kutandikwa bila huruma na wapambe wa Takosani binti Inatesh.

---

<sup>12</sup> *The Codex Gigas* ni biblia ya shetani. Inaitwa hivyo kwa sababu ya picha kubwa ya shetani iliyomo ndani yake. Inaaminika iliundwa katika karne ya 13 (Olali 2012:274)

Mtunzi anamsawiri mhusika Sikujua kwa njia ya kuendeleza dhamira kuwa viongozi wanaotawala vibaya lazima watagunduliwa na kuadhibiwa kwa matendo yao wanapokuwa uongozini.

Katika mandhari ya kinjozi, Sikujua anashiriki biashara ya miili ya nyeti za maalbino. Haya yanajitokeza wazi katika *mchezo wa ukweli* unaochezwa na wahusika watatu: Sikujua, *The Codex Gigas* na Daktari Majini Tisa. Mchezo huu unaigizwa akilini mwa Sikujua (uk. 62-65).

Kutokana na matendo yake, Sikujua ni mtovu wa maaadili; hana adabu wala soni. Msimulizi anasema baada ya kugutuka kutoka *mchezo wa ukweli* anashikana na mrembo wake Takosani kwenda kustarehe ufukweni Vumawimbi. Huko, wanafanya mapenzi bila kujali macho ya wavuvi waliokuwa wakisafisha ngalawa zao (uk. 65-66).

Sikujua, kwa sababu ya kutojua, anaingizwa katika ushetani na Takosani binti Inatesh na anaanza kuvalia kihuni na kukata nywele zake mtindo wa kiajabu. Baadaye, anashirikiana na Takosani kumuua kasisi Yunasi na familia yake baada ya kuwaibia gari lao. Anakamatwa na polisi na kuwekwa rumande, huku rafiki yake (Takosani) akikiri kwamba yeye ni mtumishi wa shetani (uk. 214-216).

Kwa ujumla, Sikujua ni mhusika bapa-kielelezo; hakubadili msimamo wake wa kumpenda toto shoo Takosani binti Inatesh kuanzia mwanzo hadi mwisho. Licha ya kushuhudia ishara za kiajabuajabu, anashikilia tu kumpenda na hatimaye anakuwa mshiriki wa Takosani katika 'ushetani'.

### **(c) Takosani binti Inatesh**

Msimulizi anamweleza Takosani kama “totoshoo maridadi” anapokutana na Sikujua katika *Reficul Meadows*. Jina lake ni Takosani lakini alipewa jina ‘Inatesh’ kule *Reficul Meadows* (uk. 41).

Kupitia maelezo ya msimulizi, tunapata wasifu wa Takosani. Tunaambiwa:

Miguu yake mieupe yenye umbo la kuvutia wanaume  
wengi ilizidi kumfanya ajione kiumbe mwenye bahati,  
pua yake yenye asili ya Msomali hakika hungeweza  
kuamini kama mrembo ni Mbajuni wa Faza ama  
Mdawida kutoka Bura Ndogo. Alikuwa mrefu wa futi  
sita, ngozi yake ilitawaliwa na manyoya mengi mpaka  
mashavuni (uk. 45).

Mtunzi anamsawiri mhusika huyu kupitia mazungumzo yake na Sikujua. Tunapata kujua wasifu wake kuwa aliwahi kuolewa na Mwarabu na ndoa ikavunjika baada ya siku saba. Anasema wanaume wamemtenda na anataka abaki peke yake, asiolewe tena.

Sikujua anapopendekeza kumuoa, Takosani binti Inatesh anamwekea masharti kadhaa ambayo anaona (Sikujua) angeshindwa kuyatimiza. Masharti haya yalikuwa kuombea kaburi la mama yake kila usiku kule Kizingitini, kisiwani Pate, kwa kulipigia magoti na kuziweka sarafu juu yake. Pia anapenda kuoga baharini na kutazama michezo mingi ya ajabu ambayo Sikujua asingependa kuitazama. Masharti haya yanaashiria sifa na wasifu wa Takosani, kwamba si mhusika binadamu wa kawaida. Yeye ni mfuasi wa shetani na

ana sifa za kishetani. Hata anamwambia Sikujua kuwa hajamjua, na akimjua atamwacha (uk. 42-45).

Kwa maelezo ya msimulizi Takosani ni mhusika mnafikiki/ mwenye hila na asiyeleweka. Unafiki wake unajitokeza pale ambapo analia kwa uchungu akimwomba Sikujua asimuo kwa maana asingetii masharti yake. Ukweli ni kwamba, anamfumba macho tu asitambue yeye ni nani. Vilevile, Sikujua anapomwambia anaongea kama jini pale anapotaka kumpa utajiri, Takosani anakana akisema yeye si jini na hadithi za majini haziamini yeye; pia, anasema, hajui kama majini wapo na anadai yeye ni binadamu halisi (uk. 48-49).

Mhusika huyu vilevile anasawiriwa kupitia matendo yake ambayo yanatuelekeza kwenye wasifu wake. Mfano mzuri ni pale anapoagana na Sikujua chumbani mwake, anaondoka kupitia ukutani, sio mlangoni. Vilevile anampeleka Sikujua kimiujiza hadi mapangoni na chumbani mwake na kumwomba santuri ya 'mwaka wa shetani' na kuisikiliza kinyumenyume. Matendo haya ni dhahirisho kamili kuwa Takosani ni jini, sio mhusika binadamu. Anasawiriwa kinjozi. Hata manukato chapa ya *poison* ambayo anajifukiza ni ishara ya uhusika wake - ni jini (uk. 47).

Takosani ni mhusika katili na mpinzani mkubwa wa MKUU. Akishirikiana na Sikujua, anamwua kasisi Yunasi, mkewe Saida na watoto wao wawili kwa kuwapiga risasi. Alikuwa katika gari la mama yake aina ya *Nyayow Payonia*, akiwa na Sikujua. Mwanzoni, wanavunja kasha katika kitengo cha udhibiti wa silaha na kuiba bunduki aina ya *metal storm* na makasha mawili ya risasi. Takosani anatumia ujanja kwa kuwa anachukua

fedha, vitu vya thamani na vitambulisho vyote vya familia vya Yunasi ili kuchelewesha kutambulishwa kwao (uk. 214-215).

Kwa maelezo ya msimulizi, Takosani ana sura ya kihuni. Anaonekana kama mtumiaji wa dawa za kulevya, amejichora picha za kutisha katika mwili, amejitoga masikioni, puani, kwenye ulimi, udevuni, midomoni, kwenye nyusi na kujivika vipuri. Isitoshe amekata nywele kwa mtindo wa ajabu. Takosani alikuwa amevalia fulana iliyochorwa mafuvu ya watu na picha ya joka kubwa (uk. 214-215). Hizi ni sifa kihuni.

Takosani binti Inatesh<sup>13</sup> ni mhusika ambaye ni mtumishi wa shetani. Anakiri ndiye aliyepanga njama ya mauaji ya familia ya Yunasi; kwamba yeye ni mpinzani wa Masihi Yesu Kristo na ni binti wa shetani ambaye ameweka imani yake kwa msingi wa *The Codex Gigas*. Msimulizi anatuambia hivi:

Takosani alikiri kuwa yeye alikuwa mpinzani wa Masihi Yesu Kristo na binti wa shetani. Alizidi kusesitiza kuwa maisha yake yalitawaliwa na nadharia za ajabu kiasi cha kuasi imani ya Kikristo aliyokuwa nayo mama yake. Akifanya haya yote, alikuwa ameweka imani yake kwa msingi wa kitabu kimoja – *The Codex Gigas* (uk. 217).

---

<sup>13</sup> *Inatesh* – neno hili limeandikwa kinyumenyume; ni ‘shetani’ – mpinzani mkuu wa Mungu.

Takosani anakiri kuwa ana mpango ulioratibiwa na shetani wa kuwaandaa vijana wote duniani ili waasi. Anaamini vita vya mwisho vya 'Armageddon'<sup>14</sup> vilikuwa karibu kuanza lakini baba yake, shetani, hakuwa amemwambia tarehe maalum vita hivyo vitakavyoanza (uk. 218).

Mtunzi anamtumia mhusika Takosani kuendeleza dhamira ya uhalisiajabu. Takosani ni mhusika bapa-kielelezo ambaye habadiliki katika mtazamo wake wa ushetani. Alikuwa mtumishi wa shetani kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi kama anavyokiri mwenyewe. Anapewa jina linaloashiria yeye ni binti wa shetani; na anaelewa na kutekeleza mipango ya ushetani.

**(d) Mishi binti Bwan Rehema**

Mhusika Mishi amesawiriwa kupitia kwa maelezo ya msimulizi ambaye anatupa wasifu wake kwa mkupuo. Anatuambia:

Dada huyo alikuwa shombe, kwani licha ya ngozi yake kuonyesha kuchanganya damu, nywele zake zilikuwa za Kiarabu. Alikuwa ameiteremsha ile kanga aliyojitanda kichwani. Mashavu yake yalikuwa yameumuka sawia, huku macho yake yakiwa yamefunikwa kwa wanja. Midomo yake iliiva kwa rangi nyekundu ya midomoni (uk.103).

---

<sup>14</sup> *Armageddon* – kulingana na kitabu cha Ufunuo wa Yohana 16:14, *Armageddon* ni mahali ambapo panaaminiwa vita vya mwisho wa ulimwengu vitapiganiwa. Lina asili katika Kiebrania kumaanisha 'Mlima wa Har-Magedoni'.

Mishi anapenda marembo ya wanawake na zaidi kujiremba usoni na kuvalia mapambo mazuri. Msimulizi anasema haya kumhusu Mishi:

Shingoni alikuwa amevalia mkufu wa dhahabu ulioendana na herini zake na bangili alizokuwa amevaa mkono wa kushoto. Kwa kweli alikuwa malkia wa malkia wote (uk. 115).

Huu ni wakati ambapo Mishi akiwa na mtoto Saida anaomba lifti usiku mmoja kutoka kwa Baya. Aliomba afikishiwe Chumbageni, nyumbani kwake. Mwalimu Baya anavutiwa na ‘uzuri’ wa mhusika Mishi binti Bwan Rehema. Katika mazungumzo na Mwalimu Baya, Mishi anajitokeza kama mwanamke mwenye tahadhari. K.m jinsi anavyomwitikia Baya ‘naam’ inamvutia mno. Hata hivyo Mishi, anadharau hali ya kuwa Baya ana cheo cha ualimu ilhali ni kijana mdogo. Anaona zipo kazi nyingine ambazo Baya angeweza kufanya (uk. 104).

Matendo ya Mishi yanamsawiri kinjozi na kuashiria yeye ni nani. Mwalimu Baya anapokuwa anampeleka Mishi Chumbageni katika gari lake la Vokswageni, gari linakwama kwenye njia ya reli huku treni ikiwa imefika. Licha ya kuwa treni inaelekea kuwagonga, Mishi anatulia kwenye kiti chake na anaangalia mbele bila ya hofu yoyote. Hii ni ajabu! (uk. 106). Pili, Mishi anakunjua mikono na kumkumbatia Baya huku akisema neno ‘shemhamforash’<sup>15</sup> kabla treni haijagonga Vokswageni yake. Hakika, treni ilipita ‘ndani yao’ bila kuwagonga na wakanusurika wote. Kupitia tukio hili, Mishi

---

<sup>15</sup> *Shemhamforash* – zamani, neno hili lilitumiwa kumrejelea mungu wa Kiebrania (“Yahweh”). Lakini siku hizi, linatumiwa kama kifungu cha kishetani badala Mungu wa Kiebrania. K.m *Hail Satan, shemhamforash!*

anatumiwa na mtunzi kukuza dhamira ya uhalisiajabu; na kuonyesha jinsi mhusika huyu si binadamu wa kawaida, ni jini. Pia, anaashiria kuwa 'yote yang'aayo si dhahabu' kama ambavyo Mwalimu Baya anafikiri kutokana na wasifu wa nje wa Mishi.

Mhusika Mishi ni wa kinjozi, ni jini. Baada ya Mishi kumuaga Mwalimu Baya, kunasikika mlio wa 'ko ko ko' kama vile mtu aliyevaa viatu vya mchuchumio alikuwa akitembea na vilitoa mlio kama vile mbao hutoa ikigonga sakafu. Hatimaye, msimulizi anatumbea maumbile kamili ya mhusika Mishi binti Bwan Rehema. Miguu yake ilikuwa ya kwato za ng'ombe na ana magamba mgongoni. Mishi anapotamka tu neno 'shemhamforash', mwili wake unatoa mwanga wenye rangi ya mbalamwezi angavu. Alikuwa na jicho moja kwenye paji la uso wake, na mwili wake ulikuwa nusu toka juu hadi chini: titi moja, mkono mmoja, mguu mmoja, nusu ya kila kitu. Kwa maelezo ya Mzee, Mishi alikuwa shetani wa mahaba kutoka Gehenna, na kwamba aliwahi kuwa mke wa Shemhamforash (uk. 117-118).

Mtunzi anamtumia mhusika Mishi kuendeleza ujumbe wa uhalisiajabu na kutoa mafunzo kuwa mtu asidanganyike na maumbile ya nje anayoyaona kwa mara ya kwanza. Pia, ni muhimu kuwa makini na kutilia maanani mazungumzo na matendo yasiyo ya kawaida ya mhusika yeyote yule.

**(e) Saida**

Huyu ni mhusika mdogo katika *Watu wa Gehenna*. Yeye ni mhusika duara au mviringo. Mtunzi anamsawiri tangu awe mtoto mdogo anapokuwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu hadi utu uzima anapolewa na mchungaji Yunasi na kuhamia New York anakopata ajira.

Katika hatua hizi za maisha, Saida anabadilika kulingana na wakati na mazingira yanayomzunguka.

Mwanzoni, Saida anasawiriwa akiwa mtoto mdogo anapopatikana njiani na Mishi (dada ya mamake) wakimwomba Mwalimu Baya lifti awapeleke hadi nyumbani, Masiwani. Katika mandhari ya kinjozi, Saida anachorwa kama jini pale anapopatikana garini mwa Mwalimu Baya kimiujiza baada ya kuachwa nyumbani kwa mamake awali. Kisha anatoweka ghafla. Hii ilikuwa ishara kuwa Saida si mhusika binadamu halisi. Saida akiwa mdogo anatamani kujiunga na Chuo Kikuu cha Kuhisika, ili apate heshima ambayo angepewa kama msichana wa chuo kikuu (uk. 127).

Kupitia mawazo yake (uzungumzinafsia), tunapata kuufahamu mtazamo wa Saida kuhusu dini. Saida hapendi dini na anasema ina upungufu mkubwa kwa kuwa inawanyima wasichana uhuru wa kufanya jinsi wependavyo. Anasema amechoshwa na nasiha za *Sunday school* zinazomkera na makatazo na amri anazoonza zinamfunga kwenda magomani na kucheza beni za usiku. Anatamani kuvaa anavyotaka na kufanya anavyotaka. Mawazoni, Saida anakiri kuwa hajui hata dhehebu lake ila tu achoshwa na amri za ukristo zinazomtaka kufuata. Katika kuchukia dini, Saida anatamani mitindo mipya ya kisasa kama kuvaa nguo fupi (kibiritingoma) na kutumia vipodozi usoni mwake. Anatamani wakati atakapofikia 'maendeleo' (uk. 128). Kutokana na hamu ya kutaka 'uhuru' wa kidini, Saida anasoma kwa bidii na anajiunga na chuo kikuu baada ya kufaulu sekondari kwa matokeo mazuri.

Katika mazungumzo yake na Siyawezi, Saida anadai kuwa madhehebu mengi huleta fujo hadharani. Mifano ni Legio Maria, Wakorino, Dini ya Msambwa, *African Israel Church Nineveh*, Dini ya Roho, *Israel Silimbika International Church* na *Roho Revelation Church*. Ni bayana kuwa Saida ni mwasi wa kanuni za kidini (uk. 131).

Kupitia maelezo ya msimulizi, tunasawiriwa wasifu wa Saida anapokuwa chuoni. Kwanza, anapenda starehe na raha. Anapapia usasa kwelikweli - mitindo ya kisasa, fashoni na nguo za fahari, vitu vya urembo, vipindi vya televisheni na nyimbo za video za kisasa. Marafiki zake ambao anashiriki nao starehe walikuwa wajeuri. Saida anajivunia mavazi kutoka nchi za kigeni kama Ufaransa. Anakengeuka kabisa na jamii yake akawa anamwambia Siyawezi yeye hana dini (uk. 128-129).

Utovu wa maadili na ukengeushi unazidi kubainika kupitia matendo yake akiwa na marafiki zake Kinaya, Pasua, na Ujana wa Chuo Kikuu cha Kuhisika. Kwanza, wakiwa katika *Student Centre*, wanasikiliza nyimbo zenye ujumbe wa kishetani kwa mfano, *Gehenna in Sight* (uk. 132). Licha ya ushauri wa Siyawezi kwao, wanampuuza. Saida na wenzake wanahudhuria karamu ya watu wengine bila ya kualikwa na nusura waiharibu karamu. Saida anavalia kibiritingoma, kimini ambacho nusura kionyeshe nyeti zake. Anapopandwa na madadi ya muziki, anacheza na kuvua nguo hadharani huku akibaki uchi wa binadamu (uk. 138-139). Matendo haya yanaonyesha utovu wa maadili wa hali ya juu; kupenda anasa na ulevi.

Baada ya *stag party*, Saida anaugua na analazwa hospitalini. Marafiki zake wote wanamtoroka ila tu Siyawezi ambaye anamtembelea na kumpelekea nakala za

mihadhara ya masomo. Tukio hili linambadilisha kabisa Saida ambaye anabadili mwenendo wake na fikra zake za uhuru, maendeleo na usasa. Msimulizi anamsawiri akijutia jinsi hapo mwanzoni, alivyomdharau Siyawezi chuoni. Matukio haya yanadhihirisha uduara wa mhusika Saida. Saida anauchukua mtazamo mpya kuhusu maisha kwa ujumla. Anasema:

Usasa si kukataa dini na maadili na kung'ang'ania fikira na tamaduni ambazo zipo mbali na dini yake. Sasa alifahamu ya kuwa uhuru si katika tu kuzuia ukaidi wa nafsi na kukosekana kwa unyenyekevu wa matarajio bali ni kujisalimisha kwa wasiwasi. Sasa alifahamu ya kuwa dini ya kikristo imemthamini mwanamke pamoja na uhuru wake na kumpatia haki zake (uk. 143).

Saida anaazimia kubadilisha maisha yake kulingana na sheria ya Mungu aliyetukuka. Mtunzi anamtumia mhusika Saida kuonyesha kuwa 'mui huwa mwema' na kilicho na mwanzo, huwa na mwisho. Mtunzi anamsawiri Saida kama kiumbe aliyebadilika na anakamilisha masomo yake ya Chuo Kikuu cha Kuhisika na kufuzu.

Saida anaolewa na mchungaji Yunasi na wanahamia New York wanakopata kazi nzuri katika jengo la *Gehenna Systems Centre* (GSC). Wanayafurahia maisha yao.

Wakati mmoja, kunatokea mlipuko wa jengo la GSC ambalo linadondoka lote (zaidi ya ghorofa 999), lakini Saida ananusurika kutokana na kuchelewa kufika kazini siku hiyo.

Tukio hili la kunusurika linambadilisha zaidi Saida ambaye anatambua ya kuwa mipango ya mwanadamu ni tofauti na mipango ya Mungu. Anabaini umuhimu wa kumkubali Yesu mapema na hata anamkumbuka Siyawezi na nasaha zake kwake wakiwa chuoni Kuhisika. Ujumbe tunaoupata ni kwamba, ni muhimu binadamu kumkubali Yesu mapema kwa kuwa, mtu huwa hajui siku wala saa kama anavyosema kasisi Yunasi.

Hatimaye, Saida pamoja na familia yake wanauawa na Takosani binti Bwan Rehema na Sikujua wakiwa katika gari lao (uk. 212). Hadithi inapomalizika katika mandhari ya kinjozi, Saida ni mmoja wa watu wa Gehenna. Analia kwa uchungu akitafuta usaidizi (uk. 219). Hii inaashiria kuwa Saida hakuokoka na kumkubali Yesu.

#### **(f) Siyawezi**

Ni dadake Baingana na ni mtoto wa Lakeisha. Alilelewa na baba wa kambo, Eks Ngwenyama. Akiwa mdogo, Siyawezi alikuwa na ndoto ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Kuhisika na kusomea Kiingereza na Elimu ya Uhasibu.

Maisha ya awali yanakuwa mazuri hadi pale mama yao anapowatelekeza baada ya kuolewa na mume mwingine anayempata kwenye mtandao wa *facebook*. Pamoja na nduguye, Siyawezi anakulia kuwa mwizi na mwuzaji wa unga wa kulevya, hali inayompelekea kutiwa mbaroni na kufungwa jela miaka mitatu. Anapotoka kizuizini akiwa na umri wa miaka 16, Siyawezi anabadilika zaidi; anajiita *sweet sixteen* na anajuana na wanaume wengi matajiri; ambapo mmoja wao anamtia mbaroni na kumfunga jela tena.

Wakati huu, maisha ya jela yanambadilisha Siyawezi kabisa kitabia. Kwa maelezo ya msimulizi, anatoka jela akiwa mcha Mungu aliyeongoka na akawa anamwogopa Mola wake. Anashika ibada sawasawa na kuacha kuvaa kibiringoma. Anaingia shuleni na kusoma kwa bidii na hatimaye anafuzu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Kuhisika ili akasomee masomo ya Kiingereza na Elimu ya Uhasibu.

Kweli, Siyawezi ni mhusika mviringo. Mtunzi anamsawiri toka utotoni akiwa mwenye furaha nyumbani kwao, akabadilika na kuwa mwizi kutokana na maisha magumu ya 'kiyatima', akafungwa jela na mwishowe, kubadilisha mwenendo na kuwa msichana mwadilifu na mcha Mungu.

Siyawezi pia anasawiriwa kupitia mazungumzo yake na Akilimali Van Krockoff kuhusu katiba kielelezo. Anamuunga mkono mgombea kiti cha ugavana. Krockoff anapomtanabahisha kuhusu viongozi na vyama, Siyawezi anakubaliana naye kuwa ni vizuri kuunda na kujenga vyama vinavyowajali wananchi kuliko vinavyojali maslahi ya wanasiasa binafsi. Katika mazungumzo kuhusu siasa na ushirikina, Siyawezi anakubali kuwa hata katika visiwa vya Pate kuna mafundi mahiri wa sayansi hii; mfano ukiwa Bi. Kirembwe. Wanasiasa hutumia uchawi na hata popobawa kuwadhulumu wapinzani wao. Anasema, imani ya ushirikina na masuala ya majini, mazimwi na wanga yana historia ndefu kisiwani Pate. Kupitia mazungumzo haya, tunajiwa na dhana kuwa, kuna ushirikina miongoni mwa wakiyafra, na viongozi hutumia nguvu za giza ili kupata uongozi.

Tunapokutana na Siyawezi katika Chuo Kikuu cha Kuhisika kama mwanafunzi, ni msichana nadhifu na mwadilifu. Kwa maelezo ya msimulizi, Siyawezi ni mkristo halisi na anafuata kanuni za kikristo. Anapenda kuvaa mavazi ambayo yanamsitiri vyema kulingana na mafunzo ya dini ya kikristo. Kutokana na uadilifu wake, Siyawezi anajipa jukumu la kuwanasihia wanafunzi wenzake wazingatie mafunzo ya kidini na nidhamu ya chuo. Katika mazungumzo yake na Saida na marafikize (Kinaya, Ujana na Pasua), anawashauri wazingatie kanuni za dini na kuvaa mavazi ya heshima. Hata wanaposikiliza nyimbo za 'kishetani, katika *Student Centre*, Siyawezi anawakabili kijasiri na anawaonya dhidi ya mwenendo huo. Anawaambia hivi:

Biblia na nyimbo za kilimwengu haziyumkini kukaa  
kwenye moyo mmoja ... Bali ikimakinika mojawapo  
katika moyo, huiondoa ile nyingine mara moja. (uk.  
134)

Saida anamwona Siyawezi kama msichana mrembo, mwenye nidhamu na mchapakazi. Licha ya kuwa mwanafunzi, Siyawezi anawafundisha baadhi ya wanafunzi wenzake chuoni lugha ya Kiingereza na Uhasibu. Vilevile, Siyawezi anasawiriwa kama mhusika mwenye utu. Licha ya kudharauliwa na Saida na marafiki zake, anamzuru (Saida) hospitalini anapokuwa mgonjwa na anampelekea nakala za mihadhara ya masomo aliyokosa. Marafiki zake Saida walikuwa wamemkimbia wakati anahitaji msaada wao (uk. 141-144).

Kwa kiasi fulani, jina la Siyawezi linaweza kuchukuliwa kama la kimajazi. Tukiyaangazia maisha yake, huenda Siyawezi hawezani na maisha ya kisasa kama wanavyoyaishi wenzake hususan Kinaya, Saida, Pasua na Ujana. Yeye alishikilia kanuni za dini na anaamua kuwa mwadilifu baada ya maisha yake ya uovu awali.

Kwa ujumla, Siyawezi amesawiriwa na mtunzi kama mhusika duara na mwadilifu. Alishikilia kanuni za kidini baada ya kubadilika na akawasaidia wenzake. Ametumiwa kufanikisha ujumbe wa umuhimu wa kuwa mwadilifu na kufuata kanuni za chuo na za dini.

## **2.5 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeshughulikia kipengele cha uhusika na wahusika. Tulitanguliza kwa kufafanua dhana za uhusika, wahusika na usawiri wa wahusika katika kazi za kifasihi. Kisha tukachunguza mbinu ambazo watunzi tofauti huzitumia katika kuwasawiri wahusika katika kazi zao za kifasihi. Tumezifafanua mbinu hizi na kutoa mifano ya wahusika waliosawiriwa kwa jinsi hizo katika riwaya tunayoishughulikia.

Hatimaye, tumechanganua makundi ya wahusika wanaopatikana katika riwaya teule ya *Watu wa Gehenna*. Tumewaweka katika makundi makuu: wahusika wakuu na wahusika wadogo/ wasaidizi pamoja na kufafanua aina zake hususan uduara/ mviringo, ubapa, jumui na wa kinjozi. Tumefafanua kwa undani sifa na wasifu wa wahusika tuliowateua katika makundi makuu mawili.

Hakika, mtunzi amefaulu katika kuwasawiri wahusika aliowatumia katika riwaya yake. Wahusika kwa jumla wameweza kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa njia inayoeleweka kutokana na usawiri wao na mazingira wanamojikuta.

## **SURA YA TATU: UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA WATU WA GEHENNA**

### **3.0 UTANGULIZI**

Semantiki ni tawi la isimu ambalo huchunguza uchambuzi wa lugha katika kiwango cha maana. Huchunguza maana ya maneno yanayopatikana katika lugha husika, iwe ya kifasihi au la (Wamitila 2003:190). Katika sura hii, tunashughulikia jinsi mwandishi amekiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuleta maana mbalimbali katika kazi yake; na pia matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyosawiriwa. Kwa ufupi, semantiki ni matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Tunajadili matumizi ya tamathali za usemi kwa sababu zina uhusiano na semantiki kwa kuwa zinabeba maana mbalimbali katika muktadha ambamo zinatumiwa.

### **3.1 TAMATHALI ZA USEMI.**

Kuhenga (1977) na Wamitila (2008) ni wataalamu ambao wameshughulikia dhana hii. Wamitila anazungumzia tamathali za usemi kama 'lugha ya kitamathali'. Anasema dhana ya tamathali inatumiwa kwa upana ili kujumlisha sifa nyingi za kimtindo ambazo hutumiwa katika kazi za kifasihi. Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa dhana hii hutumika kuelezea aina ya ukiushi wa kimakusudi katika matumizi ya lugha, na ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au wa kimuundo. Katika ukiukaji huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.

Mbatiah (2001:77) pia anakubali kuwa, tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo tamathali ya usemi ni fungu la

maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Lugha ya kitamathali huwa na umuhimu mkubwa katika utunzi wa kazi za kifasihi. Wamitila anabainisha majukumu matatu makuu ya lugha ya kitamathali. Kwanza, ni urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuji; Pili, ni jukumu la ufafanauaji au uelezaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum; na tatu, jukumu la uthabitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani. Majukumu haya matatu yanaweza kuhusishwa na lengo kuu la kuzua lugha au usemi wenye uwezo wa kushawishi. (Wamitila 2008:393).

Mbinu zote za kitamathali zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa. Huvutia nadhari ya hadhira na kuziathiri hisia zao. Hivi basi, tamathali za usemi ni mojawapo ya vigezo vya kupimia ubunifu na umbuji katika kazi fulani. Mifano ya tamathali za usemi ni sitiari, taashira, tashbihi, tashihisi, balagha, chuku, tanakuzi (oksimora), dhihaka, kinaya, kwelikinzani (paradoksi) na nyinginezo. Mbinu hizi zina uamili wake katika uwasilishaji wa dhamira ya kifasihi.

Hata mtaalamu Simpson (2004:41) anasema kuwa, tamathali hizi hupewa nafasi muhimu katika uhakiki wa kimtindo. Katika utafiti wetu, tunaangalia tu zile mbinu ambazo zinatufaa katika kuichanganua mada yetu.

### 3.1.1 Sitiari

Hii ni tamathali ya ulinganishi usiokuwa wa moja kwa moja. Haitumii maneno yanayoashiria ulinganishi ‘kama’, ‘ja’, ‘mfano wa’, ‘tamthili ya’, n.k. Tamathali hii hulinganisha vitu viwili kwa njia ya moja kwa moja. Hutumia sifa za kitu kimoja kuelezea kitu kingine bila kutumia kilinganishi (Njogu na Chimerah 1999:91; Wamitila 2008:397).

Wamitila anasema kuwa, msingi wa sitiari ni uhamishi wa maana. Kwa hivyo, ili uchunguzi wa sitiari ukamilike, sharti kuchunguza dhana tatu muhimu: kilinganishi (kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha); kilinganishwa (kile kinachofananishwa) na msingi (sifa yenyewe ya ulinganishi) (Wamitila 2008:421). Kwa mfano tukisema, ‘Bakari ni fisi karamuni’, kilinganishi ni fisi, kilinganishwa ni Bakari na msingi - ni sifa ya fisi kupapia kila aina ya chakula hata iwe mizoga iliyooza.

Katika *Watu wa Gehenna*, kuna mifano ifuatayo ya sitiari.

*Nitaliegesha **benzi** hili hapo* (uk. 68). Sitiari hii inatumiwa na dereva Faki Nahodha katika mazungumzo yake na Baadayadhiki. Faki anaita ‘gari’ lake ambalo ni aina ya ‘Tuk Tuk’ benzi. Hii inaonyesha jinsi Faki anavyothamini gari lake (Tuk Tuk) kwa sababu ndilo humpatia riziki ya kila siku. Analionea fahari na kuonyesha kuwa, hata ‘Tuk Tuk’ inaweza kutenda majukumu yale yale ya gari aina ya benzi.

*‘Naam’ ile ilitokea kwa mpango na kwa taratibu zote za jinsi neno linavyoweza kutoka kinywani mwa **malaika*** (uk. 104). Msimulizi anatumia sitiari ‘malaika’ kumlinganisha Mishi binti Bwan Rehema na malaika - kiumbe asiye na hatia, mzuri. Mishi aliitikia vizuri sana hali inayomfanya aonekane kama malaika. Kwa kweli, sitiari hii inatumiwa

kinyume kabisa kwa sababu Mishi anayedhaniwa kuwa ‘malaika’ alikuwa kinyume chake (ni shetani au jini); hata alikuwa na miguu ya kwato za ng’ombe na alikuwa mke wa ‘shemhamforash’ awali.

*Aliweka mizigo.....kwenye boneti iliyo mbele ya mgongo huo wa **kobe*** (uk. 103).

Msimulizi anatumia sitiari hii kulinganisha gari aina ya Vokswageni na mnyama ‘kobe’ kutokana na umbo lake ambalo ndio msingi wa kulinganisha.

Siyawezi anapowasihi Saida na marafikize kuhusu nyimbo za ‘kishetani’, anasema miongoni mwa wakristo kuna watu wanaolenga kuwapoteza **wanakondoo** kutoka njia ya Mwenyezi Mungu. Hapa wakristo wanalinganishwa na wanakondoo kwa maana ya watu wanaohitaji mwongozo, hifadhi na ulinzi dhidi ya watu waovu. Pia, Kinaya anasema waache mazungumzo na hao **wakaidi na wenye akili finyu** (uk. 135). Kisitiari hawa ni wakristo waliookoka na kamwe hawaungi mkono mitindo ya maisha ya kisasa na utovu wa maadili pamoja na uvunjaji wa kanuni za chuo. Pia tunaambiwa kuwa, *“Mahudhurio (katika nyumba za ibada).....huwa hafifu.....haijulikana kama ni **wachungaji** wamefungukiwa uwezo au **kondoo** wamekuwa watukufu....”* (uk. 170).

Katika sitiari hii, viongozi wa kanisa wanalinganishwa na wachungaji huku wafuasi wakilinganishwa na kondoo. Sitiari hii inatumiwa kuonyesha namna kiwango cha maadili kimeshuka hadi wafuasi hawaendi makanisani.

*Meza yao ilikuwa ni **msitu** wa chupa zisizokuwa na chapa za kileo kikali* (uk. 138). Ni wakati Ujana, Kinaya na Saida wakiwa katika *Student Centre* ya chuo kikuu wakistarehe kwa vinywaji. Wengi wa chupa za kileo ambacho walikuwa wamekunywa

unalinganishwa na msitu/miti mingi; walikuwa wamekunywa vileo vingi mno. Sitiari hii inatumiwa kudhihirisha tabia mbaya na kiwango cha ulevi wa wanafunzi hawa wa kike katika Chuo Kikuu cha Kuhisika.

*Mkamateni huyo! Ni **investment*** (uk. 185). Huu ni wakati watu wakiongozwa na Bi. Saeeda Khan, wanamfukuza Baingana ili wamshike. Baingana analinganishwa na *investment* (kiwekeza) kwa kuwa yeye ni zeruzeru na kwa kawaida maalbino wanauawa na sehemu za miili yao zikauzwa ili kupata pesa nyingi. Sitiari hii inaonyesha jinsi biashara ya nyeti za maalbino inavyoendelezwa na watu ambao hawawaoni mazeruzeru kama binadamu. Watu wanatumia viungo vya maalbino kutokana na imani zao za kishirikina hasa wanasiasa.

*Waheshimiwa hulipwa kwa kuweka **sponji** zao juu ya sponji za viti vile maalum* (uk. 204). Hapa msimulizi analinganisha makalio ya wanasiasa (wabunge) na sponji (ya kwanza). Ujumbe ni kwamba wanasiasa hulipwa mishahara mikubwa kwa kuonekana tu katika jengo la bunge na kukalia viti vizuri (sponji ya pili) bali si kwa kuchangia mijadala maalum itakayoleta maendeleo nchini. Pia, *lazima wapambane na **vuvuzela**.....* (uk. 204). Sitiari ya vuvuzela inaashiria wanasiasa ambao kazi yao ni kuropoka tu na kutoa ahadi za uongo kwa raia. Hii ni sifa ya vuvuzela, yaani, kutoa mlio wa sauti ya juu. Katika muktadha huu vilevile, kuna sitiari ya kulinganisha idadi ya wabunge na idadi ya **matako** na kwamba spika ataongea na kuta (uk. 206). Sitiari hii inaonyesha jinsi wabunge wachache sana wanahudhuria vikao vya bunge kwa kuwa hakuna sheria kuhusu idadi ya

wanaohudhuria. Hivi basi wabunge wanakosa kuwajibika ilhali wanalipwa mishahara mikubwa.

### **3.1.2 Jazanda**

Huwa na muundo wa kisitari. Jazanda ni mafumbo ambamo ndanimwe maana ya kitu imefichamana. Ni sawa na 'istiara' yaani "kilichositiriwa" (Njogu na Chimerah 1999:32). Istiara ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea aina fulani ya sitari iliyopanuliwa. Hutumiwa kuelezea hali ambapo hadithi fulani inaweza kufasiriwa kwa namna tofauti. Wahusika au matukio yanayopatikana katika hadithi hiyo huwa na maana nyingine zaidi ya ile ya kijuujuu. Hulinganishwa na watu au matukio yaliyo nje ya ulimwengu wake (Wamitila 2003:69; 2008:510).

Kimsingi, istiara inafanya kazi ya ulinganishi lakini katika kiwango kipana zaidi. Ulinganishi huu hutokea kwa njia ya hadithi ambapo wahusika wake, matukio yake na muundo wake mzima, vinasimamia wahusika wengine na matukio mengine. Kuna mifano kadhaa katika riwaya tunayoishughulikia ya *Watu wa Gehenna* kama ifuatavyo:

#### **Kielelezo cha Sataranji (uk. 14/22)**

Sataranji ni mchezo wa ubao wenye miraba 64 unaowashirikisha wachezaji wawili. Kila mchezaji huwa ana visanamu 16 vinavyopangwa kwa namna maalum ambayo ni sawa kila upande na kila safari. Mhusika Mzee Afisul ambaye ndiye nafsi ya Eks anatumia jazanda hii kumweleza Eks fomula ya *intelligence* ya akili ya binadamu. Anaeleza kuwa jinsi ambavyo mchezo wa sataranji huchezwa ndivyo ambavyo akili ya binadamu hufanya kazi. Tofauti katika rangi ya visanamu (nyeupe na nyeusi) inadhihirisha utofauti

uliopo ulimwenguni baina ya wana-kiafra na watu wengine (wazungu). Kwamba, hii ndiyo kanuni ya ulimwengu – watu weupe hupewa nafasi ya mbele katika kila hali; ndilo tabaka tukufu. Kwa hivyo, jazanda hii inatumiwa kupeleka mbele utunzi wa riwaya, na pia, kukuza na kuendeleza ujumbe wa utabaka na unyanyasaji miongoni mwa binadamu.

Tunaambiwa kuwa, baada ya Bi. Saeeda kufanyiwa operesheni ya sikio lake, *alipata fahamu akiwa kwenye eleveta iliyoandikwa kwa rangi nyekundu tena nzito ya kutisha katika maandishi yaliyokuwa na matonematone ya damu, maandishi aina ya chillers:*

**WATU WA GEHENNA** (uk. 6). Jazanda hii inatumiwa kurejelea hatima ya mhusika Bi. Saeeda kwamba, yumo katika kupewa adhabu kali kutokana na kudhulumu wafanyakazi wa nyumbani na kushiriki biashara ya nyeti za maalbino. Hata ingawa anatafuta msaada ili aweze kujinusuru, mwisho wake ni kutumbukizwa mahali paitwapo ‘Gehenna’, penye adhabu ya milele. Kwa hivyo, ujumbe wa mtunzi unaendelezwa kupitia kwa jazanda hii pamoja na kuujenga mtindo wa riwaya kwa jumla.

Vilevile, kuna **jazanda ya vyakula** (uk. 31-35) katika riwaya hii. Wakati Eks akiwa mfu, anashiriki mazungumzo na MKUU kwa miaka saba. Katika maongezi haya, MKUU anamweleza umuhimu wa matunda na mboga ambazo Eks na mkewe waliona ni vyakula vya sungura. Anamweleza kuwa karoti ni muhimu kwa macho ya binadamu; nyanya zina elementi ya likopine ambazo ni muhimu kwa moyo na lishe ya damu; zabibu pia ni chakula cha moyo ; jozi nayo huinua hali ya mfumo wa neva katika ubongo

wa binadamu na figili husaidia kuimarisha mifupa. Kutokana na jazanda hii ya vyakula, mtunzi anapeleka mbele utunzi wa kazi yake kimtindo, na vile vile kukuza maudhui kwamba vyakula hasa mboga na matunda ni muhimu kwa afya na mwili wa binadamu. Hata MKUU anasema kuwa, kama Takosani binti Abdallah angekula vyakula hivi, angepata mtoto na asingelaumu wengine (kwa kukosa mtoto).

Katika mazungumzo kati ya Sikujua na Takosani binti Inatesh, kuna jazanda nyingi za ki-ishara ambazo zinajitokeza (uk. 41-47). Kwa mfano, kusali katika kaburi la mamake kila usiku kwa kulipigia magoti na kuweka sarafu juu yake, kuoga baharini, kupenda michezo ya kiajabu na macho yake kubadilikabadilika kila wakati hadi analazimika kuvaa miwani. Vilevile, Takosani anaagiza kulipia chumba nambari 13 (*Room Thirteen*) badala ya nambari 18; nayo maneno *Room Thirteen* yameandikwa mlangoni kwa rangi nyekundu sana kama ya damu. Isitoshe, ngozi yake (Takosani) inatawaliwa na manyoya mengi hadi mashavuni; na anapenda starehe za kwenda fukwe za Bahari ya Hindi. Pia, Takosani anajifukizia manukato makali chapa ya *poison* na, wakati mmoja anamuaga Sikujua na kuondoka kupitia ukutani. Vilevile, ana magamba mgongoni.

Mtunzi anatumia jazanda hizi na nyingine nyingi kutusawiria wasifu wa mhusika Takosani. Kwamba, hakuwa binadamu wa kawaida kutokana na maneno na matendo yake. Alikuwa mtumishi wa shetani kama anavyokiri mwenyewe (baada ya kumwua Yunasi na familia yake). Kwa hivyo, ujumbe ni kuwa, ni vizuri kuwa makini na kutahadhari katika maingiliano na watu tusiowajua. Jazanda hii imetumiwa kupeleka ujumbe wa mtunzi mbele katika *Watu wa Gehenna*.

Vilevile, kuna jazanda ya treni kupita 'ndani ya' Vokswageni ya Mwalimu Baya akiwa na Mishi (uk. 107-108). Huu ni wakati gari la Baya linakwama kwenye njia ya treni nayo treni ikawa imefika. Mishi binti Bwan Rehema anatamka neno *shemhamforash* na treni inapita 'ndani yao' bila ya kuwadhuru. Baadaye, Mwalimu Baya anatambua kwamba, miguu ya Mishi ni ya kwato za ng'ombe. Pia, kila wakati Mwalimu Baya anapotembelewa na Mishi (jini), anahisi kijibaridi kikimpuliza na kutopata usingizi pamoja na kuhisi harufu ya manukato ya Yasmin aliyokuwa amejipaka Mishi awali (uk. 112, 115). Mtunzi anatumia ishara hizi kujenga utunzi wake na kutuchorea wasifu wa mhusika Mishi. Kwamba, ni jini na wala si binadamu wa kawaida. Anakuza ujumbe wa umazingaombwe.

Katika uk. 180, kuna jazanda ya radi kuipiga dari ya nyumba ya Hikmat na kupasua kioo na sehemu ya nyuma ya nyumba yake pamoja na kuunguza paa lote. Mtunzi anatumia jazanda hii kudhihirisha jinsi ambavyo ni vigumu kulisuluhisha tatizo la rushwa. Dawa ya rushwa ni ngumu kupatikana kwa hivyo, ni muhimu kwa wanaothubutu kuipiga vita kuwa tayari kupambana na dude hili la rushwa.

Kuna jazanda ya **kulia machozi ya damu** (uk. 188). Baada ya Bi. Saeeda Khan kuhukumiwa kifo na mahakama ya Gehenna, anaanza kulia machozi ya damu; nayo mikono ya watu wa Gehenna ikawa imepambwa kwa mifupa ya watu waliokufa zamani. Mtunzi anatumia jazanda hii kukuza utunzi na ujumbe wa hatari na adhabu inayowakumba watu waovu, wa Gehenna. Damu inaashiria hatari au adhabu kali na

mifupa ya wafu kuonyesha kuwa kila muovu ataadhibiwa kulingana na matendo yake maovu aliyoyatenda akiwa duniani.

Jazanda nyingine inahusu **kimbunga kiitwacho *Hurricane Anne Heg*** (uk. 190). Lakeisha anawatelekeza watoto wake (Baingana na Siyawezi) na kuolewa na mume mwingine aliyempata katika *facebook*. Huu ndio wakati nyumba yao inapigwa na kimbunga cha *Hurricane Anne Heg* na kuiangamiza. Istiara hii inaashiria matatizo makubwa yanayowakumba akina Siyawezi hadi furaha yao ikapotea. Wanatorokwa na wazazi wao na kuingilia wizi kwa sababu ya ukosefu wa mahitaji ya kila siku na malezi mema ya wazazi.

### **3.1.3. Tashbihi au tashbiha**

Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili huliganishwa kwa njia ya moja kwa moja. Ulinganishaji huu hutambulishwa na matumizi ya viungio: 'kama', 'mfano wa', 'mithili ya', 'ja', 'kama vile', 'sawa', 'tamthili ya', 'kulingana na', 'fanana na' n.k.

Tamathali hii hutumiwa sana katika kazi za kifasihi na huwa na mchango mkubwa katika kuyawasilisha maudhui na mawazo ya mwandishi (Wamitila 2003:222). Dhamira moja ya ulinganishi huu ni kuisitiza sifa na kutujengea picha ya aina fulani akilini. Ifuatayo ni mifano ya tashbihi zilizotumiwa katika *Watu Wa Gehenna*.

*Mavazi meupe yaliyong'ara na kuwafanya waonekane kama malaika* (uk. 4). Tamathali hii inatumiwa kuwarejelea madaktari waliomfanyia upasuaji wa sikio Bi. Saeeda Khan. Walikuwa wamevalia vizuri mno na kuvutia katika mavazi yao meupe jinsi malaika wanavyofikiriwa kuwa na kuvutia. *Wanyama waliokauka kama sanamu kwa baridi hiyo*

(uk. 7). Tashbihi hii inatumiwa kurejelea hali ya viumbe ilivyokuwa ngumu katika Rusu ya nne, *Burnt For Rest*. Joto lilikuwa limetoweka na baridi ikawa kali kupindukia kiasi cha kuwakausha wanyama wakaonekana hawana uhai kamwe. Tashbihi hii inakuza ujumbe wa namna hali ilivyokuwa katika mazingira ya Gehenna ambako watu waovu wanapata adhabu yao. Inaafikiana vizuri na muktadha kuwa hakuna raha Gehenna ila kilio, huzuni na uchungu mwingi kwa watu wanaotenda maovu.

Tashbihi nyingine ni hizi: *watu hao ni kama waliokuwemo kwenye bahari ya luja* (uk. 8). *Gari lilijipanga kuelekea mahali palipoonekana kama bahari. Walipofika katikati ya sehemu hiyo iliyokuwa kama bahari, aliona gari lao ...* (uk. 60). Mtunzi analinganisha mahali ambapo gari lililomchukua Sikujua na Takosani linatua na bahari. Hii ni kutokana na uzuri wa mji walimokuwa na ghorofa za kupendeza. Hali hii ya usafiri ilikuwa imetokea katika fikra ya Sikujua. Tashbihi hii inatumiwa kukuza ujumbe wa uhalisiajabu na uteuzi wake umefaa katika kudhihirisha muktadha unaohusika.

*Mabehewa ya treni yakipita ndani yao kama waliokuwa mizuka* (uk. 107). Tashbihi hii inatumiwa kukuza ujumbe wa uhalisiajabu ambapo treni inapita ndani ya gari la Vokswageni la Mwalimu Baya kana kwamba halikuwepo. Gari pamoja na waliokuwemo (Baya na Mishi) wanalinganishwa na mizuka ambayo sifa yake kuu ni kutoonekana kwa macho halisi ya binadamu. Inakuza sifa ya uhalisiajabu.

*Matiti yake yananing'inia kama embe bolibo* (uk. 110). Tashbihi hii inalinganisha umbo la matiti ya Mishi ambaye hakuwa amevaa sidiria na umbo la embe aina ya dodo. Maana ni kuwa, matiti yake ni makubwa. Pia, (Saida) *alianza kuwaonyesha watu matiti*

*yake yaliyokuwa yamesimama tisti kama embe dodo* (uk. 139). Tashbihi hii inarejelea utovu wa maadili wa Saida katika karamu ya watu wengine na matiti yake vilevile ni makubwa. Mtunzi anakuza maumbile ya mhusika Mishi na Saida, na kutuchorea utovu wao wa maadili: hawavai sidiria ili waonekane nadhifu.

Pia tunaambiwa, *Mwalimu Baya alikaza mwendo na kukanyaga mafuta kama aliyepagawa kuelekea nyumbani* (uk. 112). Tashbihi hii inatumiwa kulinganisha mwendo wa haraka wa gari la Mwalimu Baya na wa mtu aliyepagawa. Hii ni baada ya Mwalimu Baya kubaini kuwa miguu ya Mishi ilikuwa ya kwato za ng'ombe; anaingiwa hofu na anaharakisha kwenda kwake huku akiomba Mungu amhifadhi. Vilevile tunaambiwa kuwa, *Mwalimu alihisi mwili wa binti yule umepoteza joto lote na umekuwa baridi kama barafu* (uk. 116). Mwili wa Mishi unakuwa baridi mno baada ya Mwalimu Baya kugundua kwamba, binti huyo ana magamba mgongoni. Mwandishi anatumia hali hii kuonyesha jinsi mhusika huyu hakuwa binadamu wa kawaida. Anaendeleza maudhui ya uhalisiajabu.

*Hikmat alifyatuka kwa upande wake kama risasi* (uk. 123). Tashbihi hii inalinganisha wepesi wa kukimbia wa Hikmat na risasi. Huu ni wakati wa maandamano ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kuhisika ambapo Hikmat anafyatuliwa risasi na polisi lakini anafaulu kutoroka kwa sababu ya wepesi wake.

Mfano mwingine wa tashbihi ni: *Walimu wamebaki kama mayatima au wanaofanya kazi za kujitolea* (uk. 171). Mhusika Ikmat anatumia tashbihi hii kulinganisha hali mbaya ya kikazi ya walimu nchini na ya mayatima wasio na wazazi au watu wa kuwalinda. NAT

na KUPPE ni mashirika yanayostahili kupigania haki za walimu lakini hayafanyi hivyo; kwa hivyo, walimu wanabaki wakidharauliwa na kunyanyaswa bila shirika la kuwatetea. Mtunzi anakuza ujumbe wa kutowajibika na ufisadi miongoni mwa mashirika mbalimbali nchini.

Kuna tashbihi nyingine, *mmomonyoko wa maadili unaoshika kasi kama moto wa nyika* (uk. 166-167). Tashbihi hii inatumiwa kuonyesha jinsi ambavyo maadili yamefifia upesi katika jamii na ni kama hayapo tena. Wepesi huu unalinganishwa na moto ueneapo haraka katika sehemu ya nyika. Mtunzi anakuza utunzi wake pamoja na kuendeleza maudhui ya kumomonyoka kwa maadili hasa miongoni mwa vijana.

Kuna tashbihi nyingi nyingine ambazo zimetumiwa na mtunzi katika riwaya tunayoishughulikia na ambazo hatujazifafanua kwa undani. Mifano ni hii: *walimpiga* (Baingana) *kama mbwa mwizi* (uk. 186); *Shimo lilikuwa pana kama kinywa cha chewa* (uk. 186); *Mapenzi ni kama donda yanapoingia moyoni* (uk. 173). *Parange linalowaka moto mkali uliokolea kama moto wa gesi* (uk. 185). *Kundi la Bi. Saeeda lilimfikia na kumvamia kama simba marara; na Baingana alibaki kama gagazi* (samaki wa kuchomwa). Gari la mchungaji Taabu, *likija kwa kasi ya ajabu. Ilikuwa kama radi* (uk. 199). Taabu, baada ya kumgonga mfuasi wake kwa gari lake, alimfuata upesi mno hospitalini akidhani amekufa ili wakate sehemu zake za siri wakauze.

#### **3.1.4 Kinaya/Kejeli**

Hii ni mojawapo ya tamathali za usemi ambazo hutumiwa kwa mapana katika fasihi. Kinaya hujengwa kwenye msingi wa kuwepo mgongano au ukinzani fulani kati ya hali

halisi na matarajio ya wanaohusika. Kinaya hutokea pale ambapo maneno yanayotumiwa yanaelekea kukinzana na maana inayohitajika katika muktadha maalum na inayokusudiwa na msemaji (Wales 1990: 224). Vilevile, kinaya huweza kutokea kutokana na kuwepo kwa ukinzani kati ya hali mbili. Kuna mifano ifuatayo katika *Watu wa Gehenna*.

Kupitia maelezo ya msimulizi, tunaambiwa kuwa watu wa Gehenna walifanya kazi kwa *ushirikiano, ingawa azimio lao lilikuwa kujitosheleza kibinafsi... kulikuwa na hiari ya mwenye nguvu na hiari ya mnyonge* (uk. 9). Ni wazi kwamba hakuna umoja wa aina yoyote miongoni mwa watu wa Gehenna. Mtunzi anakuza ujumbe wa hali ilivyokuwa katika mandhari ya Gehenna - ubinafsi na watu kuwa hatari.

Pia, ujumbe katika wimbo *Walijuta* ulioimbwa na watu wa Gehenna ni kinaya (uk. 8-9). Katika wimbo huu, Gehenna inasemekana kuwa mahali patakatifu. Hiki ni kinyume cha ukweli kwa kuwa hata watu waliokuwa Gehenna wanajuta mambo mengi mabaya ambayo wametenda hasa kwa sababu mandhari ya Gehenna ni moto mkali unaowachoma na kuwateketeza waovu mfululizo.

Tunaambiwa kuwa, *Eks na mkewe waliani kuwa maboga na matunda ni chakula cha sungura; walivichukia* (uk. 19). Hiki ni kinaya kwa sababu kwa kawaida mboga na matunda ni vyakula bora kwa binadamu na huongeza virutubishi mwilini kama anavyowaeleza mhusika MKUU (uk. 32-35). Mtunzi anaendeleza ujumbe kuwa, ingawa nyama ni nzuri, matunda na maboga pia ni vyakula bora kwa mwili wa binadamu.

Katika muktadha huu wa vyakula, tunapata kinaya cha kidhihaka au kejeli. Mkewe Eks anaamini kuwa:

Mapenzi yangenoga nyumbani pale alipomlisha  
mumewe kwa vyakula vilivyokaangwa kwa mafuta  
nyingi. Alikuwa na imani sugu kuwa mumewe sharti  
awe na kitambi kama dhihirisho la lishe bora (uk. 19).

Hiki ni kinaya kwa sababu kula chakula chenye mafuta mengi hakunogeshi mapenzi. Ukweli ni kwamba 'kula' mafuta mengi kwenye chakula husababisha unene na kitambi ambavyo kamwe si dhihirisho la lishe bora; ni udhaifu wa kiafya. Dhihirisho riwayani ni kuwa, Eks anashindwa kutekeleza mengi mazuri kukiwemo kitendo cha ndoa kutokana na unene wake. Isitoshe, usiku anakuwa na matatizo ya kupumua. Kwa hivyo, ujumbe ni kwamba, ni vyema binadamu kula vyakula vyenye lishe bora.

Kuna kinaya pale ambapo Sikujua anakutana na Takosani binti Inatesh na kumpenda mara ya kwanza; na anaomba awe mke wake. Kinaya kinajitokeza pale Takosani analia kwa uchungu akimwomba Sikujua asimuo maana asingeweza kutii masharti yake (uk. 42). Ni kinyume kwa sababu, muda mfupi tu baadaye, Takosani 'anampenda' na kukubali ombi lake. Pia, Takosani anakataa kumpa Sikujua utajiri kwa kudai (Sikujua) atamsahau Mungu. Hiki ni kinaya kikubwa kwa sababu Takosani mwenyewe anakiri ni binti ya shetani, na mpinzani wa Masihi Yesu Kristo tangu akiwa mdogo.

Hatimaye kuna kinaya cha kiucheshi pale ambapo wapambe wa Takosani wanamkaribisha Sikujua kwa mbwembwe, lakini mara wanamkumbusha makosa

aliyoyafanya akiwa duniani na wanamwadhibu bila huruma (uk. 60). Kinaya cha kiucheshi kinajitokeza pia pale Mwalimu Baya (baada ya kustarehe na Mishi), anajikuta juu ya mti wa mbuyu sokoni Chamada huku nguo zake zikiwa zinaning'inia kwenye matawi yake (uk. 117). Ni kinaya katika hali ya kuwa, mwalimu mzima mwenye heshima zake, anakumbwa katika hali kama ile ya kuaibisha mbele ya watu.

Mfano zaidi wa kinaya ni katika wimbo unaoimbwa na Ujana akiwa na marafikize (Kinaya na Saida) wakiwa katika *Student Centre*. Ujana anasema kwamba, anahitaji pesa, mwanamume, vinywaji, muziki na Gehenna! (uk. 138). Hiki ni kinyume kwa kuwa Ujana ameenda kusoma katika Chuo Kikuu cha Kuhisika bali sio kutafuta starehe hizo.

Mtunzi anamtumia mhusika Kinaya kudhihirisha ukinzani fulani (uk. 135-138). Kinaya alikuwa 'rafiki' mkubwa wa Saida wakati wakiwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kuhisika. Walishiriki kila starehe pamoja na kumchukia Siyawezi, msichana aliyekuwa mwadilifu. Hata hivyo, kinaya kinajitokeza bayana wakati Saida anapougua baada ya *stag party* na kulazwa hospitalini. Kinaya anamtoroka na kukataa kumpelekea nakala za mihadhara. Siyawezi ndiye anayemtembelea Saida hospitalini na kumjulia hali (uk. 141-143).

Mtunzi vilevile anatumia mbinu ya kinaya katika kuusawiri uhusiano 'wa karibu' baina ya Bi. Saeeda Khan na mtoto Baingana (uk. 182). Bi. Saeeda anajifanya anampenda mtoto Baingana na kumpa 'tam tam' ilhali ukweli ni kuwa, anadhamiria kumwua na kuuza sehemu zake za mwili (kwa kuwa ni albino) ili apate faida.

Mbinu ya kinaya inabainika wazi pia, kupitia mhusika Bi. Saeeda Khan. Anapofikishwa mbele ya mahakama ya Gehenna, na kuhojiwa na jaji, Bi. Saeeda anajitetea kuwa yeye ni raia mwema, mwanamke mwema na tena mwanafamilia mzuri na mchapakazi. Anasema jinsi alivyojitahidi kufanya yote sawa na mapenzi ya Mungu (uk. 187). Hiki ni kinaya kwa kuwa Bi. Saeeda si mtu mwema; anashiriki biashara ya kuwaua mazeruzeru na kuuza sehemu zao za mwili. Pia, anawadhulumu wafanyakazi wa nyumbani kama Bi. Mwanahamisi Mruke.

Kinaya cha kitashtiti kinajitokeza katika tabia ya Lakeisha anapowatoroka watoto wake (Baingana na Siyawezi) na kumwachia baba yao wa kambo, Eks Ngwenyama (uk. 192-193). Sababu kuu ni kwamba, anaolewa na mume ‘tajiri’ anayempata kwenye mtandao wa *facebook*. Tunatarajia mama mzazi awalee na kuwahifadhi watoto wake kadri awezavyo. Lakini hapa, Lakeisha anatenda kinyume cha matarajio haya. Mtunzi anatumia kinaya hiki kukuza ujumbe wa malezi ili kuwatanabahisha wazazi kuwa wawe tayari kuwatunza watoto wao. Anaonyesha uozo wa kijamii. Mbinu ya kinaya pia inachangia pakubwa utunzi wa mwandishi huyu.

### **3.1.5 Taswira**

Ni matumizi ya lugha kwa namna inayojenga picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji. Picha hizi hujengwa akilini mwa msomaji kwa maelezo fulani na huweza pia kujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashbihi na sitiari. Lengo la kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo

fulani. Mwandishi Tom Olali ametumia taswira kadhaa katika riwaya yake ya *Watu wa Gehenna*. Ifuatayo ni mifano michache.

Katika sura ya kwanza, mwandishi anatumia taswira ya mandhari ya Gehenna. Gehenna ni mahali pa matanuu manne yenye moto mkali. Ina volkano nne juu ya milima minne inayogawanywa na bonde katikati. Haina mahali tambarare na kuna giza totoro. Milima hii minne ndiyo inayojenga rusu nne ambazo ni za ufisadi (*korappzion*), ukabila (*traibbolizim*), dhuluma kwa watoto (*chhaldabius*) na mahame ya *Burnt For Rest*. Taswira hii inatuhirishia jinsi mahali pa adhabu kwa watenda maovu duniani yalivyo. Kwa kila aina ya dhuluma inayotendwa, kuna adhabu kali itakayoandama nayo.

Mtunzi pia anatumia taswira ya mahali ambapo Baadayadhiki, Sikujua na Takosani binti Inatesh wanafanyia mazungumzo yao katika ufuo wa Vumawimbi. Anasema hivi:

Waliondoka.....Tondooni na wakafululiza wakipitia  
uwanjani hadi Mkia wa Ng'ombe ambapo pana jengo  
la kale la msikiti, makaburi kumi na matatu, na idadi  
kadha ya nyumba za karne nyingi zilizopita. (uk. 67)

Taswira hii inatubainishia zaidi wasifu wa wahusika hawa, hasa Takosani. Desturi yake ya kupenda mandhari ya makaburi na mahame inaashiria kuwa yeye si binadamu halisi, ni jini au binti ya shetani kama anavyosema mwenyewe baadaye.

Vilevile, tunapata taswira ya maumbile ya Mishi kupitia maelezo ya msimulizi. Anatueleza kwamba:

Alikuwa shombe licha ya ngozi yake kuonyesha kuchanganya damu; nywele zake zilikuwa za Kiarabu. Mashavu yake yalikuwa yameumuka sawia, huku macho yakiwa yamefunikwa kwa wanja. Midomo yake iliiva kwa rangi nyekundu ya mdomoni. (uk. 103)

Maelezo haya yanajenga sura ya Mishi hasa baada ya kutumia vipodozi. Hatimaye, mtunzi anatuchorea maumbile halisi ya Mishi baada ya Mwalimu Baya kugundua kuwa (Mishi) ni jini. Anatuambia hivi:

Chumba kizima kilijazwa na mwanga uliotoka ndani ya mwili wa binti huyo... Mishi alikuwa na jicho moja kwenye paji la uso wake huku mwili wake ukiwa nusu toka juu hadi chini. Titi moja, mkono mmoja, mguu mmoja, nusu ya kila kitu. (uk. 117)

Maelezo haya yanatudhihirishia usawiri wa mhusika Mishi, yeye ni jini au zimwi: hata tunaelezwa kuwa miguu yake ilikuwa ya kwato za ng'ombe (uk. 110). Katika kutamatisha uhusiano baina ya Mwalimu Baya na Mishi, mtunzi anatuchorea taswira ya yanayomkumba Mwalimu hatimaye. Kwamba, kesho yake asubuhi, anajikuta juu ya mti wa mbuyu huku nguo zake zikiwa zinaning'inia kwenye matawi yake (uk. 117). Hapa, tunapata picha halisi ya yanayompata Mwalimu Baya baada ya kukumbana na Mishi, jini.

Kuna pia taswira ya treni kupita ‘ndani ya’ gari la Vokswageni la Mwalimu Baya bila ya kuwadhuru waliokuwemo (Mishi na Baya) (uk. 107). Taswira hii inatufichulia zaidi sifa za mhusika Mishi, ni mke wa Shemhamforash.

### **3.1.6 Tashihisi/Uhaishaji**

Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa na uhai ama vyenye sifa za kidhahania vinapewa sifa za binadamu. Katika hali hii, kitu kisicho binadamu, iwe ni mnyama au mdudu hupewa sifa ya binadamu. Hii ni kwa kuwa maana ya tashihisi ni kunafsisha au kufanya kitu kuwa na maumbile au mahasa kama vile nafsi ya mtu. (Kuhenga 1977:15).

Tamathali hii inatumiwa na mwandishi Olali katika riwaya yake ili kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani ya kihisia pamoja na kusisitiza jambo fulani. Kwa mfano: mifupa ya miguu ya Eks inapewa sifa ya kinafsi. Mwandishi anasema, *mifupa ya miguu yake ilifanya hima kuubeba mwili wa Eks.... Ilishindwa* (uk. 17). Katika mfano huu, mifupa inapewa sifa ya kuharakisha na hatimaye kushindwa. Lengo la mtunzi ni kusisitiza udhaifu wa kiafya ambao unamkumba Eks kutokana na athari za kikazi katika kampuni ya *The World Cementers Inc.*

Katika mahojiano ya Mzee Afisul na Eks, tunapata nafsi ya Eks ikipewa sifa ya kibinadamu ya kuhojiwa. Mahojiano yanaenda hivi:

*“Je, nafsi yako hukupa majibu?”*

*“Ndiyo!”*

*“Imekupa majibu ya yale yanayokusumbua?”*

*“Amenipa!”*

*“Imekupa ama amekupa?”*

*“Amenipa!”*

*“Nafsi yako iko hai?”*

*“Iko hai. Ni mimi!” (uk. 21).*

Vilevile, Mzee Afisul ni mhusika asiyeonekana. Eks anasikia tu sauti yake. Yeye ni kama upepo; ni mhusika wa kinjozi au wa kidhahania. Kutokana na hali hii, Mzee Afisul kama mhusika amehuishwa –amepewa sifa ya kumhoji Eks kuhusu binadamu ni nani (uk. 20). Eks anamwuliza Mzee Afisul, “Mbona kete nyeusi isianze na kufuatwa na kete nyeupe?” Hapa kete au kisanamu kimepewa sifa ya kuanza mchezo wa sataranji (uk. 29).

### **3.1.7 Maswali ya balagha**

Hii ni tamathali ya kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu. Maswali hayo hayahitaji majibu kwa sababu majibu yake yako wazi kwa msikilizaji au msomaji. Huwa ni mbinu nzuri ya kumfikirisha msomaji, kumshawishi kuhusu jambo au hali fulani; na pia kusisitiza usemi. Mifano ifuatayo imo katika *Watu wa Gehenna*.

*Multinational kama ile angeweza kukabiliana nayo? (uk. 16).* Mwandishi anatumia tamathali hii kusisitiza hali ambayo inamkumba Eks baada ya kuwacha kazi katika *The World Cementers Inc* kutokana na athari za kiafya. Hakupewa fidia yoyote na malipo ya uzeeni yalikuwa kidogo mno. Kwa hivyo, kampuni hiyo ya kimataifa ni ‘kubwa’ mno -

kiasi ya kwamba, Eks angeifuatilia, asingefaulu kulipwa hela zaidi. Swali hili la kibalagha linaonyesha jinsi ambavyo wafanyakazi hasa wa Kiafra wanavyonyanyaswa na mashirika ya kimataifa.

Maswali ya balagha yanatumiwa pia na Saida, ambaye, baada ya kuugua na kulazwa hospitalini, anatorokwa na marafiki zake, akiwemo Kinaya. Tukio hili linamfanya Saida atafakari upya uhusiano wake na hao marafiki zake. Kwa mfano anajiuliza, *“Je, kuna faida gani ya urafiki ikiwa hauzai matunda wakati wa shida? Je, rafiki si ni yule akufaaye wakati wa dhiki?”* (uk. 141). Mbinu hii pia imejitokeza kama uzungumzinafsi. Maswali haya yanatumiwa kutanabahisha wasomaji kuwa waangalifu katika kuchagua marafiki kwa sababu baadhi huwa wanafiki.

Baada ya kuwahutubia watu Ndotoni akiomba kiti cha ubunge, Hikmat anapozinduka kutoka mawazoni/ndotoni, hakujielewa kama kweli ulikuwa ukweli au ndoto/luja. Anasema, *“Nafsi yake ilikuwa inamchezea shere? Au labda alikuwa katika hali halisi?”* (uk. 161). Mtunzi anatumia hali hii ya Hikmat kutuchorea mandhari ya kinjozi katika kazi yake ya *Watu wa Gehenna*.

Vilevile, mtunzi anatumia tamathali hii kuwatanabahisha watu kuhusu tabia isiyopendeza ya viongozi katika Kiafra ambao huunda vyama vya kisiasa ili kujinufaisha binafsi na bali si kuwanufaisha wananchi. Msimulizi anasema, *“Ndiyo, ya nini tupoteze muda kujitakia mazuri wenyewe na kuwakaangia sumu wengine?”* (uk. 163) anapowarejelea viongozi wa Kiafra (hasa wanasiasa).

*“Wakulima... watanufaika vipi iwapo hawawezeshwi na wale tuliowaweka madarakani ili wawatumikie? Kwa nini... tunaambiwa kilo ya pamba itanunuliwa kwa shilingi 66, lakini kesho inakuwa shilingi 666 au pungufu?”* (uk. 164). Mtunzi anatumia maswali haya katika mjadala kufirikisha wasomaji kuhusu hali ya viongozi waliochaguliwa kukosa kuwajibika na pia ufisadi ulivyoenea miongoni mwao. Anawazindua wafanye mabadiliko ya uongozi.

Mfano mwingine wa tamathali hii ni: *“Si heri zama zile za watawala weupe?”* (uk. 165). Uongozi mbaya na kudhulumwa kwa wananchi kunafanywa na viongozi wa Kiafra. Dhuluma zimekuwa nyingi kiasi ya kwamba wakiafra wanaona ingekuwa afadhali kuwa chini ya watu weupe kuliko chini ya waafrika. Wazungu walijali angaa kuwatafutia wakulima soko la mazao yao.

Mfano mwingine ni pale wanajopo wanapojadiliana kuhusu kumomonyoka kwa maadili, wanasuta vituo vingi vya matangazo kwa kupotosha wananchi. Wanasema, *“Nenda vijiwani, sikiliza redio za siku hizi, zile za FM Stations, majarida na magazeti aina aina, lugha inayotumika inajenga?”* (uk. 169).

### **3.1.8 Takriri/urudiaji**

Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa (Msokile 1992:61). Lengo kuu la mwandishi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kutilia mkazo jambo linaloelezwa. Kwa mfano:

Nafsi ya Eks inapomhoji Eks kuhusu *“binadamu ni nani”*, Eks anamjibu, *“Binadamu ni mimi. Mimi ni binadamu”* (uk. 11). Urudiaji huu unaleta msisitizo kuonyesha kuwa yeye Eks ni tofauti na viumbe wengine kama ndege na wanyama.

Daktari anaposisitiza hatari inayoweza kutokea iwapo watakosea katika upasuaji wa sikio la kulia la Bi. Saeeda Khan, anasema hivi: *“Kosa lolote dogo, dogo tu, linaweza kuleta matatizo makubwa. Matatizo makubwa kuliko ukabila!”* (uk. 5).

Vilevile, msimulizi, katika kusesitiza urefu wa mito Volldennberg na A.L. kwenye Rusu ya *Korappzion*, anatumia urudiaji wa maneno. Anasema, *“Mito hiyo ilipinda...na kuanguka bwaaaa... chini, chini, chini, chini yapata maelfu ya futi”* (uk. 6). Kuna takriri ya neno ‘chini’.

Tunaambiwa, Eks na mkewe walipenda kula nyama huku wakichukia maboga na matunda. Msimulizi anasisitiza hali hii kwa kurudia neno ‘nyama’. Anasema hivi: *“Walipenda sana kula nyama - nyama iliyochomwa hasa. Ilikuwa ni nadra kwao wasile nyama na dukani kwa muuzaji nyama, walikuwa na daftari la deni – deni la nyama. Mbali na ile nyama ya kuchomwa.”* (uk. 19).

Msimulizi anapotusisitiza kuhusu mchezo unaofanyika katika akili ya Sikujua, anasema: *“Mchezo wenye wahusika watatu... Mchezo wa ukweli. Na mchezo wa ukweli ni mchezo wa ukweli. Mchezo ulianza...”* (uk.62). Kifungu ‘mchezo wa ukweli’ kinarudiwarudiwa.

Saida anapomkataza Siyawezi asiendeleo kumweleza kuhusu dini na sheria zake, anamwambia, *“Inatosha, inatosha, haya yanatosha”* (uk. 130). Hii ni kuonyesha ametosheka na kuchoshwa na nasaha za Siyawezi hataki kuambiwa zaidi.

Katika hotuba ya Hikmat kwa halaiki kubwa ya watu akiomba kura za kiti cha ubunge Ndotoni, kuna takriri ya maneno na vifungu ambavyo vinajitokeza. K.m umati ulimhimiza kuendelea kuhutubu kwa kusema, *“Tora Hikmat! Tora Hikmat! Tora Hikmat!”* (uk. 159). *“Toboa Hikmat! Toboa!”* (uk. 160). Kila anapotaja ujumbe kuhusu viongozi waovu, hadhira inakariri, *“Waende Gehenna! Watu wa Gehenna hao!”* (uk. 156-157). Nalo dua la mzee mmoja pia lilirudiwa katika hotuba nzima (uk. 155/157).

Katika *Watu wa Gehenna*, kuna matumizi ya anafora katika wimbo ‘Wanajuta’ (uk. 8-9). Neno moja limetumiwa kutangulia mistari karibu yote ya wimbo huu. Neno hili ni ‘wanajuta’. Mbali na kujenga utunzi wa riwaya hii, takriri hii imetumiwa kukuza ujumbe wa majuto ya watu waliotenda maovu na kuingizwa Gehenna ambapo sasa wanaadhibiwa vikali.

Vilevile katika wimbo unaoimbwa na Ujana katika Kiingereza kuna matumizi ya anafora ili kusisitiza tabia yake ya uhitaji. Maneno, *“Oh, I need some ..... ”* yanarudiwa katika mistari yote ya wimbo ila katika mstari wa mwisho (uk. 138).

Katika kazi hii pia, kuna takriri ya maana ambayo inajitokeza. Kwa mfano, *“Eneo hili lilikuwa mahali pa maumivu, mateso na majuto mengi... ni kueneza chuki na uhasama miongoni mwa makabila mbalimbali”* (uk. 7). Haya ni matumizi ya maneno yenye maana sawa (visawe) na yanaonyesha jinsi hali ilivyokuwa ya kilio Gehenna.

Watu wanaomfukuza Baingana ili wamuue wanatumia *“kila aina ya silaha kama rungu, jiwe, shoka, sululu, mundu na kila silaha uifahamuyo”* (uk. 186). Hapa kuna takriri ya

maana kwa kuwa maneno haya yote yanarejelea silaha. Mtunzi amefanya hivi kusisitiza jinsi watu walivyo wabaya na wanavyompiga mtoto zeruzeru.

### **3.2 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeshughulikia matumizi ya lugha katika kiwango cha kisemantiki. Tumeangazia tamathali mbalimbali za usemi zikiwemo sitiari, jazanda, tashbihi, kinaya/kejeli, taswira, tashihisi, maswali ya balagha na takriri. Mtunzi amezitumia tamathali hizi ili kutoa mvuto wa kisanaa na kupitisha ujumbe wake kwa njia teule inayoeleweka. Tamathali hizi zina majukumu kadha: zimetumiwa kufafanua maana, kuibua hisia, kuhuisha na kurembesha huku jukumu kuu likiwa ni kuongeza ujumi katika *Watu wa Gehenna*.

Mtunzi amefaulu pakubwa kutumia tamathali hizi za usemi na zimefanikisha uwasilishaji wa maudhui kwa msomaji pamoja na kukuza na kuendeleza dhamira zake mbalimbali.

## **SURA YA NNE: MANDHARI NA USIMULIZI KATIKA WATU WA GEHENNA**

### **4.0 UTANGULIZI**

Sura hii inashughulikia vipengele viwili vya kifani ambavyo ni mandhari na usimulizi. Tumetanguliza kwa mandhari na baadaye tukaangazia dhana ya usimulizi.

### **4.1 DHANA YA MANDHARI**

Matendo yoyote ambayo hutokea katika kazi za kifasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalum. Hiki ndicho kinachoelezwa kama mandhari. Kwa hivyo, mandhari ni elementi ambayo hufichua ni wapi na lini ambapo matukio fulani yanafanyika.

Wamitila (2003:108) anaifafanua dhana hii kwa kusema:

Dhana hii hurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia, yaani mazingira ya utendaji wake au usimulizi wake. Katika maana pana, dhana hii huelezea mazingira ya kijamii na kielimu wanamojikuta wahusika wa kifasihi.

Katika maelezo haya, Wamitila anaeleza upana wa dhana ya mandhari. Anasema kwamba, mandhari si mazingira tu bali hurejelea masuala mengi yakiwemo itikadi, mila, desturi, jamii na elimu. Hivyo, ina maana kuwa, mandhari yanaweza kuhamishwa katika mazingira tofauti kulingana na muktadha (Wamitila 2002: 27).

Mandhari huchangia katika kueleza mambo mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali yao na huweza kuwa mihimili mikuu ya kuyaendeleza maudhui ya kazi ya kifasihi.

Matendo ya wahusika yanachochea na mandhari na mazingira yao. Mazingira anamojikuta mhusika yanaathiri kwa kiasi kikubwa wasifu wake kama mhusika. Mara nyingi, wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika, lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia.

Mandhari huwa na elementi zinazoyatambulisha. Elementi hizi ni eneo halisi la kijiografia kama nyumbani, gerezani, pangoni na msituni; au wakati ambapo tukio fulani linatendeka au kipindi maalumu cha kihistoria au kipindi cha mwaka (mfano msimu wa mvua au kiangazi) (Wamitila 2002: 29).

Njogu na Chimera (1999:46) wanasema:

Mandhari ni mahali au makazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi, na mnamotukia matukio mbalimbali ya kifasihi. Mandhari ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio, na inahusu mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana; mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao; na nafasi zao za kitabaka.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa wawili, mandhari ni kama kipengele cha kudhibiti wahusika na ni muhimu katika kuchanganua kazi za kifasihi. Kwa maoni yao, mandhari ina dhima au majukumu mbalimbali katika kazi za kifasihi; na ambayo hutofautiana kulingana na malengo ya msanii anayehusika. Wanasema kuwa, kufahamu mandhari kunawasaidia wasomaji kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika. Pili, mandhari inatupa mwelekeo kuhusu maudhui.

Kuna aina nyingi za mandhari zinazopatikana katika kazi za kifasihi. Hata hivyo, tumeshughulikia aina mbili tu za mandhari ambazo zinapatikana katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*.

## **4.2 AINA ZA MANDHARI KATIKA WATU WA GEHENNA**

### **4.2.0 Utangulizi**

Katika *Watu wa Gehenna*, kuna upanuaji wa mwanda wa kisimulizi; ambapo tunapata mandhari ya kinelibini. Riwaya mpya kama ilivyo *Watu wa Gehenna* haina mipaka wazi ya mianda ya kisimulizi: huweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu dhanifu au wa njozi, na maingiliano kati ya aina hizo tofauti huvunjwa. Vilevile, hali hii huweza kutokea pale hali ya usimulizi inaachwa na riwaya au mhusika na kujitosa kwenye tathmini ya kisaikolojia (hasa kupitia ndoto).

### **4.2.1 Mandhari ya kijiografia/ halisi**

Mazingira ni nguzo muhimu katika mandhari na huwa ni msingi wa kanuni ya ushabihikweli katika kazi za kifasihi. Msingi mkuu wa kanuni hii ni matumizi ya maeneo ya kijiografia ambapo mwandishi huelezea mazingira halisi kiasi kwamba, anayeisoma kazi hiyo na anayafahamu mazingira hayo yanayoelezwa, anaweza hata kuona maeneo 'wanakopita' wahusika wenyewe. Hata hivyo, huwa ni mahali palipobunilizwa na pana wahusika wa kibunifu (Wamitila 2008:348, 352). Lengo huwa ni kumfanya msomaji aweze kuamini kuwa matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanayotokea katika ulimwengu huo wa kibunifu yanaweza kukubalika. Kuna mifano ifuatayo ya mandhari hii katika *Watu wa Gehenna*.

Katika riwaya tunayoishughulikia, mtunzi anarejelea mandhari halisi ya miji na sehemu mbalimbali za pwani ya Kenya. K.m katika mazungumzo baina ya Siyawezi na Akilimali Van Krockoff, Siyawezi anamweleza kuhusu sayansi ya ndumba katika visiwa vya Pate; na jinsi wanasiasa wanavyotumia popobawa kuwadhulumu wapinzani wao (uk. 56-57). Wanazungumzia mambo mengi kuhusu imani za watu wa visiwani katika ushirikina na nguvu za giza na hasa wanasiasa.

Vilevile, mwandishi anarejelea bandari ya Wete ambayo hutumiwa kusafirishia miili ya maalbino kwenye merikebu za kuelekea Tanga. Katika muktadha huu, mazingira halisi yanatajwa kwa wingi kama vile mahame ya Mkama Ndume yaliyoko Ras Mkumbuu; Pemba, Mkoani, Weshi, Kiweni na Machumani (uk. 63-65). Mandhari haya yanatumia na mwandishi ili kuonyesha kuwa biashara ya miili na nyeti za mazeruzeru ni ukweli; ipo na inaendelezwa na viongozi na watu wengine ambao hutumia sehemu za visiwani kuhifadhi na kusafirishia 'malighafi' hiyo hadi 'sokoni'.

Mandhari ya kijiografia pia yanajitokeza katika mazungumzo baina ya Faki Nahodha na Baadayadhiki; kwamba, makazi yao ya awali ni mji wa kale/ Mombasa na Pemba mtawalia (uk. 68-70). Wanazungumza kuhusu mambo yanayojiri katika miji hiyo, pamoja na kuzitaja barabara nyingi za mkoani Chake Chake (uk. 70). Faki anarejelea kisa cha mwanasiasa, Waziri wa Afya aliyeshiriki biashara ya kuwaua wagonjwa na kuwafyonza damu, na kuendeleza biashara ya nyeti za maalbino visiwani.

Mwandishi pia anarejelea mandhari halisi anapotueleza kuhusu safari ya Mwalimu Baya. Anasema, Baya aliondoka eneo la Mkunazini, akapitia barabara za Pangani na

Morogoro anapokutana na Mishi njiani akielekea Chumbageni. Mwalimu Baya alikuwa amehamia Al Jazeera al Khadra (Pemba) kutoka nyumbani kwake Lamu.

Mazingira haya ya uhalisia yanatumiwa ili kufanya matukio yanayofanyika baadaye kuweza kukubalika kama ya kawaida katika jamii za maeneo ya pwani. Kwa mfano ukarimu wa mhusika Baya unamwingiza katika balaa ya kulaaniwa na binti aliyekuwa mke wa Shemhamforash (uk. 117).

#### **4.2.2 Mandhari ya kidhanifu/kinjozi.**

Haya ni mandhari ambayo hayawezi kuhusishwa na uhalisi. Aghalabu hupatikana katika kazi ambazo zina misingi yake katika 'njozi' fulani. Mandhari haya ndimo riwaya ya *Watu wa Gehenna* imetungiwa. Riwaya hii ina wahusika wawili tu na hadithi nzima inafanyika katika akili au mawazo ya mhusika mmoja, Eks. Katika hali hii, tunapata hadithi ikisimuliwa katika mandhari ya kinelibini, yaani, wahusika wanatoka katika ulimwengu halisi hadi ulimwengu wa kinjozi na kurejea tena katika ulimwengu wa uhalisia. Mwandishi anavunja mipaka ya kimwanda ili kuelezea mazingira tofauti yanayowakumba wahusika. Ufuatao ni ufafanuzi wa mandhari hayo katika riwaya tunayoishughulikia.

Mwanzoni mwa riwaya hii, mwandishi anatueleza mandhari ya Gehenna yanayowajumuisha wakazi wa Gehenna. Gehenna ina matanuu manne yenye moto mkali na ina volkano nne juu ya milima minne inayogawanywa na bonde katikati. Milima hii inajenga rusu nne ambamo watenda dhambi mbalimbali huadhibiwa.

Mandhari hayo ni ya kinjozi kwa kuwa yamo akilini mwa Eks. Hata Mzee Afisul anamwambia Eks hivi:

Nafsi yako inakuchezea shere tu. Gehenna imo akilini  
mwa binadamu. Akilini mwa X. Akilini mwako. Ni  
uginingi. (uk. 26)

Ni bayana kuwa mazingira haya yanakuza na kuendeleza ujumbe wa kuwaonya binadamu kwamba, kwa kila aina ya maovu wayatendayo wakiwa ulimwenguni, kuna adhabu kali ya moto inayowasubiri.

Mandhari ya kinjozi pia yanajitokeza wakati Eks anapohojiwa na wahusika wa kiungu, Mzee Afisul na MKUU. Mzee Afisul ambaye hana umbo la kibinadamu anamhoji Eks akiwa mawazoni kuhusu 'binadamu ni nani' na anatumia kielelezo cha sataranji kumfafanulia kuhusu *superior intelligence* (uk. 20). Vilevile, akilini mwa Eks, nafsi yake Eks inamwamuru kufa ambapo anakufa na kufufuka baada ya miaka saba. Tunaambiwa:

“Nakuamuru ufe!” Nafsi ya Eks alimshurutisha. Eks  
alikuwa mara moja.

“Fufuka!” Eks alifufuka.

Baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kulichukua miaka  
saba. (uk. 30)

Hatimaye MKUU anamhoji Eks kwa miaka hiyo saba. Anamwonya dhidi ya kupotoshwa na Mzee Afisul; anamweleza umuhimu wa kula mboga na matunda na kumpa amri saba

za kumfariji baada ya kifo cha mkewe, Takosani binti Abdalla. Mwandishi Olali anatumia mandhari haya ya kinjozi ili kujenga mtindo wa kuyawezesha matukio yasiyo ya kawaida kutukia (kama vile kufa na kufufuka) na kuweza kukubalika. Pia anakuza na kuendeleza ujumbe wa uhalisiajabu katika kazi yake na hata kuwasawiri wahusika wa kinjozi au wa kimazingaombwe.

Mahusiano ya Sikujua na Takosani binti Inatesh yanasawiriwa katika mandhari ya kinjozi: yanatendeka katika akili ya Sikujua. Kwa mfano, baada ya kufanya starehe na Sikujua, Takosani anaondoka kupitia ukutani na pia, Sikujua anapofumba macho, wanajikuta wameketi sehemu yenye mapango (uk. 48-49). Hatimaye wote wawili 'wanaabiri gari' na kufika baharini ambapo gari linazama na Sikujua anapoteza fahamu. Sikujua anapozinduka, wanajikuta katika mji wenye ghorofa za kupendeza (uk. 60). Huko, Sikujua anaadhibiwa kwa makosa aliyoyatenda akiwa mbunge ulimwenguni. Mtunzi amekuza mtindo wake katika kuwasawiri wahusika wa kinjozi hasa Takosani na anakuza ujumbe wa adhabu watakazopata watenda maovu.

Mlipuko wa jengo la *Gehenna Systems Centre* (GSC) unatokea katika mandhari ya kinjozi. Mhubiri Yunasi anafanya kazi katika ghorofa ya 666 ya jengo la GSC na mkewe, Saida katika ghorofa ya 999. Yunasi anashuhudia mlipuko huo mkubwa: *Gehenna Airlines Flight 666* kutoka Ziwa Sadiki inalipiga jengo la GSC inapokuwa inaelekea Fikirini. Ghorofa zote 999 za jengo hilo zinadondoka chini na watu zaidi ya elfu ishirini wanaangamia, lakini Yunasi ananusurika kimiujiza kwa kuongozwa na mtu aliyevalia koti lenye maandishi 'MKOMBOZI' hadi mahali salama. Mkewe pia ananusurika kwa sababu

anachelewa kufika kazini siku hiyo. Hatimaye Yunasi anafurahi anapoamka na kugundua kuwa lilikuwa ni jinamizi (uk. 148-154).

Mwandishi anatumia mandhari haya kuonyesha ubunifu wake mkubwa katika utunzi. Mandhari haya yanamwezesha kueleza matukio ambayo hayawezi kutendeka kwa urahisi katika mazingira halisi au ya kawaida. Kwa mfano, jengo lenye ghorofa 999 ni nadra kupatikana ulimwenguni; na ajabu zaidi ni kwamba, jengo hilo linapolipuliwa, ghorofa zote zinadondoka chini. Kwa hivyo, mwandishi anakuza ujumbe wa uhalisiajabu pamoja na kuonyesha umuhimu wa kumkubali Bwana Yesu Kristo mapema katika maisha ya binadamu.

Mfano mwingine wa mandhari ya kinjozi ni pale Hikmat anapowahutubia wananchi wa Ndotoni akiomba kura za ubunge. Mkutano huu wa hadhara unafanyika katika akili ya Hikmat. Akiwa ndotoni, Hikmat anawahutubia wananchi akiwazindua dhidi ya kudhulumiwa na kunyanyaswa na viongozi walio mamlakani pamoja na kuwafafanulia manifesto ya Chama cha Mwananchi. Halaiki ya watu inamshangilia na kumwombea dua (uk. 155-160). Hikmat anapozindukana, anashindwa kuelewa iwapo ilikuwa ndoto au ukweli. Mwandishi anatumia mandhari haya kukuza ujumbe wa kuwazindua wananchi dhidi ya viongozi wabaya na hasa mafisadi, matatizo na dhuluma zinazowakumba, na hatimaye kubainisha sifa za uongozi mzuri unaoweza kuleta maendeleo katika nchi. Vilevile, mtunzi ameweza kumsawiri na kumkuza mhusika Hikmat kama mwanamapinduzi.

Kipindi cha *The Night of the Living Dead* pia kinafanyika katika mandhari ya kidhanifu. Runinga ambayo Hikmat anaitazama imo akilini mwake, kwa hivyo kipindi hiki kinatendeka akilini mwake. Katika kipindi hiki, wanajopo Kmat, Ikmat na Mat ni wahusika wa kinjozi: wote ni nakili za nafsi za Hikmat ambaye pia anachangia katika mjadala. Mjadala unahusu mataifa ya Kiafra na hususan utekelezaji wa maazimio ya *Mirage 0000*. Wanajopo wanajadiliana kuhusu uongozi mbaya Kiafra na kufifia kwa maadili (uk. 162-179). Mwandishi anatumia mandhari hayo kukuza na kuendeleza ujumbe wa uongozi mbaya katika mataifa ya Kiafra.

Mwandishi vilevile anatuchorea mandhari ya kinjozi kupitia mhusika Lakeisha na mwanawe, Baingana ambaye ni albino. Lakeisha akiwa ndotoni, anashuhudia mauaji ya mwanawe yanayofanywa na Bi. Saeeda Khan anayempiga Lakeisha kwa ubapa wa parange, huku wanaume wawili wakimkata Baingana viungo vyake vya mwili ili waende wakaviuze (uk. 183-184). Isitoshe, Lakeisha anashuhudia mwanawe ambaye tayari ni mfu na amezikwa, akifukuliwa na kukatwa viungo vya mwili na nyeti zake kama ulimi, mkono na kunyofolewa nywele. Hatimaye, Lakeisha anazinduka kutoka ndotoni. Mandhari hayo ni muhimu katika kukuza ujumbe wa dhuluma kwa mazeruzeru ambao wanauawa ili nyeti zao ziuzwe na kutumiwa katika shughuli za kishirikina hasa na wanasiasa.

Baada ya Baingana kumliwaza mamake kutokana na jinamizi; naye analala na anaota ndoto mbaya pia. Katika mandhari hayo ya njozini, Baingana anafukuzwa na Bi. Saeeda Khan kwa parange linalowaka moto. Watu wengi wanamfukuza wakidai yeye Baingana

(albino) ni *investment*. Wanapomkamata, wanampiga kama mbwa mwizi na anaanguka katika shimo pana. Punde, Baingana ndiye anayemfukuza Bi. Saeeda Khan, ambapo jaji wa mahakama ya Gehenna ‘anatokezea’ na kumhukumu Bi. Saeeda kifo bila ya kuruhusiwa kukata rufani (uk. 183-187).

Mwandishi anatumia mandhari haya kiubunifu kwa kuvunja mpaka wa kimwanda. Anatupeleka hadi wakati wa baada ya kifo cha binadamu. Kuhukumiwa kwa Bi. Saeeda na kutumbukizwa katika rusu ya *chhaldabius* kunakuza ujumbe kuwa, kila uovu unaotendwa ulimwenguni una adhabu yake Gehenna. Vilevile, mtunzi ameweza kueleza mateso na madhila yanayowakumba mazeruzeru katika jamii ulimwenguni. Mwanda unapanuliwa na wakati unafupishwa kupitia mandhari hayo ya kinjozi. Punde tu Baingana anapopigwa na umati, kwa kudai kuwa ni *investment*; safari ya Gehenna inaanza na mara Bi. Saeeda anahukumiwa na jaji wa mahakama ya Gehenna.

Mandhari ya kinjozi pia yanajitokeza pale ambapo gari la Mwalimu Baya linakwama kwenye reli. Tukio hili linafanyika katika akili au mawazo ya Mwalimu Baya anapokuwa amempa Mishi lifti ya kwenda Chumbageni usiku. Vokswageni ya Baya inapokwama relini na treni ikikaribia, Mishi anamkumbatia Baya na kutamka neno la kishetani ‘shemhamforash’. Matokeo ni kwamba, treni inapita ‘ndani yao’ bila ya kuwadhuru. Ni ajabu! Mwandishi anatumia mandhari hayo kukuza ujumbe wa kiajabu na kumsawiri mhusika Mishi; kwamba ni mhusika wa kimazingaombwe.

Mwishoni mwa hadithi, mwandishi anavunja kabisa mpaka wa kimwanda na kutupeleka katika mandhari ya baada ya kifo cha binadamu. Mandhari hayo ni ya Gehenna na yamo

katika fikra ya Bi. Saeeda Khan kama ilivyokuwa mwanzoni mwa hadithi. Katika mandhari hayo, kuna wahusika wawili wakubwa: Munkari na Nyamaume, na watu wa Gehenna. Munkari anawatolea mhadhara, *The Matrix of Corruption in Kiafra* ambapo anawafafanulia matendo maovu yanayowafanya watu kuingizwa Gehenna kwenye moto mkali usiozimika (uk. 219-242).

Mandhari hayo ni muhimu kwa sababu yanamwezesha mwandishi kufafanua bila kikwazo mambo yanayomfika binadamu baada ya maisha ulimwenguni kufikia mwisho. Anatuchorea wazi picha ya Gehenna, mahali ambapo watu wote wanaotenda dhambi wanaadhibiwa. Kuna moto mkali usiozimika milele. Kwa hivyo, mwandishi anatumia tukio hilo kama onyo kwa binadamu waovu waache kuwadhulumu na kuwanyanasa wenzao ulimwenguni.

Kwa kweli, hii ni mifano tu ya mandhari ya kinjozi katika *Watu wa Gehenna*.

### **4.3 MUUNDO WA USIMULIZI**

#### **4.3.1 Utangulizi**

Wataalamu tofauti wamefafanua dhana ya usimulizi kama ifuatavyo. Wales (1990:264) anasema kuwa, “Usimulizi ni kipengele cha mchakato mzima wa mawasiliano au diskosi/ usemi baina ya mwandishi na msomaji, na kati ya msimulizi na msimuliwa”. Nao Njogu na Chimerah (1999:47) wanasema: “Usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa

hadithi”; na Wamitila (2003:325) anaeleza ‘Usimulizi’ kama uelezaji wa matukio katika hadithi.

Kwa kawaida, hadithi haiwezi kumfikia msomaji bila ya kuwapo na usimulizi wa hadithi yenyewe. Uwasilishaji wa hadithi hutegemea nyenzo tofauti zikiwemo za kidrama, kifilamu, kishairi na kisimulizi. Katika kuchunguza usimulizi wa hadithi, mambo kadha ya kimsingi huzingatiwa: mtiririko wake, iwapo unafululiza au una mikatizo isiyokuwa ya kawaida; ni usimulizi wa moja kwa moja au ni changamano; aina ya usimulizi (wa nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu); usimulizi unavyofungamana na masuala yanayozungumziwa na athari zake katika uelewekaji wa kazi inayohusika (Wamitila 2008: 133-134). Kwa hivyo, usimulizi ndiyo njia kuu ya kuwasilisha kisa katika riwaya au kazi za kinathari, ingawa kuna majaribio ya kuwasilisha visa kwa njia ya mazungumzo.

Usimulizi katika *Watu wa Gehenna* ni changamano, si wa moja kwa moja. Kuna aina mbalimbali za usimulizi katika riwaya hii. Zifuatazo ni aina mbili za usimulizi ambazo zinazojitokeza riwayani humo.

#### **4.3.2 Usimulizi ngazi**

Huu ni usimulizi ambapo hadithi kuu ina vihadithi vingine vidogo vidogo (Wamitila 2003:325). Kuna hadithi kuu inayomhusu mhusika Eks Ngwenyama na matatizo yanayoikumba Kiafra na wana-kiafra kwa ujumla. Hata hivyo, kuna vihadithi vingine ambavyo vimeegemezwa katika hadithi hiyo kuu.

Katika sura za nne na tano kuna usimulizi wa hadithi ya MKUU anapomhoji Eks akiwa ameshakufa. Usimulizi huu unatokea katika mandhari ya kinjozi - baada ya kifo cha

binadamu. Usimulizi huu unaathiri ujumbe kwa kiasi kikubwa na pia kuchangia usawiri wa wahusika Eks na MKUU. Ujumbe wa uhalisiajabu unakuzwa pakubwa.

Katika sura za sita na saba vilevile, hadithi inabadilika. Usimulizi unamhusu Sikujua na Takosani binti Inatesh ambao wanakutana njiani na Sikujua anampenda Takosani kwa mara ya kwanza. Usimulizi huu unachangia pakubwa ujumbe wa uhalisiajabu. Usimulizi ngazi unajitokeza katika sura ya nane ambapo pana hadithi ya Krockoff van Akilimali na Siyawezi wanapozungumzia katiba kielelezo ya nchi mojawapo ya Kiafra.

Vijihadithi vingine ndani ya hadithi kuu ni kisa cha Mwalimu Baya na Mishi; cha Baadayadhiki na Faki Nahodha; cha maandamano ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kuhisika; na cha mlipuko wa jengo la *Gehenna Systems Centre* miongoni mwa hadithi nyingine.

#### **4.3.3 Usimulizi wa nafsi ya tatu.**

Pia huitwa usimulizi maizi. Usimulizi huu huwasilishwa na msimulizi asiye mmoja wa wahusika katika hadithi inayohusika. Hutambulishwa kwa mofu 'a'. Aghalabu, msimulizi 'huingia' katika akili ya mhusika na kueleza yaliyomo kwa njia ambayo anaiona yeye. Wakati mwingine, msimulizi anaweza kuwa 'nje' anatazama; na hata kubaki katika muktadha wa kinjozi wa wakati na mwanda. Vilevile, msimulizi anaweza pia kuwa katika muktadha tofauti na awe kila mahali na kujua yanayoendelea huko. Msimulizi huelezea matukio yanayomhusu mtu mwingine. Katika hali hii, lugha huwa inatumiwa kiubunifu kuwakilisha mitazamo hiyo tofauti ya matukio (Verdonk 2002: 42-43).

Kulingana na Wamitila (2008:124), usimulizi wa nafsi ya tatu hufuata mkondo unaodhihirisha ufahamu wa siri na mambo yote. Msimulizi maizi huwa na sifa za kuelewa kila kitu kinachowahusu wahusika, mandhari, hadithi, mwelekeo na mtazamo wa viumbe wa hadithini (Leech na Short 1981:266-267).

Usimulizi huu ndio unaopatikana kwa wingi katika kazi za kifasihi hasa riwaya na unawezesha kuwepo kwa mtazamo mpana wa matukio yanayopatikana katika ulimwengu wa kibunifu. Katika hadithi za kifantasia, msimulizi hutumia nafsi ya tatu kuelezea mambo ambayo ni vigumu kuyatazama au kuyashuhudia. Kulingana na wataalam Njogu na Chimerah (1999:47), msimulizi wa nafsi ya tatu ana uhuru mkubwa na anaweza kuingia popote atakapo na kuhisi kama wahusika wanavyohisi. Ndiye huwa mtawala wa hadithini.

Mwandishi wa *Watu wa Gehenna* ameutumia usimulizi huu kwa kiasi kikubwa ili kueleza matukio ya kiajabuajabu ambayo ni vigumu kuyatazama au kuyashuhudia katika hali ya kawaida. Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya usimulizi wa nafsi ya tatu katika riwaya inayohusika.

Katika sura ya kwanza, mtunzi anatumia usimulizi wa nafsi ya tatu kutusawiria mandhari ya Gehenna. Gehenna ina volkano nne zilizo juu ya milima minne yenye mabonde katikati. Hakuna tambarare na moto mkali unawaka daima. Kuna rusu nne ambamo binadamu wanaotenda dhambi wanaadhibiwa vikali kwa makosa yao. Watu wanaotumbukizwa humo wanajutia makosa yao. Mwandishi anatumia usimulizi huu kukuza ujumbe wa kiuhalisiajabu na hali za ahera.

Usimulizi wa nafsi ya tatu pia unatumiwa kueleza mlipuko wa jengo la *Gehenna Systems Centre* (GSC) ambapo ghorofa zote 999 zinadondoka chini. Usimulizi huu unatokea katika mandhari ya kinjozi ya mhubiri Yunasi anayefanya kazi katika jengo hilo. Watu zaidi ya elfu ishirini wanakufa huku Yunasi na mkewe, Saida wakinusurika kimiujiza. Tunaambiwa, ndege ya *Gehenna Airlines Flight 666* iliyokuwa ikielekea Fikirini kutoka Ziwa Sadiki ndiyo inayogonga jengo hilo. Usimulizi maizi unamwezesha mwandishi kutuelezea tukio hili la mlipuko ambalo ni nadra kuweza kulishuhudia. Kwa hivyo, anakuza ujumbe wake vilivyo kwa kutumia usimulizi maizi.

Vilevile, usimulizi wa nafsi ya tatu unatumiwa kuelezea kisa cha treni kupita 'ndani ya' gari (Vokswageni) la Mwalimu Baya (uk. 106-108). Gari linapokwama kwenye reli, Mishi anatamka neno 'shemhamforash' na treni iliyokuwa ikikaribia inapita 'ndani yao' bila ya kuwadhuru hata kidogo. Hakika, hiki ni kisa ambacho hakiwezi kushuhudiwa jinsi kinavyofanyika. Kwa hivyo mtunzi ameweza kukiwasilisha kwa wasomaji kupitia kwa njia ya usimulizi wa nafsi ya tatu.

Mwandishi pia ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu kutuelezea maumbile ya kiajabu ya mhusika Mishi. Anatueleza hivi:

Chumba kizima kilijazwa na mwangaza uliotoka ndani  
ya mwili wa binti huyo. Ulikuwa ni mwanga wenye  
rangi ya mbalamwezi angavu... Mishi alikuwa na Jicho  
moja kwenye paji la uso wake, huku mwili ukiwa nusu

toka juu hadi chini. Titi moja, mkono mmoja, mguu mmoja, nusu ya kila kitu. (uk. 117).

Haya ni maumbile ambayo ni nadra kuyashuhudia katika ulimwengu halisi. Ndiposa mtunzi ameyatia katika mandhari ya kinjozi na kutumia usimulizi wa nafsi ya tatu kuyaelezea. Anafaulu pakubwa kukuza na kuendeleza ujumbe wa uhalisiajabu na usawiri wa mhusika Mishi.

Ndoto za Lakeisha na Baingana zinasimuliwa katika nafsi ya tatu kuelezea matukio yanayowakumba na ambayo ni vigumu kuyashuhudia katika ulimwengu halisi. Msimulizi anatueleza jinsi mtoto wa Lakeisha anavyokatwa miguu yake kwa parange kali na kundi la Bi. Saeeda Khan; anazikwa lakini maiti inafukuliwa na kukatwa nyeti zake: mkono, ulimi na kunyofolewa nywele kichwani ili kwenda kuuzwa kwa faida (uk. 182-186). Mtunzi anafaulu kukuza ujumbe wa biashara ya miili ya maalbino na watu waovu wenye imani za kishirikina na nguvu za giza.

Wanajopo katika kipindi cha *The Night of the Living Dead* wanasawiriwa kupitia usimulizi wa nafsi ya tatu. Kipindi hiki kinafanyika katika akili ya Hikmat na wanajopo Ikmat, Kmat na Mat ni nakili za Hikmat. Msimulizi maizi anatueleza kuhusu wahusika hao na kuhusu mambo ambayo wanajadili (uk. 162-181). Bila ya usimulizi wa nafsi ya tatu, ingekuwa vigumu kuwasawiri wahusika-wanajopo katika kipindi hicho. Kwa hivyo, mwandishi anafaulu katika kukuza ujumbe na pia mtindo na hasa usawiri wa wahusika.

Tunapata kufahamu maisha ya utotoni ya Baingana na Siyawezi kupitia usimulizi huu wa nafsi ya tatu. Msimulizi anatueleza jinsi walivyoishi kwa furaha na wazazi wao, hadi pale

mama yao (Lakeisha) anapowatelekeza wakati anapompata mume tajiri kwenye mtandao wa *facebook*. Hali ngumu ya maisha ya 'kiyatima' inawafanya wawe wezi na wauza dawa za kulevya, lakini baadaye wanabadilika (uk. 190-195). Usimulizi huu unamwezesha mtunzi kutuwasilishia ujumbe kuhusu athari mbaya za utandawazi na kutowajibika kwa wazazi katika malezi ya watoto wao. Watoto ndio huteseka hatimaye.

Mwandishi pia anatumia usimulizi wa nafsi ya tatu kutuelezea kuhusu mauaji ya mhubiri Yunasi na mkewe Saida na watoto wao wawili. Mauaji hayo yanafanywa na Takosani binti Inatesh akiwa na Sikujua. Tunaelezwa kuwa, "walivunja kasha wakaiba bunduki aina ya *metal storm* na makasha mawili ya risasi." (uk. 215). Hatimaye, wanawaua akina Yunasi kwa kuwapiga risasi (uk. 212-218). Usimulizi huu unatumiwa kueleza matukio ambayo ni vigumu kuyashuhudia. Anafaulu kukuza ujumbe wa udhalimu na upinzani dhidi ya ukristo ulimwenguni.

Hakika, hii ni mifano michache tu ya jinsi usimulizi wa nafsi ya tatu ulivyotumiwa katika riwaya hii ili kukuza ujumbe wa mwandishi.

#### **4.4 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangazia vipengele viwili vya fani: mandhari na muundo wa usimulizi. Tumeshughulikia maana ya mandhari na kufafanua aina mbalimbali za mandhari yanayopatikana katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Tumetolea mifano mandhari ya kijiografia (mandhari halisi) na mandhari ya kinjozi kama yanavyojitokeza katika riwaya hii.

Vilevile, tumeangazia muundo wa masimulizi, kwa kueleza usimulizi ni nini. Tumefafanua aina mbili za usimulizi na kuitolea mifano mwafaka katika riwaya teule. Aina hizi ni usimulizi ngazi na usimulizi wa nafsi ya tatu.

Katika kutamatisha sura hii, tumebaini kuwa mandhari na usimulizi wenyewe umechangia pakubwa kukuza na kuendeleza maudhui ya uhalisiajabu katika *Watu wa Gehenna*. Mtunzi ameweza kutuwasilishia ujumbe kwa mnato na ambao isingewezekana pasina vipengele hivi kutumiwa.

## SURA YA TANO: HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunatoa mahitimisho ya utafiti wetu. Tunafanya hivyo kwa kutoa muhtasari wa yale tuliyoyatekeleza na kuyaibua katika uchunguzi huu kwa kurejelea madhumuni na maswali ya utafiti. Kisha, tumeshughulikia ufaafu wa nadharia katika utafiti huu na hatimaye tunatoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

### 5.1 Muhtasari wa utafiti wetu

Katika kazi hii, tulidhamiria kutekeleza madhumuni matatu.

Kwanza, tulidhamiria **kubainisha jinsi vipengele mahsusi vya mtindo vilivyotumiwa katika *Watu wa Gehenna* vinavyoathiri muundo wake**. Tumetekeleza dhamira hii katika sura za pili, tatu na nne ambapo tumejadili vipengele tulivyoviteua na kuvishughulikia vya uhusika na wahusika, tamathali za usemi, mandhari pamoja na usimulizi.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia kipengele cha uhusika na wahusika kwa kuonyesha mbinu zilizotumiwa kuwasawiri wahusika katika riwaya inayohusika na tukaeleza makundi ya wahusika hao wanaopatikana katika riwaya hii. Tumefafanua sifa na wasifu wa wahusika wakuu na wahusika wadogo tuliowateua huku tukiangazia aina zao, yaani iwapo ni duara, bapa, jumui au wa kinjozi.

Utafiti wetu umebaini kwamba, njia ya usawiri wa wahusika katika *Watu wa Gehenna* ni tofauti kabisa na usawiri wa kijadi (ambao unadhihirisha uhalisia wa kijamii). Usawiri

wao ni wa kinjozi hata ingawa kwa hali halisi wanawakilisha binadamu katika jamii. Tumbainisha kwamba, wahusika hawa wametumiwa kwa ufanifu mkubwa katika kuujenga mtindo wa riwaya hii. Lugha yao imefungamana na mazingira yao na hata elimu yao; wanajibizana katika mazungumzo na kwa njia hii kuakisi hali halisi. Vilevile, wamepewa matumizi yao maalum ya tamathali za usemi na mbinu za lugha pamoja na msamiati.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia tamathali za usemi katika kiwango cha kisemantiki. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo tumechanganua ni sitiari, jazanda, tashbihi, kinaya / kejeli, taswira, tashihisi na maswali ya kibalagha pamoja na takriri. Utafiti wetu umeonyesha majukumu makubwa yaliyotekelezwa na mbinu hizi katika kujenga mtindo wa riwaya tunayoishughulikia.

Katika sura ya nne, utafiti wetu umeshughulikia vipengele vya mandhari na usimulizi. Tumeangazia aina mbili tu za mandhari katika riwaya inayohusika: mandhari halisi na mandhari ya kinjozi. Vilevile, tumeangazia usimulizi uliotumiwa katika *Watu wa Gehenna*: usimulizi ngazi na usimulizi wa nafsi ya tatu. Utafiti wetu umeonyesha kuwa, usimulizi umetegemea lugha kwa kiasi kikubwa, na, pamoja na mandhari vimewezesha mwandishi kuujenga mtindo wa kazi yake.

Lengo letu la pili katika utafiti huu lilikuwa **kuchunguza jinsi mtindo wa *Watu wa Gehenna* unavyoathiri uwasilishaji wa ujumbe**. Tumetekeleza dhamira hii katika sura za pili, tatu na nne vilevile. Katika sura ya pili, utafiti wetu umebaini wazi kwamba usawiri wa wahusika katika riwaya hii umewezesha mtunzi kuwasilisha maudhui

mbalimbali katika hadithi. Kupitia wahusika hasa wa kinjozi, tunapata kufahamu maudhui ya biashara haramu ya nyeti za mazeruzeru, ufisadi na uongozi mbaya, athari mbaya za utandawazi pamoja na kudhulumiwa kwa wafanyakazi wa nyumbani. Haya yote yamewezekana kupitia wahusika wa aina mbalimbali na mwandishi amefaulu kutuwasilishia matukio ya kiajabuajabu kupitia wahusika wa kinjozi.

Katika sura ya tatu, mwandishi amewasilisha ujumbe wake kupitia tamathali za usemi. Utafiti huu umebaini kwamba, mtunzi ameteua tamathali za usemi kwa njia ya kipekee ili kuendeleza maudhui mbalimbali katika *Watu wa Gehenna*. Mbinu hizi zimeathiri maana katika uwasilishaji dhamira na maudhui mbali na kuondoa uzoevu wa matumizi ya lugha.

Hatimaye katika sura ya nne, vipengele vya mandhari na usimulizi vimesaidia katika kuwasilisha ujumbe. Utafiti wetu umebaini kwamba, mwandishi ameweza kuwasilisha maudhui mazito kama mauaji na biashara ya nyeti za maalbino na adhabu ya Gehenna kupitia mandhari ya kinjozi na usimulizi hasa wa nafsi ya tatu. Masuala mengi yasingewasilishwa katika muktadha wa kawaida. Utafiti huu umebaini kuwa, mandhari yamechangia pakubwa uwasilishaji wa maudhui na kuuendeleza usimulizi wa hadithi. Mandhari ya kinjozi kwa mfano, yamemwezesha mwandishi kuelezea mazingira ya kiajabuajabu pamoja na miujiza mingi bila ya kikwazo chochote. Amefaulu kuufafanulia umma matatizo yanayoathiri nchi na ulimwengu kwa jumla.

Lengo la tatu la utafiti wetu lilikuwa **kuchanganua mtindo wa riwaya husika ili kuiainisha riwaya hiyo**. Dhamira hii tumeitekeleza katika sura za pili, tatu na nne. Kama

tulivyofafanua tayari, utafiti wetu umebaini kuwa riwaya tunayoishughulikia ni ya uhalisiajabu au ya kimajaribio. Kuna ukiushi wa kaida zilizozeleka za utunzi wa riwaya.

Kwanza usawiri wa wahusika ni tofauti na wa kijadi. Mtunzi anamtumia mhusika jumui ambapo Eks Ngwenyama anachukua majukumu ya wahusika wengi tofauti katika hadithi nzima. Pia kuna wahusika wa kiungu kama MKUU, Mzee Afisul na malaika (Munkari) ambao wanatumiwa na mtunzi kukuza ujumbe wake. Vilevile kuna matukio mengi ya kiajabuajabu ambayo yanawasilishwa kupitia mandhari ya kinjozi na usimulizi maizi.

Utafiti wetu pia umebaini kuwa mandhari yaliyotumiwa ni ya kinjozi na yamewezesha msimulizi kuwasilisha ujumbe kupitia usimulizi wa nafsi ya tatu. Kuna mvunjiko wa kisimulizi ambapo matukio hayafuatani moja kwa moja; ploti ni changamano. Hali hizi ni tofauti na zilivyo katika riwaya halisi ambapo maudhui aghalabu ni ya kimaadili, wahusika ni halisi na usimulizi huwa wa moja kwa moja, si changamano.

## **5.2 Ufaafu wa Nadharia**

Tulitumia nadharia mbili katika utafiti wetu: Nadharia ya Umitindo na Nadharia ya Uhalisiajabu. Nadharia hizi zimetufaa katika kuchanganua mada ya utafiti wetu ambayo ni, 'Mtindo katika *Watu wa Gehenna*'.

Nadharia ya Umitindo imetusaidia kuchanganua vipengele vya kisantiki hususan tamathali za usemi, na kutuwezesha kuchanganua mtindo katika riwaya tunayoishughulikia. Mwandishi ametumia sitiari, jazanda, tashbihi na taswira miongoni mwa mbinu nyingine. Vilevile, kupitia kigezo cha mazungumzo, tumeweza kubainisha

kwamba, usawiri wa wahusika umekuza mtindo pamoja na kuathiri uwasilishaji wa ujumbe katika riwaya inayohusika. Mwandishi amewapa wahusika matumizi ya lugha teule na kuwasawiri kwa ubunifu mkubwa.

Nadharia ya Uhalisiajabu imetufaa katika kuchunguza mandhari, usimulizi na wahusika katika *Watu wa Gehenna*. Utafiti wetu umebainisha kwamba, kuna matukio mengi ya kiajabuajabu hasa kutokana na kujengeka katika mazingira ya kimazingaombwe pamoja na usawiri wa wahusika wa kinjozi. Ndoto na uhalisia vimechanganyika ambapo uchunguzi wetu umebainisha mandhari ya kinelibini. Kuna mvunjiko wa kisimulizi; matukio hayafuatani kimantiki. Utafiti wetu umebainisha pia kwamba, wakati na mwanda vimepanuliwa katika usimulizi wa riwaya hii. Mwandishi amefaulu kuwasilisha matukio yaliyotendeka miaka mingi iliyopita kupitia mbinu rejeshi na hata matukio yatakayotendeka miaka ijayo na hasa baada ya maisha ya binadamu ulimwenguni. Kwa hivyo, kwa kuupanua mwanda, mandhari tofauti yamebainika wazi na kuwezesha ukuzaji na uwasilishaji wa ujumbe.

Kupitia mihimili hii ya Nadharia ya Uhalisiajabu, matokeo ya utafiti wetu yameonyesha kuwa, riwaya ya *Watu wa Gehenna* ni ya uhalisiajabu. Kwa hivyo, nadharia tulizozitumia katika utafiti wetu zimekuwa za manufaa katika kufanikisha utekelezaji wa mada yetu ya utafiti.

### **5.3 Mapendekezo ya tafiti za baadaye**

Ni maoni na matumaini yetu kwamba, utafiti huu utawapa mwongozo mzuri wasomaji wa *Watu wa Gehenna* na riwaya nyingine za kimajaribio katika fasihi ya Kiswahili. Hata

hivyo, tunatambua na kukiri kwamba, uchunguzi huu unahusu sehemu ndogo tu japo muhimu. Katika utafiti wetu, tumeshughulikia baadhi ya vipengele vya mtindo katika *Watu wa Gehenna*. Tumechanganua uhusika na wahusika, tamathali za usemi, usimulizi na mandhari.

Ni mapendekezo yetu kwamba, tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza maudhui katika riwaya hii. Vilevile, utafiti unaweza kufanywa kuhusu vipengele vingine vya fani kwa kutumia nadharia tofauti na hizi mbili tulizozitumia.

## MAREJELEO

- Bakari, M. (2011) “Usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi *Sadiki Ukipenda* (2002)”. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.
- Carpentier, A. (1979) *The Lost Steps*. Harmondsworth: Penguin Books.
- Chapman, R. (1973) *Linguistics and Literature: An Introduction to Literary Stylistics*. London: Edward Arnold.
- Cooper, B. (1998) *Magical Realism in West African Fiction: Seeing with a Third Eye*. New York: Routledge.
- Crystal, D. & D. Davy, (1969) *Investigating English Style*. London: Longman Group.
- Crystal, D. (1997) *Dictionary of Linguistics and Phonetics*. 4<sup>th</sup> Edition. Blackwell: Oxford.
- Guenter, I. (1995). “Magic Realism in the Weimar Republic”. In Zamora P.L. and Faris W.B. (1995) *Magic Realism: Theory, History, Community*. London: Duke University Press.
- Hawthorn, J. (2001) *Studying the Novel, 4<sup>th</sup> Edition*. London: Arnold Publishers.
- Indangasi, H. (1988) *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Kezilahabi E. (1990) *Nagona*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

- Kitsao, J. (1975) "A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts". Tasnifu ya Uzamili (M.A): Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Nairobi: E.A.L.B.
- Leech, G.N. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.
- Leech, G.N. & Short M.(1981) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose 2<sup>nd</sup> Edition*. Harlow: Longman Group Ltd.
- Llosa, M.V. (1966) *The Green House*. New York: Harper and Row.
- Lugwiri, P.O. (2011) "Sitiari, Taashira na Tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka: Uhakiki wa Kimtindo*". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Marquez, G.G.(1998) *One Hundred Years of Solitude*. London: Everyman's Library.
- Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text-books Graphics and Publishing.
- McIntosh, A. (1963) "Language and Style" In Pride, J.B. & Holmes, J. (eds). (1984), *Sociolinguistics*. Harmondsworth: Penguin Books.
- Mohamed, S.A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: E.A.E.P. Ltd.

- \_\_\_\_\_ (2001) *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- \_\_\_\_\_ (2006) *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.
- Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: E.A.E.P. Ltd.
- Mugwika, F.K. (2012) “Dhana ya Uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba*”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Murray, P. (1978) *Literary Criticism: A Glossary of Major Terms*. New York: Longman Ltd.
- Ngara, E. (1982) *Stylistic Criticism and the African Novel*. London: Heinemann.
- Njogu, K. na Chimerah R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyabunga, V.A. (2005) “Uhakiki wa *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) za K.W. Wamitila”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Olali, T. (2008) *Mafamba*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- \_\_\_\_\_ (2010) “Structure and Anti-Structure of Swahili novel: A Stylistic Analysis of *Babu Alipofufuka*” katika *The Nairobi Journal of Literature* (Na. 6 ya mwaka 2010).

- \_\_\_\_\_ (2012) *Watu wa Gehenna*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Omar, S.M. (2012) “Uchambuzi wa Tamathali za Usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Ongarora, S.O. (2007) “Mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Onyoni, J.K. (2012) “Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala na Mama Ee*”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Quirk, R. *et al.* (1985) *A Comprehensive Grammar of the English Language*. London: Longman.
- Rushdie, S. (1981) *Midnight’s Children*. London: Jonathan Cape.
- \_\_\_\_\_ (1988) *The Satanic Verses*. United Kingdom: Viking Press.
- Simpson, P. (2004) *Stylistics: A Resource book for Students*. London: Routledge.
- Sorensen, L. (ed.) (2000) “Wittkower, Rudolf.” *Dictionary of Art Historians*. Retrieved November 27, 2000.
- TUKI (2006) *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Toleo la Tatu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

- Verdonk, P. (2002) *Stylistics*. London: Oxford.
- Wafula, R.M. na Njogu K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: JKF.
- Wales, K. (1990) *A Dictionary of Stylistics 2<sup>nd</sup> Edition*. London: Pearson Education Ltd.
- Wamitila, K.W. (1999) *Nguvu ya Sala*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2002a) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2002b) *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.
- Zamora, P.L. na Faris W.B. (1995) *Magical Realism: Theory, History, Community*. London: Duke University Press.